Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Nne – Tarehe 24 Aprili, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

*D U A*

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati ifuatazo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 *(The Annual Report and Accounts of the Surface and Marine Transport Regulatory Authority for the Financial year 2006/2007).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 40

**Udhibiti wa Mahesabu na Watendaji wa Halmashauri za Wilaya**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa karibu Halmashauri zote za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji zimeanza kutengeneza vizuri vitabu vyao vya mahesabu na kupata Hati safi na kwa kuwa Kamati ya *LAAC* kwa kushirikiana na *CAG* na TAMISEMI ilipofanya ziara kwenye Halmashauri mbalimbali iligundua kwamba mahesabu yaliyoonyeshwa kwenye vitabu ni tofauti kabisa na miradi inayotekelezwa kwenye maeneo husika, na kwamba miradi mingi kwenye baadhi ya Wilaya inatekelezwa kwa kiwango cha chini tofauti na miongozo ya Serikali:-

(a) Je, kwa nini Serikali isitenge fedha zaidi kwa ajili ya kufanya *Value for Money Audit* na *Performance Audit* badala ya kupitia vitabu tu?

(b) Je, Serikali inasemaje juu ya watendaji mbalimbali (Wakuu wa Idara) ambao wamekaa kituo kimoja kwa muda mrefu?

(c) Je, Serikali itamalizaje tatizo la Wakuu wa Idara Kukaimu kwa muda mrefu zaidi ya miezi sita kama miongozo inavyoelekeza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Halmashauri zetu kwa sasa zimeanza kutengeneza vizuri vitabu vyao vya Mahesabu na kupata Hati Safi. Hata hivyo wakati mwingine mahesabu yanayoonyesha kwenye vitabu ni tofauti na miradi inayotekelezwa kwenye maeneo husika, na kwamba miradi mingine kwenye baadhi ya Halmashauri inatekelezwa kwa kiwango cha nini tofauti na miongozo ya Serikali.

Serikali ilishaliona tatizo hilo na ndiyo maana kuanzia mwaka 2007/2008 ukaguzi wa hesabu za Halmashauri ulihusisha pia ukaguzi wa miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ili kujiridhisha na vyote, usahihi wa mahesabu, miradi inayotekelezwa pamoja na thamani ya fedha iliyotumika kutekeleza miradi hiyo. Serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa Mkaguzi na Mdhbiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ili utaratibu huu wa ukaguzi wa miradi ya maendeleo uwe endelevu. *(Makofi)*

Aidha Ofisi yangu inavyo vitengo vya Ukaguzi (*inspection*) na ufuatiliaji na tathimini *(Monitoring and Evaluation)* ambavyo vimekuwa vikifanya ukaguzi na ufuatiliaji wa uendeshaji wa shughuli za mamlaka za Serikali za mitaa ikiwemo namna miradi ya maendeleo inavyotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kwa kuanzisha utaratibu wa kuzitembelea Halmashauri siyo tu kwa lengo la kujiridhisha na taarifa zilizotolewa kama zinaendana na hali halisi, bali pia kujiridhisha kama utekelezaji wa shughuli za Halmashauri unazingatia thamani halisi ya fedha *(Value for Money).*

(b)Mheshimiwa Spika, kufanya kazi katika kituo kimoja kwa muda mrefu siyo tatizo, isipokuwa wakati mwingine inaweza kuathiri utendaji kutokana na mtumishi kuzoea sana kituo na hivyo kufanya kazi kwa mazoea. Inapotokea hali kama hiyo njia mbalimbali hutumika ili kumrekebisha mtumishi wa aina hiyo.

Njia hizo huanzia kwa mwajiri wake ambaye ni Halmashauri husika kwa kumchukulia hatua za kinidhamu na hatua za kisheria. Serikali wakati mwingine humbadilishia kituo mtumishi huyo pale inapoamini kuwa njia hiyo itafaa zaidi. Njia hii imekuwa haitumiki zaidi kwa kuwa ni gharama kubwa kumhamisha mtumishi kutoka

kituo kimoja kwenda kituo kingine, badala yake uchukuaji wa hatua za kinidhamu na za kisheria ndio njia ambazo zimekuwa zikitusaidia kuwarekebisha watumishi wa aina hiyo.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa baadhi ya Halmashauri, baadhi ya Wakuu wa Idara hukaimu kwa muda mrefu pengine hata zaidi ya miezi sita. Mtumishi anayezungumziwa katika miongozo ambaye hatakiwi kukaimu kwa muda wa zaidi ya miezi sita ni yule ambaye ana sifa zote za kushika nafasi inayokaimiwa. Sifa hizo ni pamoja na kiwango cha elimu alicho nacho na uzoefu wake kazini.

Kama inatokea nafasi fulani inakaimiwa na mtumishi ambaye hana sifa zote za kuwa Mkuu wa Idara husika, basi mtumishi huyo atatakiwa kuendelea kukaimu hata kama ni kwa zaidi ya miezi sita na ni yule ambaye ana sifa zote za kushika nafasi inayokaimiwa.

Kama inatokea nafasi fulani inakaimiwa na mtumishi ambaye hana sifa zote za kuwa Mkuu wa Idara husika basi mtumishi huyo atatakiwa kuendelea kukaimu hata kama ni kwa zaidi ya miezi sita mpaka ama atakapokuwa na sifa zote au atakapopatikana mtumishi mwingine mwenye sifa zote. Hata hivyo Serikali imekuwa ikijitahidi kutafuta watumishi wenye sifa zinazotakiwa na kujaza nafasi za Wakuu wa Idara katika Halmashauri ambazo ziko wazi au zimekuwa zinakaimiwa.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *CAG* ameanzisha kitengo cha *Value for Money in Performance Audit* na anao watalaam wote na kwa kuwa kwenye Mheshimiwa Spika, kwenye Kamati yake ya *LAAC* amewateua watalaam wote wakiwemo Mainjinia wataalam wa mahesabu na wengineo.

(a)Je, ni lini TAMISEMI itaanzisha kitengo kama hiki ili kuongeza nguvu kwenye Kamati hii na waanze kufuatana na Kamati pamoja na wataalam wa *CAG* kukagua miradi?

(b)Kwa kuwa tumeshagundua kwamba sasa hivi vitabu ni vizuri lakini utekelezaji kule si mzuri kama unavyotakiwa. Je, Serikali sasa iko tayari kuwasiliana na Spika ili Kamati hii iwe inatumia muda mrefu kukagua miradi kule Wilayani badala ya kukaa na kuangalia vitabu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu huu anaozungumzia wa kwamba tumejaribu kupata watalaam wa aina mbalimbali katika eneo hili la *CAG* na utaratibu huo pia kwamba wewe Mheshimiwa Spika, umekuwa unautumia ni utaratibu ambao ni mzuri natambua kwamba Mheshimiwa Mgana Msindai alikuwa Mwenyekiti *Local Authorities Account Committee* na mimi nilikuwa Mjumbe katika Kamati hii na natambua kwamba yeye ni Makamu Mwenyekiti, mpaka sasa hivi tunavyozungumza. Kama nilivyoeleza Wizara tumekuwa na utaratibu huo wa kuwa na ukaguzi wa ndani. Sasa kama ni suala la kuchukua *mode* hiyo na kuingiza katika utaratibu wetu kwa maana ya *structure* zile ambazo zimechukua na watalaam wa aina hiyo, mimi sioni kabisa

kwamba kuna tatizo lolote la kufanya hivyo kwa sababu kufanya hivyo tunafanya mambo yetu yaweze kuwa ya makini zaidi na ku-*create efficient.*

Mheshimiwa Spika, la pili, kwanza nashukuru sana kwamba Mheshimiwa Mgana Msindai pamoja na Kamati yao wamekuwa wanafanyakazi nzuri sana na kwamba hapa tulipofika sasa hivi kwa kweli tumeweza kufika kwa sababu Kamati ya *Local Authorities Accounts Committee* imechukua hatua hii ya kutokukaa Dar es Salaam na Dodoma na kupokea tu taarifa pale na kuishia hapo hapo. Utaratibu huu ni utaratibu mzuri. Sasa wamekwenda, na wanakwenda kwenye miradi na kwenda kujionea thamani halisi ya miradi ile kule ilipo ndiyo maana unaona taratibu ripoti inayokuja hapa inayoonyesha kwamba kazi nzuri imefanyika kule. Nichukue nafasi hii kwa kweli kuipongeza sana Kamati yetu ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa kazi nzuri ambayo inafanya. (*Makofi*)

Kwa hiyo, sasa suala la kuwasiliana na wewe ili tuzungumze tuone uwezekano wa kufanya muda wanaokaa kule ni mimi sina tatizo mimi ninachojua ni suala la bajeti kama itaruhusu. Lakini sisi tunalichukua hilo tutawasiliana na wewe Mheshimiwa Spika, na kwa vile unasikia nikiambiwa hivi hapa matumaini yetu ni kwamba utatusikiliza. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Hilo naafiki kabisa! (*Makofi*)

**MHE. ROSEMARY KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati hizi tatu *PAC, POC* na *LAAC* bado zimeonekana hazina meno ya kutosha kwa kutoweza kuwashughulikia watendaji wabovu ambao wamekuwa hawawakilishi risiti za mahesabu yao kwenye vitabu vyao. Sasa Serikali haioni kwamba ipo haja ya kuleta msaada wa Sheria ambapo Kamati hizi zote tatu zitakuwa na polisi wakati wa kukagua vitabu hivi ili watendaji wote wabovu watakaonekana hawajawasilisha mahesabu yao vizuri waweze kukatwa na polisi hapo hapo watakapokuwa wanahojiwa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Hii inaitwa instant justice. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, hapa zinazungumzwa Kamati mbalimbali inazungumzwa *PAC, POC,* na *LAAC*. Labda niseme jambo moja kwamba hizi Kamati zote wakati zinafanyakazi yake, cha kwanza ni kwenda kuchukua taarifa ile ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na wanapitia na kuangalia mapungufu yot eyaliyotokea pale na kama Kamati hii zinaona kwamba kwa kuna mapungufu hayo kamati hizi zinafanya kwanza kuwasiliana na zile mamlaka zote zinazohusika ikiwemo Bunge lenyewe hapa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ndiyo maana sasa hivi tunavyozungumza iko taarifa ambayo italetwa hapa ambayo itaonyesha hali halisi iliojitokeza kwa maana ya ukaguzi uliofanyika katika maeneo hayo. Mheshimiwa Kirigini anazungumzia suala la kwamba hizi kamati ziwe zinafuata na polisi mimi nadhani tumejiwekea utaratibu wa kugawana majukumu kwa kweli kusema kwamba hapa tutatoka hapa kila wakati *LAAC* inapokwenda inafuatana na askari hapo hapo itakuwa siyo sahihi kwa sababu ziko taratibu ambazo zimewekwa ambazo zinaweza zikafuatwa na wakati huo huo zikachukuliwa kwa wale ambao wanaonekana kwamba wamefanya makosa. Nashindwa kusema hapa kwamba kwa niaba ya Serikali tutasema

kwamba twende polisi kule kwa kweli kwa sababu taratibu hazituwezeshi kufanya hivyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Pia ukishakubali hivyo itabidi siku nyingine sasa uende na hakimu na afisa Magereza wa Wilaya.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baadhi ya watumishi wamekuwa wakikaa kwenye kituo zaidi ya miaka 15 bila kuhamishwa wakati huo huo wengine wamekuwa wakihamishwa kituo kimoja na kingine mara kwa mara. Wale wasiohamishwa mara nyingi katika ofisi yako ndipo panapofanyika manuvour ya kubadilisha kuwahamisha. Je, suala hili, utalirekebeshaje katika ofisi yako kwa sababu lipo na mimi nina ushahidi ukihitaji kuupata?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu hapa kwamba utaratibu wa kuhamisha watumishi katika maeneo mbalimbali ni utaratibu ambao unatumika Serikalini na utaratibu ambao umekusudiwa kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi.

Wakati mwingine mtumishi anaweza akakaa miaka 15 kama anavyosema. Liko lile tatizo tulilolisema hapa kwamba anaweza akawa anafanyakazi vizuri lakini akawa amezoeleka na kwa hiyo, labda ufanisi pale ukaacha kupatikana.

Katika hali ya namna hiyo tunapobaini kwamba kuna tatizo la namna kwamba kuna mtumishi ambaye ana utalaam wa kutosha anafanyakazi yake vizuri lakini sasa anashindwa kuleta ufanisi basi tunashauriana na tunafika mahali tunamhamisha.

Sasa kuna jambo limezungumzwa hapa ametumia neno *manuvour, manuvour* ni kufanya kidogo ambacho hakiko katika utaratibu hivi. Mtu anakaa miaka miwili, mwaka mmoja halafu anapitapita anakuja TAMISEMI anakwenda kwa Halmashauri halafu mnambadilisha. Mimi ningemuomba Ponsiano Nyami kwa sababu anao ushahidi wa Manuvour hiyo awasiliane na sisi atupatie.

Sisi tukikuta kwamba kuna *manuvour* zimefanyika namna hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu anasikia hapa na sisi wote tunasikia hapa tutachukua hatua zinazotakiwa. Nataka kurudia tena kwamba neno *manuvour* ni kitu kinachofanyika ambacho ni kinyume kinyume hivyo. Kwa hiyo, hiyo ndio tunaitafuta.

Na. 41

**Ruzuku kwa Serikali za Vijiji na Mitaa**

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali hutoa ruzuku kwa Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji kupitia TAMISEMI ili kufidia kodi zilizofutwa; na kwa kuwa kiasi cha asilimia ishirini

(20%) hutakiwa kupelekwa Serikali za Vijiji na Mitaa ili kusaidia Miradi ya Maendeleo katika maeneo hayo:-

(a)Je, TAMISEMI inaelewa kuwa kuna baadhi ya Halmashauri hazipeleki fedha hizo kwenye Serikali za Vijiji na Mitaa?

(b)Je, TAMISEMI inaelewa kuwa kuna baadhi ya Halmashauri kutokana na mapato ya ndani hazipeleki ile asilimia 10 kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake asilimia 5 na Mfuko wa Vijana asilimia 5?

(c)Je, TAMISEMI inazichukulia hatua gani Halmashauri zisizotekeleza matakwa haya kwani zinarudisha nyuma maendeleo katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Laus Omar Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo;-

(a) Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kufuta kodi zenye kero zilizokuwa zinatozwa na Halmashauri imekuwa ikitoa ruzuku kufidia kodi zilizofutwa. Serikali pia ilitoa maelekezo kwa Halmashauri zote nchini kulipa asilimia ishirini (20%) ya fedha hizo za fidia kwenye Serikali za Vijiji.

Halmashauri nyingi zimejitahidi kupeleka fedha hizo vijijini, baadhi ya Halmashauri zimekuwa zinatoa aidha kiasi kidogo tu au hazitoi kabisa bila kuzingatia maelekezo ya Serikali. Hili ni kosa kubwa kwa upande wa Halmashauri.

Napenda kuchukua nafasi na fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge ambao pia ni Madiwani kwenye Halmashauri zao kupitia Mabaraza yao kuhakikisha fedha hizi zinapelekwa vijijini bila visingizio vyovyote vile.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mwaka 2006/2007 asilimia 60 ya Halmashauri zote yaani Halmashauri 73 zilizingatia maelekezo na asilimia 17 yaani Halmashauri 20 ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe hazikuzingatia kabisa maelekezo yaliyokuwa yametolelwa. Mwaka 2007/2008 asilimia 43 yaani Halmashauri 51 zilizingatia maelekezo ya Serikali.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishaziagiza Halmashauri zote nchini kuchangia asilimia kumi (10%) ya mapato yao (*own source)* kwenye Mfuko wa Wanawake na vijana na siyo asilimia 5 kwa ajili ya Watoto kama alivyosema Mheshimiwa Mhina. Ni kweli kwamba baadhi ya Halmashauri zimeshindwa kuchangia kulingana na maelekezo ya Serikali. Fedha hizi ni kwa ajili ya kukopesha vikundi vya Wanawake, Vijana ili kuwasaidia kuondoa umaskini. Halmashauri inayopuuza kuchangia

fedha hizi siyo tu inapuuza maelekezo ya Serikali bali pia inapuuza maelekezo yaliyotolewa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

(c) Mheshimiwa Spika, Halmashauri itakayoshindwa kutekeleza agizo la kupeleka asilimia 20 kwenye vijiji hupewa adhabu ya kukatwa alama ya ufaulu wa kupata fedha za ruzuku za maendeleo. Aidha, Halmashauri inayopuuza kutekeleza maagizo ya kuchangia asilimia 10 kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake na Vijana hulazimika kuliweka hilo kama deni, yaani kama hukupeleka inatakiwa uliweke kama deni.

Kama nilivyojibu swali la 147 la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani katika Mkutano wa Nane wa Bunge lako Tukufu tarehe 5 Julai, 2007, kwa mara nyingine tena naziagiza Halmashauri ambazo hazijachangia kikamilifu kutekeleza maagizo hayo ya kutenga asilimia kumi (10%) ya mapato yake kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake na Vijana na kutoa asilimia 20 ya fedha za ruzuku za fidia ya mapato na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji Ofisini kwangu kila baada ya miezi mitatu.

Aidha, natoa wito kwa vikundi mbalimbali vya Vijana na Wanawake vinavyokopa virejeshe mikopo yao kwa wakati ili wenzao waweze kukopeshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena napenda kuchukua fursa hii ya kipekee kuishukuru sana Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa kuhimiza Halmashauri na kuhakikisha kuwa madeni ya Mfuko huu kutoka Halmashauri na kwa wakopaji yanalipwa.

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na kuipongeza Halmashauri yangu ya Korogwe kwamba imetekeleza kwa malipo hadi kufikia shilingi milioni 8. Nataka nieleze wazi kwamba kuna Halmashauri nyingine ambazo hazijatekeleza agizo hilo hadi kufikia shilingi milioni 300. Sasa kuna uwezekano kweli wa Halmashauri hizi kupeleka fedha hizi kwa wadau na kama zitashindwa kufanya hivyo, je, hatuoni kama zinadidimiza maendeleo ya wale wadau wenyewe? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Laus Mhina ametoa mpaka takwimu hapa kwamba kuna Halmashauri ambazo hazikutoa na fedha hizi zimefikia karibu shilingi milioni 300 na hivyo kuonyesha wasiwasi kwamba itakuwa kuzilipa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa imekuwa ikifanya kazi kubwa sana. Kwanza, utaratibu huo kwamba hawazipeleki hizo fedha na zimekuwa kiasi kikubwa kiasi hicho na kama hawafanyi hivyo maana yake wamefanya faulu pale, na kwa hiyo watapata hati chafu sasa. Kwa sababu anapokwenda mkaguzi pale anachokagua pale ni kuhakikisha kwamba hiyo asilimia 10

kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake na Vijana inatengwa. Sasa amesema kwamba kuna kiasi hiki kinaonekana hakijalipwa mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, jitihada inayofanyika ni kuhakikisha kwamba Halmashauri hizi zinatoa na kupeleka hizo fedha kama zilivyoelekezwa, na ndiyo maana hata sisi wenyewe kama Wizara tumekuwa na utaratibu huo wa kuuliza na tunataka ripoti kila baada ya miezi mitatu atwambie kwa maana wasipopeleka hizo fedha kwa ajili ya Wanawake na Vijana, hata huo mpango tulionao wa kuhakikisha maisha bora kw Watanzania inawezekana hautawezekana.

Kwa hiyo, nataka nichukue takwimuh hizi na tutakwenda kuzifanyia kazi, lakini nimekwishatoa maelekezo hapa kwamba Serikali inaagiza Halmashauri zote zihakikishie kwamba zinatenga asilimia 10 kwa ajili ya Wanawake na Vijana na zile asilimia 20 ambazo zinaenda pale kama fidia kwa ajili ya ile kodi ambayo ilikuwa inaonekana ni kero ziweze kupelekwa.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa, makosa mengi yanayofanyika na hasa hizo asilimia 20 za kwenda Vijiji na Mitaa ni kwa sababu Madiwani huwa hawaelewi sheria nyingi na maagizo mengi, na bahati mbaya inatokea saa nyingine na sisi Madiwani Wabunge tunakuwa hatuelewi. Je, kuna utaratibu gani wa kusaidia hao Madiwani waelewa ili waweze kusaidia Halmashauri hizi na kuwachukulia hatua wale Wakurugenzi ambao wanafanya makusudi ku-*reallocate* hizo fedha? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, sisi sasa hivi tunazo hela zinazopelekwa katika Halmashauri asilimia 40 kwa ajili ya kujenga uwezo, na asilimia hiyo 40 imekusudia kutoa semina kwa ajili ya Madiwani wetu pamoja na Waheshimiwa Wabunge waliopo katika Halmashauri zetu. Kwa hiyo, suala la kwamba hao Madiwani wanaonekana hawaelewi sheria, wengi sasa hivi kwa kweli walio wengi wanaelewa sheria hizi na taratibu hizi wanazifahamu. Kwa sababu lipo hilo fungu ambalo ninalizungumza hapa, pale kwenye Halmashauri inabakia asilimia 60 na kule kwenye vijiji na maeneo yale ya kwenye Kata tunawapelekea asilimia 40.

Sasa ile asilimia 60 inayobaki pale kwenye Halmashauri imekusudiwa isaidie kuwafanya Madiwani wetu waweze kuona na kuzitafsiri vizuri sheria hizi zinazozungumzwa hapa, na watumishi kwa maana ya Mkurugenzi Mtendaji ambaye ameelekezwa kwamba apeleka hizi fedha asilimia 20 zinazotakiwa kwenda kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hapa kwamba hizi asilimia 20 zinazozungumzwa hapa hazipelekwi kule kwa ajili ya shughuli za maendeleo wao wenyewe wakiamua kufanya hivyo ni sawa, hizi asilimia 20 ambazo zinazungumzwa hapa!

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, niwie radhi kidogo. *Sergeant at Arms* ningeomba ndugu zetu watu wenye ulemavu kwa ruksa ya Spika wengine wakae *Speaker's Gallery* kwa sababu sasa *Galleries* zote zimejaa. Endelea. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nilichokuwa ninaeleza hapa ni kwamba hiyo asilimia 20 tunayoizungumza hapa ndiyo ile ambayo tunasema wakati mwingine mnaweza mkamtolea sasa pale Mwenyekiti wa Kijiji posho yake kidogo pale. Kwa kweli fedha zile ndizo zinazotumika kwa ajili ya shughuli za kuendesha ofisi wala hazikukusudiwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Sasa kama kuna Mkurugenzi Mtendaji ambaye hapeleki fedha huko maana yake kwamba shughuli zinakwama pale kwa sababu hizi fedha ndizo zinazotumika kwa ajili ya kuendesha shughuli katika vijiji vyetu na katika zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, narudia tena kusema hapa kwamba sisi tutachukua hatua za kinidhamu popote pale ambapo inaonekana kwamba fedha hizi hazipelekwi tena fedha hizi ni fedha za Serikali zimepelekwa pale kwa ajili ya kufidia fedha zile ambazo zingetozwa kwenye Halmashauri zetu.

**SPIKA:** Swali fupi tu la mwisho Mheshimiwa Diana Chilolo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa zipo Halmashauri ambazo zina makusanyo madogo sana katika Halmashauri zao; na kwa kuwa ruzuku ya nyongeza inayostahili kupelekwa kwenye Halmashauri, Halmashauri nyingi hazipewi kama walivyostahili kupata na kushindwa kulipa haya madeni kwa sababu ya kuwa na ufinyu wa fedha. Je, Serikali haioni kwamba kuna kila sababu ya kupeleka kwenye Halmashauri ruzuku ya ziada kwa kiwango walichokiomba ili waweze kulipa madeni haya yanayosemwa sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya kifupi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli anachosema Mheshimiwa Diana Chilolo, Halmashauri zilizo nyingi hapa kwenye *own source* yale mapato ya ndani ni kidogo sana, nyingine asilimia moja, nyingine asilimia mbili, nyingine mpaka asilimia tano. Kwa msingi huo anachosema Mheshimiwa Diana Chilolo ni kwamba tuone uwezekano sasa wa kuwaongezea fedha hizo. Sasa suala la bajeti maana yake ni nini? *(Makofi)*

Bajeti ni utaratibu unaonyesha mapato ya matumizi ya Serikali na mapato na matumizi ya Serikali yanapitishwa na Bunge hili hapa ndani na Mheshimiwa Diana Chilolo yupo hapa atatusaidia kama tunatakiwa kupeleka nyongeza kwa ajili ya hilo eneo kwa sababu zimepungua kule basi tutafanya hivyo kama anavyosema.

Lakini hapa siwezi kutoa majibu mengine kwa sababu bajeti ilikwishapitishwa na tumefika hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kusisitiza hapa kwamba mpango tulionao ni kuhakikisha kwamba Halmashaluri zetu zinajitegemea bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini.

Kwa hiyo, kama tutafanya juu chini kuhakikisha kwamba tunakuwa na vyanzo vya mapato katika Halmashauri zetu tutakuwa tunaondokana na tatizo hili.

Lakini nasema naiona *point* ya Mheshimiwa Mbunge ikibidi kufanya hivyo itabidi kuja Bungeni hapa ili tuweze kujua sasa hiyo nyongeza itatoka wapi tuweze kuipeleka katika Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Na. 42

**Kusimamia na Kuboresha Biashara za Mipakani**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa, viwanda ni muhimu katika jamii katika kuongeza thamani ya bidhaa, pato na ajira; na kwa kuwa, biashara na nchi jirani ni muhimu katika kuinua vipato vya wananchi wa mipakani:-

(a)Je, Serikali inasaidiaje Mkoa wa Rukwa na hususan Jimbo la Kalambo kuboresha biashara za mipaka ya Kasesya, Mtula na Kasanga?
(b)Je, Serikali haioni kuwa, kwa kutoshughulikia yale yanayofanyika mipakani inasababisha biashara haramu kushamiri katika maeneo hayo?

(c)Je, Serikali ina takwimu zozote za biashara inayofanyika katika mipaka ya Zambia na Kongo kwenye vituo vya Kasesya, Kasanga, Kipili na Kirando?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali imetekeleza Programu ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo kuanzia mwaka 2003 hadi mwaka 2006.

Programu hiyo, pamoja na mambo mengine, ilihusu ujenzi wa Soko la Matai ambalo limekamilika mwaka 2006. Soko la Matai lipo karibu na mpakani. Kama likitumika vizuri litasaidia kuboresha biashara kati ya nchi yetu na nchi za Zambia na *DRC*.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza juhudi za kurasimisha biashara za mipakani, Wizara itaendelea kuimarisha ushirikiano na nchi jirani kama Zambia na *DRC* Congo kupitia Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) na uhusiano kati ya nchi na nchi.

Ushirikiano huu unalenga kuondoa vikwazo vya biashara, uendelezaji wa miundombinu ya biashara, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini na pia ujenzi wa vituo vya ukaguzi na huduma nyingine mpakani.

Mafanikio ya utekelezaji wa mkakati huu yanategemea ushirikishwaji wa sekta zote za kiuchumi hususani kilimo, usafirishaji, ufugaji na nyinginezo.

Wizara imekamilisha mkakati a kukuza mauzo nje ambao utahusisha pia uendelezaji wa miundombinu ya biashara itakayosaidia kukuza biashara mipakani.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa sasa hatuna takwimu za kuonyesha bidhaa na thamani kwa kila kituo, hata hivyo katika kipindi cha miaka mitatu ya 2005, 2006 na 2007, bidhaa zilizoingia mkoani Rukwa kutoka nchi za Zambia na *DRC* zilikuwa na jumla ya thamani ya shilingi 1,069,638,657.49/= na bidhaa kuu zilikuwa ni sukari na umeme. Bidhaa zilizouzwa Zambia na *DRC* kwa kipindi hicho ni pamoja na mahindi, maharage na samaki na zilikuwa na thamani ya 2,240,222,424/=.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kupata fulsa niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza ni kuhusu swali langu la msingi (a), nilikuwa naulizia vituo vya mpakani Kasesha na Mtula, mahali ambapo pana makubaliano kati ya Zambia na Tanzania, wilaya zetu zile wilaya ya Mbala na wilaya ya Sumbawanga ili pawe na Gulio au Soko ambalo linafanyika kila tarehe 6 na tarehe nyingine kama 22 katika vituo hivyo. Sasa pale Halmshauri imewekeza, imejenga machinjio, imejenga......

**SPIKA:** Mheshimiwa uliza swali tafadhali.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, lakini Wizara hii ya Bisahara tumeshaiomba kwa zaidi ya miaka minane ambayo mimi nimekuwa Mbunge, nimeshaomba Wizara ya Biashara itusaidie katika ujenzi wa vituo hivyo vya mpakani. Swali hili halikujibiwa; Je, Wizara itafanya kazi gani kuhakikisha katika vituo hivi tunafanya biashara nzuri?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, inaonekana hakuna takwimu ya shughuli zinazofanyika mpakani. Tunauza vitu vingi sana katika nchi ya Kongo, mafuta na bidhaa za viwandani, lakini takwimu hazionekani.

Je, hatuoni kwamba tunapoteza kufanya biashara lakini bila kuwa na takwimu?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na masoko, napenda kumjibu Mheshimiwa Mwananzilla, maswali yake mawili ya nyongeza kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, jibu tulilotoa hapa ni jibu ambalo linaelezea mkakati mzima na sio tu wa vituo alivyovitaja Mheshimiwa Mwananzilla, bali ni vituo vyote vya mpakani.

Sasa endapo Mheshimiwa anapenda tujaribu kuangalia kituo kimoja kimoja kama ambavyo amesema kwenye swali lake la nyongeza basi sisi tupo tayari kushirikiana naye na Halmashauri husika kwasababu vituo hivi vinajengwa na Halmashauri husika. Wizara yangu inatoa ushauri pale ambapo unatakiwa. Tunachopenda kumwahidi tu hapa ni kwamba Wizara itatoa ushirikiano kwa Halmashauri lakini tutaomba na yeye mwenyewe tuwasiliane kwa ajili ya kuweka mkakati utakaofanikisha hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu la takwimu ambalo ni swali lake la pili la nyongeza, suala la takwimu ni suala ambalo ni tata kwa sababu vituo vya mpakani vya nchi yetu ni vingi sana na wanaofanya biashara, mwingine anafanya usiku, mwingine anafanya mchana na sio wote wanaokuwa *recorded.*

Tuseme tu kwamba kwa mfumo ambao tumejiwekea, tuendelee kuuboresha kwa kiasi kwamba tutachukua takwimu zaidi kwa kila mtu anayefanya biashara na tukiweza kufanikisha hili ndipo hapo sasa tunaweza tukasema kwamba tunaweza tukaja na takwimu za kuonesha kwamba kwa mwezi huu, kwa mwaka huu, kila kituo cha mpakani mwa Tanzania na nchi jirani kimeweza kuwa na takwimu husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niseme tu kwamba ni hali yetu ambayo haijaweza kuboresha miundombinu ya kuweza kufahamu na kukusanya *data* zote ndio ambayo inafanya hilo ambalo Mheshimiwa Mwananzilla anasema na nia ya serikali ni kujaribu kuboresha hayo pale ambapo uwezo wa kifedha unawezekana.

**SPIKA:** waheshimiwa tunaendelea na muda umetutupa mkono. Mheshimiwa waziri wa Viwanda na Biashara, maelezo ya ziada.

**WAZIRI WA VIAWANDA NA BISAHARA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa jibu la nyongeza zaidi ya majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge, kwamba suala la takwimu kwenye mipaka yetu ni muhimu sana ili kujua biashara ambayo Tanzania inafanya na nchi jirani. *(Makofi))*

Kwa ajili hiyo Wizara yangu imetoa umuhimu uinaostahili na tunajaribu kuona kama tunaweza kuwa na mradi wa kuona kwamba takwimu zinakusanywa na kushirikiana na Wizara nyingine ambazo zinahusika na biashara ya mipakani. Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha kwamba nchi

yetu inakuwa na mfumo mzuri wa kukusanya takwimu ili tuweze kujua biashara ambayo inafanyika na ninajua kwamba kuna biashara nyingi sana ambayo inafanyika na sio tu mazao ya kilimo bali ninajua hata kuna bidhaa za viwanda ambazo zinakwenda Zambia na *DRC*.

Kwa hiyo, kwa kweli suala la takwimu ni muhimu sana na ninashukuru sana kwa kuona umuhimu huo na sisi tutashirikiana naye kwa karibu sana.

Na. 43

**Ufufuaji wa Viwanda Mbeya**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais aliahidi kufufua Sekta ya Viwanda Mbeya, kikiwemo Kiwanda cha Nyama – Mbeya:-

(a) Je, ni lini Serikali itatimiza azma yake hiyo?

(b) Je, ni hatua gani zimefikiwa hadi sasa za kimchakato?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwalugula Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifutavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, swali hili linafanana kwa kiasi kikubwa na Swali Na. 1430 linalohusu Ufufuaji wa Viwanda Mbeya, lililoulizwa na Mheshimiwa Mpesya na kujibiwa hapa Bungeni tarehe 21 Aprili, 2008 Na. 127 kwenye orodha ya shughuli za Bunge za siku hiyo. *(Makofi)*

Kama nilivyojibu siku hiyo, Serikali itaendelea na juhudi za kuvutia wawekezaji waendelee kuwekeza katika Jiji la Mbeya na Tanzania nzima kwa ujumla kwa kuendelea kuboresha zaidi mazingira ya uwekezaji na kubainisha fursa zilizoko katika sekta ya viwanda katika Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali itaendelea kutatua matatizo yanayokwamisha uzalishaji hususan matatizo ya umeme, maji na miundombinu ili kuimarisha ufanisi, viwanda vya Jiji la Mbeya na mkoani mbeya kwa ujumla.

(b) Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha *Tanganyika Packers Limited Mbeya*, bado hakijapata mwekezaji. Kiwanda hiki kimetangazwa mara mbili katika juhudi za kupata mwekezaji bila mafanikio. Juhudi za kutafuta mwekezaji zinaendelea. Aidha kiwanda cha nyama cha Mbalizi ambacho ujenzi wake ulianza mwaka 1975 na kusimama mwaka 1985 kabla ya kukamilika kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za ukosefu wa fedha

bado hakijapata mwekezaji. Juhudi za kuendelea kutangaza viwanda hivi kwa wawekezaji mbalimbali wakiwemo wa-Iran, Korea, Italia, na kadhalika zinaendelea chini ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mpesya kwa jinsi anavyohimiza maendeleo ya viwanda katika Jiji la Mbeya na Tanzania kwa ujumla.

**SPIKA:** Hatahivyo anauliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Mpesya.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri yenye kutia matumaini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kurudia rudia huku kwa swali kunalenga katika kutimiza ahadi ya Rais aliyoitoa ya kufufua viwanda katika Jiji la Mbeya, ningependa kujua; Ni lini kiwanda cha *ZZK* kitaanza kufanya kazi?

Ni lini kiwanda cha *Mbeya Industries* kitaanza kufanya kazi na ni lini kiwanda cha nguzo cha Mbeya kitaanza kufanya kazi? Ili kiweze kuwapatia vijana ajira?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, hivi karibuni Jiji la Mbeya lilitoa eneo kubwa sana kwa ajili ya ujenzi wa viwanda kwa mfumo wa *EPZ*, na katika taratibu za Wizara za Serikali, ilikuwa ifikapo mwaka 2008 *EPZ* iwe imeshakamilishwa Mbeya. Sasa nataka kujua ni lini na kwa muda suala hili litazingatiwa na kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kumjibu Mheshimiwa Mpesya maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kukubaliana naye kwamba Mheshimiwa Rais, alitoa ahadi ya kuhakikisha kwamba Jiji la Mbeya na miji mingine yote ile ambayo kuna uwezekano wa kujenga viwanda basi viwanda vinajengwa. Na anapouliza kuhusu viwanda hivi vitatu ni lini vitafanya kazi; napenda tu kumjibu kwamba nia ya Serikali ni kwamba viwanda hivi vingeweza kufanya kazi hata leo. Tatizo linalokuja ni kwamba ukishakuwa na kiwanda ni lazima umtafute muwekezaji, sasa inapokuwa muwekezaji anasuasua au anakuja munaanza kuingia mazungumzo na baadaye anajiondoa Serikali inapata tatizo katika kujibu kwamba ni lini. Ingekuwa Serikali ndio inajenga hicho kiwanda na kuanza kukiendesha yenyewe basi ingekuwa na majibu ya kusema kwamba ni lini tunaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kumhakikishia kwamba Serikali itaendelea kuongeza jitihada katika kuwatafuta wawekezaji wengi zaidi ili watakapokuja pale basi waweze waweze kuanza hivi viwanda na vijana pamoja na watu wengine wa mkoa wa Mbeya waweze kupata hizo ajira. Namwomba tu Mheshimiwa Mpesya na wananchi wetu wa Mbeya wavute subira wakati Serikali inahangaika kuwatafuta hawa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hili la pili la *EPZ,* ni kweli kwamba ilikuwa ni nia ya Serikali kwamba tuwe tumejenga maeneo haya maalum kwa ajili ya viwanda na shughuli nyingine za kiuchumi haraka kwa kadri iwezekanavyo. Jambo ambalo limefanya mradi huo ukaacha kukamilika kama ambavyo tulikuwa tumepanga ni uwezo wa kifedha na Bunge lako litakumbuka kwamba sio fedha zote ambazo tunaomba tunazipata. Kwa hiyo, pale ambapo tutakuwa na uwezo wa kifedha wa kutosha namhakikishia Mheshimiwa Mpesya kwamba maeneo hayo nayo yatajengwa haraka iwezekanavyo.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona, nina swali dogo tu la kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa, swali la msingi la kufufua kiwanda cha nyama Mbeya, linafanana kabisa na ufufuaji wa viwanda vile vya magunia na kile kiwanda mama cha *Machine Tools Moshi.* Ningependa kujua je, Serikali imefikia hatua gani kuhakikisha kwamba kile kiwanda mama cha *Machine Tools* kimefufuliwa ili kiweze kuwa ukombozi katika kuendeleza viwanda vidogovidogo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kumjibu Mheshimiwa Lucy Owenya swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Owenya, kwamba vipo viwanda mbalimbali ambavyo havijafufuliwa; magunia ni kimojawapo, *Machine Tools* na vinginevyo. Napenda kurudia kwamba nia ya Serikali ni kwamba viwanda hivi viwe vimefufuliwa hata jana, yaani sio leo wala sio kesho, viwe vimeshafufuliwa. Kitu ambacho kinakuwa na matatizo hapa ni kuweza kuwapata wawekezaji ambao wanaweza wakawekeza pale katika vile viwanda wakatoa ajira na vilevile wao wenyewe wakapata faida. Napenda kukariri ahadi tunayoitoa hapa kwamba Wizara na serikali kwa ujumla tutaendelea na jitihada za kuwatafuta wawekezaji katika viwanda hivyo na mara watakapopatikana hatutasita kuwakabidhi viwanda hivyo ili waviendeleze. Sasa hivi anapouliza kwamba mchakato umefika wapi, kwa kweli sina jibu la kumpa lakini jitihada za kuwatafuta hao zinaendelea na tutakapofika mahali pazuri basi Mheshimiwa Owenya utaona wawekezaji wanaanza kufanya kazi katika viwanda hivyo.

Na. 44

**OSHA Kuwafikia Wafanyakazi wa Viwanda na Makampuni**

**MHE. MGENI J. KADIKA** aliuliza:-

Kwa Kuwa, OSHA ni chombo muhimu kwa kushughulikia Afya na Usalama wa Wafanyakazi wakiwa kazini:-

Je, ni lini Serikali itahakikisha kuwa, chombo hicho kinawafikia wafanyakazi walioko viwandani na makampuni mbalimbali nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum , kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa wakala wa usalama na Afya mahali pa kazi yaani *OSHA* haijawa na uwezo mkubwa wa kuwafikia wafanyakazi wote sehemu mbalimbali za kazi. Hii ni kutokana na upungufu wa wakaguzi, fedha pamoja na vifaa vya kutendea kazi kama vile magari na vifaa vya kitaalamu vya ukaguzi. Kwasasahivi *OSHA* ina jumla ya watumishi 57 na kati yao ni wakaguzi 33 tu waliopo ingawaje mahitaji halisi ni wakaguzi 100, mahitaji ya watumishi wote katika wakala ni watumishi 170.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeanza kujipanga ili kuiwezesha *OSHA* kwa madhumuni ya kuwafikia wafanyakazi sehemu mbalimbali za kazi kama ifuatavyo:-

(i)Katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Wizara yangu imeomba kibali cha nafasi mpya 14 za wakaguzi ili kuweza kupunguza tatizo la uhaba wa wakaguzi hao.

(ii)Kununua vifaa vya kutendea kazi kamavile vifaa vya kitaalamu vitavyonunuliwa kupitia mradi wa *MKUMBITA*, yaani *Best Programme.*

(iii) Kununua magari manne ili kurahisisha usafiri wa kuwafikia wafanyakazi katika sehemu mbalimbali za kazi.

(iv) Kuanzisha Ofisi nyingine tatu za Kanda ambazo zitakuwa ni Kanda ya Kusini kule Mtwara, Kanda ya Kati Dodoma na Kanda ya Pwani, Dar-es-Salaam. Kwa hivi sasa kuna Ofisi tatu za Kanda yaani ya Kaskazini – Arusha, Kanda ya Ziwa – Mwanza na Kanda ya Juu Kusini – Mbeya, ambazo zinafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, jitihada zote hizi ni kwa madhumuni ya kusogeza karibu huduma za chombo hiki, *OSHA*, katika sehemu mbalimbali za kazi. Hata hivyo pamoja na uchache wa wakaguzi, fedha na vifaa vya kutendea kazi, jumla ya sehemu za kazi 3800 zilizosajiwa zilikaguliwa katika kipindi cha mwaka uliopita.

**MHE. MGENI J. KADIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu waziri, nina maswali ya nyongeza. Kwa kuwa, kwenye makampuni ya migodi hutokea maafa makubwa mara kwa mara na watu wengi hupoteza maisha yao. Pamoja na uhaba wa fedha na wafanyakazi; Je, *OSHA* inawasaidiaje wafanyakazi hao ili kunusuru maisha na usalama kwenye kazi hiyo. *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, vilevile *OSHA* inawasimamia vipi waajiriwa kuhakikisha wanapopata ajali wakiwa kazini wanapata haki zao? *(Makofi).*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika,  kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajali kama ambazo zinatokea migodini. Ni kweli kwamba kwa siku za hivi karibuni ajali nyingi zimetokea kwenye maeneo ya migodi lakini pamoja na ajali hizo bado ni kweli kwamba sisi kama Wizara na *OSHA* kwa kutumia Sheria Na. 5 ya mwaka 2003, imekuwa ikisisitiza kwamba tuangalie usalama wa wafanyakazi maeneo ya kazi. Na hata watu wa migodi wanazo taratibu hizi na sheria hii na wanatakiwa waweke taratibu ambazo zitazuia ajali ambazo zinatokea.

Ni kweli kwamba ajali nyingine zinatokea kutokana hasa na wakati wa mvua ambapo kutokana na kutozingatia sana hali yenyewe ya wakati wa masika, yale mashimo huporomoka na wakati mwingine ni nje ya uwezo wa hata yale makampuni; isipokuwa tahadhari zinatakiwa na vilevile kujua vipindi ambavyo sio vyema mashimo yale watu wakaingia kulingana na hali halisi ya maeneo yale kwa maana ya udongo. Lakini kama *OSHA* kwa kuzingatia sheria hii itaendelea kusisitiza afya na usalama wa wafanyakazi katika maeneo haya ya kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la waajiriwa wanaoumia wakiwa kazini, *OSHA* inafanyaje? Kama tunavyojua kipindi kilichopita tulipitisha sheria ya fidia kwa watu wanaoumia kazini. Kwa hiyo kwa kutumia sheria ile na kwa kutumia utaratibu tofauti watu hawa wanafidiwa kwa mpango na kwa sheria ambayo tumeipitisha. Kazi ya *OSHA* ni kuangalia kwamba vifaa vipo na wafanyakazi wapo katika hali ya usalama. Lakini ni sheria tofauti inayohusika sasa na suala la fidia kama tulivyopitisha hapa Bungeni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi, naomba kuongezea kidogo tu kwenye jibu zuri alilolitoa Mheshimiwa Naibu Waziri pale.

Mheshimiwa Spika, ni vema tukafafanua vizuri zaidi kwamba; swali linasema kwenye makampuni ya migodi ajali zinatokea mara kwa mara. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, si kweli; ajali zinazotokea kwenye migodi ni migodi ya watu binafsi wachimbaji wadogo wadogo. Kama kuna makampuni ambayo yanajitahidi kulinda taratibu za usalama, makampuni ya migodi yanajitahidi sana, wana kawaida kwa wafanya kazi wao kusoma zile taratibu na kufanya mazoezi kabla hawajaenda katika migodi ile kufanya kazi.

Kwa hiyo, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba ajali zinazotokea ni katika wale wachimbaji wadogo wadogo. Sisemi kwamba *OSHA* haihusiki hata kuwasaidia wale wachimbaji wadogo wadogo ila si sahihi kuzungmza kwamba ni makampuni yale makubwa, si kweli.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *OSHA* ni wakala wa kusimamia usalama na afya za wafanmyakazi. Na kwa kuwa, makampuni mengi ya wazoaji taka wa jiji la Dar-es-Salam hawajali afya za wafanyakazi wao na wala

hawawapi vitendea kazi wafanyakazi wao. Je, hili nalo *OSHA* hawalioni? Au wanasubiri Wizara ipate pesa ndio iwasaidie?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mkiwa, kama lifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, wanaozoa taka katika Jiji la Dar-es-Salaam, wanatakiwa kwa sheria hii kuhakikisha kwamba wanavyo vifaa ambavyo vitawalinda wale wafanyakazi wanaofanya kazi hii. Kama hili halifanyiki nitumie nafasi hii kuagiza *OSHA* waliangalie hili na wachukuliwe hatua kama hawatakuwa wanatimiza matakwa ya sheria. *(Makofi)*

Na. 45

**Mfuko wa Wajasiriamali**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilipojibu swali Na. 158 katika Mkutano wa Kumi na Nne kuhusu ahadi ya mwaka 2007 ya kutoa mikopo toka mfuko wa wajasiria mali kwa *SACCOS*, vikundi na watu binafsi kwenye Jimbo la Nyan'hwale ilitamka kuwa, Benki Kuu ilikuwa ikikamilisha taratibu muhimu za kupata Benki?

Asasi za fedha za kugawa mikopo hiyo kwenye maeneo yote yaliyoainishwa na kwamba zipo Shs. Milioni 100 zilizotengwa kwa ajili ya Jimbo la Nyang'hwale; na kuwa wananchi, vikundi na *SACCOS* nyingi za Jimbo hilo tayari zina michanganuo ya miradi itakayogharimiwa na mikopohiyo:-

Je, hadi tarehe linapojibiwa swali hili kwa mara ya tano, mchakato wa kupeleka fedha hizo Nyang'hwale umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa James Philip Musalika amekuwa akiuliza swali kuhusu ahadi ya Serikali kupeleka fedha za mikopo ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kwa wajasiriamali jimboni kwake ambao walikosa mikopo katika awamu ya kwanza. Kama nilivyoeleza katika Mkutano wa 14 kuhusu

utekelezaji wa ahadi hiyo, Benki Kuu walikamilisha mchakato wa kupata Benki na Asasi za kutoa fedha katika maeneo waliyokosa mikopo katika maeneo ya wilaya mbalimbali. Vigezo vilivyotumika ni kwa zile wilaya zilizokosa kabisa na zile ambazo zilipata chini ya kiwango; huu ndio utaratibu uliopo lakini tunategemea kwamba kwa vile mpango huu ni endelevu fedha zitakapokuwa zinarejeshwa asasi za fedha kwa maelekezo yetu zikishirikiana na serikali za Wilaya husika watapendekeza ni wapi pa kupeleka fedha zitakazokuwa zinarudishwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hilo Benki Kuu tayari imewasiliana na Benki ya *CRDB* ambayo imeonyesha nia ya kutoa huduma za mikopo wilayani Geita. Ni matumaini yangu kwamba kwa kutekeleza nia hiyo wananchi waliojiunga na *SACCOS* zilizo hai watafikiwa. Ni kweli kwamba baada ya malalamiko ya Mheshimiwa Musalika, katika ngazi ya Wizara ilipendekezwa zitengwe shilingi milioni 100 kwa ajili ya Jimbo la Nyang'hwale, lakini baada ya kushauriana na wataalamu wa pande zote kwa maana ya Benki Kuu na Hazina kuhusu utaratibu wa kugawa fedha za mpango huu Serikali imeamua kuwa fedha zitapelekwa katika maeneo yaliyokosa katika wilaya badala ya Majimbo ili kuepusha malalmiko kwa Waheshimiwa Wabunge ambao pia maeneo yao yameathirika kwa kukosa fedha hizo.

Kwa hiyo, ni muhimu tukatumia vikao vya Halmashauri kuhakikisha kuwa Majimbo yote ya uchaguzi ndani ya wilaya yanafaidika na mgawo wa fedha hizi. Ni vigumu sisi kama Wizara kusimamia migawo ndani ya wilaya moja moja. Aidha napenda kumsihi Mheshimiwa Musalika na wananchi wa Nyang'hwale wawe na subira wakati utaratibu nilioueleza hapo juu ukiandaliwa na kutekelezwa.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, leo ni mara ya sita ninasimama kwenye Bunge lako Tukufu kuulizia ahadi ya Serikali ya kutekeleza kupeleka pesa za ujasiriamali katika Jimbo langu. Na pia leo ni mara ya sita Serikali inasimama kuelezea ahadi yake hiyo ambayo haitekelezeki, haijatekelezwa. Kwa kuwa sasa mimi naonekana muongo mbele ya wapiga kura wangu tangu mwaka 2007. Na kwa kuwa dawa ya muongo wapiga kura wanayo. Je, Serikali sasa Waziri atatamka hapa tena kwa mara nyingine kwamba aje yeye mwenyewe sasa Jimboni kule aeleze huo ukweli wake au uongo wake kwa wapiga kura yeye mwenyewe ili mimi aninusuru na hasira za wapiga kura wangu? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Sio tu hasira za wapiga kura, kuna gazeti moja jana linasema mishahara ijayo ya Bunge ni 12,000,000/= kwa mwezi. Kwa hiyo pia , utaandamwa na watu ambao wanazitafuta 12,000,000/=. Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimeeleza hapa kwa kweli kwamba mpango huu umeainishwa kiwilaya na wala si Majimbo. Na inavyoonekana baada ya Wilaya ya Geita

kupata mgawo wa kwanza wa milioni 700 ikiwa ni kati ya wilaya ambazo zilipata hela nyingi kuliko wilaya nyingine zozote nchini bahati mbaya kwa wakati ule inaonekana Jimbo la Nyang'hwale wale wajasiriamali na *SACCOS* hazikuchamkia haraka. Na kwasababu zilikuwa kiwilaya basi majimbo yale mengine mawili inaonekana yakafaidi karibu fedha zote zile. Kwa hiyo, sisi tunachosema sisi tuliliona hili kama Wizara tukaona kwa kweli ni tatizo kwa Mbunge. Lakini kwa utaratibu tulioshauriwa na wataalamu kwamba tukianza kwenda kwenye Majimbo, kwa mpango huu sisi kama serikali tutachanganyikiwa, kwahiyo tuendelee kupeleka kiwilaya. Lakini sasa wabunge kwasababu wote wanakaa kwenye Halmashauri, waone ni namna gani awamu zinazofuata na zile fedha zinazorudi zinapokuwa zimekopeshwa ziweze kwenda kwa wajasiriamali na *SACCOS* za Jimbo la Nyang'hwale ambalo vile vile ni Jimbo ndani ya wilaya ile. Kwahiyo mimi ningemshauri Mheshimiwa Mbunge, palepale kwenye Halmashauri aaangalie baada ya *CRDB* kuja kuingia na kwa kushirikiana na Halmashauri yake basin a *SACCOS* za Nyang'hwale ambazo zimeshajiandaa kama alivyosema zipate katika awamu hii inayofuata na katika fedha zinazorudi.

Mheshimiwa Spika, hili la Mheshimiwa Waziri, kwenda Nyang'hwale ni jambo la kawaida kwasababu Mawaziri tunatakiwa tupite na tuhamasishe watu wajiunge na *SACCOS.* Kwahiyo utaratibu wa Waziri ukiweza kufanikiwa kwa maana ya kupanga kuja Geita, atafika na ataelezea kwa maana ya kuhamasisha *SACCOS* na kuwahamasisha vijana waweze kupata ajira na watu wapate mikopo waweze kuondokana na umasikini.

**SPIKA:** Tuhamie kwenye Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Sina hakika kama Mheshimiwa Zambi, atapenda kuuliza swali hili ambalo jana limejibiwa kikamilifu kabisa na Wizara. Mheshimiwa Zambi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwasababu linaunyeti wake kwa wananchi wa wilaya ya Mbozi, ninaomba Mheshimiwa Waziri aendelee kulijibu.

Na. 46

**Mbolea ya Minjingu Rock Phosphate**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa mbolea ya *Minjingu Rock Phosphate (MRP)* ambyo ni yakupandia imeonyesha matokeo mabaya sana kwa asilimia 99 ya wakulima waliotumia na kwa kuwa Serikali ilisema katika Bunge la Mwaka 2008/2009 kwamba mbolea hiyo imekosa baadhi ya virutubisho:-

Je, Serikali imechukua hatua gani katika kurekebisha hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na wilaya zote zinazonufaika na utaratibu wa ruzuku imekuwa ikifuatilia kwa karibu ufanisi wa mbolea ya minjingu. Ufatiliaji huo kwa wilaya ya Mbozi umeonyesha kwamba kiwango cha ufanisi cha mbolea ya Minjingu. Ufuatiliaji huo kwa wilaya ya Mbozi umeonyesha kwamba kiwango cha ufanisi cha mbolea Minjingu ni kama ifuatavyo:-

Kata ya Ihanda (asilimia 68), Myovizi (asilimia 63), Msia (asimilia 63), Nyimbili (asilimia 68), Chiwezi (asilimia 70), Igamba (asilimia 60), Mlowo (asilimia 70), Iyula (asilimia 65), Ruanda (asilimia 78), Isansa (asilimia 70) Tunduma (asilimia 60), Isandula (asilimia 65) na Nambizo (asilimia 32).

Mheshimiwa Spika, matokeo hayo yamesababishwa na mambo yafuatayo:-

(i) Uchanganyaji wa mbolea ya minjingu ya UREA haukufanywa vizuri kama ilivyokuwa imeelekezwa na wataalamu (kilo 100 za minjingu na kilo 25 za UREA) wakati wa kupanda) hivyo ukuaji wa mwanzo wa mahindi kutokuwa mzuri.

(ii) Mahindi yaliyopandwa kwa kutumia mbolea ya minjingu katika hatua za awali (kwa wale ambao hawakuchanganya na kilo 25 za UREA wakati wa kupanda), mahindi yalichelewa kukua ikilinganishwa nay ale yaliyopandwa kwa kutumia *DAP*. Hata hivyo, baada ya kukuziwa na mbolea ya *UREA*, mahindi yale yalianza kubadilika na yanaendelea vizuri.

(iii) Maeneo ambayo wakulima walichelewa kupanda na hivyo udongo kutokuwa na unyevu wa kutosha, zao la mahindi liliathirika. Hata hivyo, baada ya mvua kuendelea kunyesha mahindi yanaendelea vizuri.

(iv) Baadhi ya wakulima hawakufuata maelekezo ya kitaalam ya kiasi cha mbolea kinachostahili kuwekwa kwenye ekari moja badala yake waliweka eneo la zaidi ya ekari moja.

(v) Aina ya udongo usiofaa kwa matumizi ya minjingu (udongo ambao siyo *acidic*).

Mheshimiwa Spika, kutoka na matokeo hayo, hatua zifuatazo zinachukuliwa:-

(i) Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri zote itayatambua maeneo ambayo mbolea ya minjingu haitafaa kutumika kama mbolea ya kupandia.

(ii) Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri kuendelea kutoa elimu kwa watumishi ugani na wakulima juu ya matumizi sahihi ya mbolea ya minjingu.

(iii)Aidha, kiwanda cha minjingu kimeanza kuboresha mbolea ya minjingu ili kuwa na ufanisi kwa kuongeza virutubisho kama naitrojeni, salfa, zink, shaba na boron.

Mbolea hiyo itakayoboresha itaitwa minjingu mazao. Uzalishaji wa mbolea hiyo utaanza mwaka 2010/2011.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, utakubaliana na mimi kwamba kulikuwa na umuhimu wa kuuliza swali hili kwa sababu hata Waziri hajui kwamba mimi ni Mbunge Mashariki. Kwa hiyo naomba Hansard isome sawa sawa kwamba mimi ni Mbunge wa Mbozi Mashariki sio Magharibi. Lakini pia naomba niweke kumbukumbu sahihi kwamba kijiji alichokisoma Mlowa, kinaitwa Mlowo, kata iliyosomwa Nambizo, inaitwa Nambinzo, baada ya masahihi hayo ninaomba niulize maswali madogo tu nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni sababu ambazo zilifanya Serikali ipeleke mbolea minjingu kwa wananchi katika maeneo hakukufanywa utafiti mzuri kuhusu ardhi yake na kwa maana hiyo kuwasababishia wananchi hasara kubwa ya mazao na hususan kata ya Nambinzo ambayo mafanikio ya mbolea hiyo ni asilimia 32 tu, Serikali inawaambia nini wananchi wa kata hiyo?

Je, Serikali sasa itakubali ombi la wananchi wa Mbozi kwamba matumizi ya mbolea ya Minjingu yasitishwe na badala yake Serikali iendelee kuwapa mbolea ya DAP ili waweze kuzalisha kwa ufanisi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwamba kwanza kuomba radhi kukosea jimbo lake kwamba ni Mashariki na sio mbozi Magharibi. Lakini kwa kuwa kata zilizotajwa ni mbozi Mashariki basi inamaa utafiti huo umefanywa kwenye jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, nipende sasa kujibu maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

Niseme kwamba mbolea hii kabla haijapeleka Serikali iliandika barua kupia kwa wakuu wa mikoa kwamba Halmashauri zote ziweze kufanya utafiti na kujua udongo wao una sifa PH 5.5 kurudi chini. Kwa sababu mbolea hii ya minjingu inakubali kwenye PH ya chini kwa hiyo wilaya zile ambazo zilifuata ushauri huu walifuata taratibu hizo na walifanya uchunguzi wakagundua kwamba mbolea ya minjingu inaweza kwenda kule ama haitaweza kwenda. Kwa mfano kuna wilaya zingine ambazo zilipelekewa DAP kwa sababu ilionekana kabisa kwamba mbolea ya minjingu haiwezi ikafanya kazi pale. Kwa hiyo taarifa ilitolewa tangu mwezi wa pili tarehe 28 kwa barua zilizoandikwa mikoni.

Pili, kwa sasa hivi tumeshaagiza chuo chetu cha kilimo na utafiti cha Uyole kiweze kwenda Mbozi nakufanya utafiti kwenye Kata zote kwa mara ya pili kiweze kugundua kwamba ni maeneo gani ambayo mbolea hii ya Minjingu inaweza ikafaa na ni maeneo gani ambayo haitafaa. Kwa sababu hivi ninavyozungumza, Mheshimiwa Mpesya na linafanya vizuri shamba lake la kahawa na kwa hiyo ni kwamba mbolea hii inafaa kwa baadhi ya maeneo sasa ndiyo tunataka tuainishe ni maeneo gani. Kwa hiyo cha muhimu zaidi ni kufanya utafiti wa udogo kujua kwamba mbolea hii ya minjingu inaweza kufaa sehemu gani?

Lakini pia kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kujua na ni kiasi gani cha mbolea kinaweza kikatumika, lakini kuna uhumu pia wa kuhamisha viwanda vyetu hapa nchini ili tuweze kuzalisha mbolea yetu ya uhakika hapa hapa nchini.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kufanya sahihi kidogo katika ibara ya kwanza ya swali langu, neno *earth,* wameweka a, *ERTH* haina a, na kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge ni kirefu cha neno *Environmental.*

**SPIKA:** Ni kifupi, sio kirefu.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Kifupi *Environmental Resources* pamoja na Technology for Humanity, baada ya hayo naomba sasa swali langu namba 47 lipate majibu.

Na. 47

**Matumizi ya Mbolea ya ERTH FOOD**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa, miaka ya hivi karibuni kumekuwa na uingizaji wa mbolea itumikayo na mazao mashambani iitwayo *ERTH FOOD.*

Je, Serikali inaifahamu mbolea hiyo na inafanya utafiti upi ili iweze kutumika sehemu nyingi hapa nchini hasa mkoani Rukwa ambako mbolea hiyo ingeweza kusaidia kuongeza rutuba ya udongo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini naomba kutoa maelezo yafuatyo kuhusiana na mbolea za organic zikiwemo hiyo ya *ERTH FOOD.*

Serikali inatambua umuhimu wa matumizi ya mbolea za aina hizo kama ambavyo nilishawahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu manufaa ya mbolea za namna hiyo kama yafuatayo:-

Huongeza virutubisho mbalimbali, Kutunza unyevu unyevu kwenye udogo na kuweka mazingira ya asili kwenye udogo hivyo kufanya hivyo uwe na uhai.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwepo kwa mbolea *ERTH FOOD* Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ilitoa kibali cha kuuza mbolea ya *ERTH FOOD* kwa kampuni ya Tanzania *Investment Group* (*TIG)* mwaka 2005. Mbolea ya *ERTH*

*FOOD* ilifanyiwa utafiti katika vituo vya utafiti vya *SUA*, Uyole, Kibaha, taasisi ya mionzi na kwa Mkemia Mkuu.

Tafiti katika vituo hivyo zilionyesha kwamba mapungufu yaliyopo katika mbolea hiyo ni kuwepo kwa kiwango cha chini cha viini lishe ikilinganishwa na viini lishe vinavyopatikana katika mbolea za kemikali yaani mbolea za viwanda. Aidha ubora zaidi wa *earth food* ni ule uwezo wake wa kuweza kuwezesha udongo kuhifadhi unyevu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishasema, Wizara yangu ilitoa kibali cha kuuza mbolea ya *ERTH FOOD* kwa kampuni *TIG* tangu tarehe 28 Oktoba, 2005 kwa masharti yafuatayo.

(i) Kutangaza kwa umma kuwepo kwa mbolea ya aina hiyo ikiwa ni pamoja na kuelezea virutubisho vinavyopatikana kutokana na kutumia mbolea hiyo.

(ii)Kabla ya kuuza mbolea ya *ERTH FOOD* kila mfuko wa mbolea uwekwe alama isiyofutika inayoonyesha vizuri kiasi cha virutubisho.

(iii) Endapo mbolea hiyo itauzwa bila kuweka alama ya kuonyesha kiasi cha virutubisho katika kila mfuko kibali kitafutwa na hivyo kusimamisha mauzo.

Mheshimiwa Spika, endapo mkoa wa Rukwa watahitaji kutumia mbolea ya *ERTH FOOD* wawasiliane na kampuni inayohusika na mkoa uhakikishe kwamba masharti hayo ya Serikali yanazingatiwa.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri nakuhakikishia ya kwamba alama aliyokuwa anaizungumzia imewekwa kwenye mifuko hiyo. Maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali sasa imetambua ya kwamba mbolea hiyo ni muhimu na kwa sababu mimi mwenyewe nimepata nafasi ya kununua mifuko ambayo imetoa mazao mazuri sana kwenye zao la mahindi na mazao mengine ya shambani.

Je, Waziri atakubaliana nami ya kwamba ni vizuri sasa vyuo vyetu vya kilimo na vyuo vya kufundishia wakulima vikapata nafasi ya kupata baadhi ya mbolea hii ili waanze kuitumia ambayo itakuwa ni chanzo cha kurutubisha ardhi yetu?

La pili kwa kuwa zao la Karanga, ndiyo zao kuu wanalolitumia katika kuleta mbolea hii je, Waziri haioni ya kwamba kuna umuhimu kuleta viwanda hivyo ili viwe katika maeneo yanayozalisha zao la karanga kama kule Mpanda, Urambo, Nachingwea, Kongwa, sehemu hizo zingepata viwanda tungekuwa na mbolea ya kutosha na kueneza nchi hii, Waziri anasemaje kuomba angalau shirika hili likaleta viwanda katika nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba vyuo vya kilimo viweze kutumia mbolea hii nadhani ni wazo nzuri ambalo wakitumia pia ni njia mojawapo ya kufanya research zaidi kuhusiana

na mbolea hii. Kwa hiyo ni wazo nzuri wanaweza wakaitumia. Lakini suala la pili la kuleta viwanda linafanana kabisa na lile ambalo Wizara ya Viwanda imejibu kwamba majukumu ya Serikali ni kuandaa mazingira kwa mwekezaji yoyote ambaye anataka kuanzisha kiwanda na hivyo namuahidi kwamba Wizara yangu kwa kushirikiana na mwekezaji yoyote ambaye anataka kuweka kiwanda kwa ajili ya kuzalisha mbolea hii tuko tayari kushirikiana naye kwa mahitaji ambayo atahitaji tutamsaidia ili aweze kuanzisha kiwanda hiki. Viwanda vinaanzishwa na *private sector* ya Serikali ni kuratibu kuweka mazingira mazuri.

Na. 48

**Uwekezaji wa Minara ya Simu za Mikononi Jimboni Magu**

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

Kwa kuwa, kampuni ya Simu za Mkononi ya *ZAIN* (zamani *CELTEL*) ilikuja jimboni Magu kuangalia mahali utakapowekwa mnara wa mawasiliano ya simu:-

(a) Je, Mbona hawajarudi tena na sasa ni zaidi ya mwaka toka waje?

(b)Je, ikiwa kampuni ya ZAIN imeshindwa, kwa nini Serikali isihamasishe kampuni ya *VODACOM* waweke mnara wao Shishani au Kabila ili wananchi wafaidike na teknolojia hii ya kisasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimwa Dr. Festus B. Limbu, Mbunge wa Magu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Kampuni ya simu ya *ZAIN* ilikwenda katika Kata ya Shishani katika Jimbo la Magu. Lengo la Kampuni hiyo kufika kwenye kata hiyo, lilikuwa ni kufanya utafiti wa masoko ilikuangalia uwezekano wa kuweka mnara wa mawasiliano. Baada ya utafiti huo ilibainika kuwa eneo hilo linakidhi mahitaji ya kimasoko na linafaa kujengwa mnara wa mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *ZAIN* haijashindwa kujenga mnara katika jimbo la Magu, bali kutokana na mtikisiko wa kiuchumi unaoikabili dunia hivi saa, kampuni hiyo ilikuwa inaangalia upya mkakati wake wa uwekezaji (*Investment Stategy*).

Hata hivyo, kampuni hii ya *ZAIN* inatarajia kukamilisha ujenzi wa mnara wa mawasiliano kwenye eneo la Kabila ifikapo Juni, 2010.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wake, kampuni ya simu ya *VODACOM*, imeyabaini maeneo ya Kata ya Shishani yaliyopo katika Jimbo la Magu tayari kwa kuyafanyia utafiti wa kimasoko na kiufundi ili kuangalia uwezekano wa kufikisha huduma ya mawasiliano kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *TIGO* tayari imeweka mawasilianokatika maeneo mbalimbali ya Jimbo la Magu yakiwemo Nyanguge, Nasa na Kisesa.

Aidha, kampuni hiyo ina mpango wa kuongeza huduma ya mawasiliano hususani kwenye maeneo ya vijijini ikiwa ni pamoja na maeneo ya Shishani na Kabila baada ya kuyafanyia uchunguzi wa awali.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na juhudi zake za kuhamasisha Makampuni ya Simu yaliyopo nchini kupeleka na kusambaza huduma za mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini ili kuharakisha maendeleo ya wananchi.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na majibu mazuri naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo, kwanza napenda nishukuru sana kwa kampuni ya *ZAIN* kwa mipango yake ya ujenzi wa mnara wa *ZAIN* pale Kabila na kwamba ifikapo Juni, 2010 utakuwa umekamilika.

Mheshimiwa Spika, pia nipongeze sana *VODACOM* kwa kuweka mnara katika kijiji cha Salama ambacho kwa hivi sasa kimesaidia sana katika kuwasaidia kimawasiliano wananchi wa Tarafa ya Ndagalu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tarafa ya Ndagalu yenye Kata tatu za Ngahaya, Kunguru na Shishani ndiyo Tarafa peke katika jimbo la Mangu lenye tarafa nne ambalo lilikuwa bado halijanufaika sana na uwepo wa mitandao hii. Na kwa kuwa tarafa hii inazalisha kwa wingi sana mazao ya kilimo na mazao ya mifugo na kwa kuwa *ZAIN* wameshafanya tathmini na kuona kwamba eneo hilo linakidhi mahitaji ya kimasoko kwanini Serikali isiishauri *VODACOM* isiendelee kufanya utafiti wa kimasoko, badala yake waende moja kwa moja wakawekeze pale Shishani?

Ili mnara ya Shishani usaidiane na Wazazui pamoja na wa Salama pamoja na Magu uboresha mawasiliano katika tarafa ya Ndagalu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza nizipokee shukrani hizo alizozitoa na nitazifikisha kwa makampuni husika na kuwaomba waendelee kutusaidia kufikisha huduma za mawasiliano katika tafara ya Dagalu ambako kuna vijiji ambavyo vinahitaji mawasiliano na soko linakubali kwamba mawasiliano yakifikishwa huduma hizi zitasaidia sana wananchi vijijini.

Lakini napenda nimuambie Mheshimiwa Mbunge kwamba si rahisi kuomba *VODACOM* waache mipango yao ambayo wameipanga na wachukue mipango ya kampuni nyingine tunajua kila business ina business plan yake na ina rule out plan yake lakini tutakachokifanya sisi ni kuhamasisha kwamba utafiti kule umefanywa so uko deeple na uhakika ku-invest katika kata au tarafa Ndagalu hut-*regreat.* Hicho ndicho kitu

Serikali inaweza kufanya ili huduma hizi za mawasiliano *VODACOM* waweze kuwahi mwanzo kabla ya hao ambao wamefika.

Na. 49

**Kampuni ya Simu ya Zain Kuongeza Minara**

**MHE. PROF. IDRIS MTULIA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kampuni za simu za *ZAIN*, *TIGO*, na *VODACOM* zinapongezwa sana na wananchi wa Rufiji kwa kuleta Mawasiliano: na kwa kuwa kampuni ya *ZAIN* imeweka minara vijiji vya Mloka na Kilimani na kuviruka Vijiji vya Mtanza, Nyaminywili na Kipugira.

Je, Serikali haioni haja ya kuishawishi Kampuni ya *ZAIN* ili kuongeza minara katika vijiji vilivyoorodheshwa hapo juu ili wananchi wafaidike na mawasiliano ya simu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo.

Kampuni ya simu ya *ZAIN* inaendelea na mchakato wa kubaini maeneo mbalimbali ambayo hayana mawasiliano nchini. Aidha, kampuni hii tayari imebaini maeneo ya vijiji vya Mtanza, Nyaminywili na Kipugira vilivyopo wilayani Rufiji na kuyaingiza katika mpango wake wa kuyafanyia utafiti ili kuweza kufikisha mawasiliano ifikapo Aprili 2010.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wake, kampuni ya simu za mkononi za *VODACOM* imefanya utafiti wa kimasoko katika maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge kwa nia ya kuboresha huduma ya mawasiliano.

Aidha kampuni hiyo imefanya utafiti wa kiufundi ili kubaini sehemu za kuweka minara na hatua mbalimbali za mchakato na utekelezaji zimeanza. Ujenzi wa minara hiyo utaanza mara tu baada ya mchakato huo kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *TIGO* inatarajia kufanya utafiti wa masoko katika maeneo ya vijiji vya Mloka, Kilimani, Mtanza, Nyaminywili na Kipugira Wilayani Rufiji katikati ya mwaka huu wa 2009. Aidha, iwapo maeneo hayo yakionekana kuwa yanakidhi mahitaji ya kimasoko, itajengwa minara ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *ZANTEL* inaendelea kupanua mtandao wake katika maeneo mbalimbali nchini. Katika wilaya ya Rufiji, tayari kampuni hiyo imejenga minara ya mawasiliano katika maeneo ya Pagae, Ikwiriri ni Muhoro. Aidha, ZANTEL

ipo mbioni kujenga mnara huko Utete na baadaye kuendelea kwenye maeneo mengine ikiwa ni pamoja nay ale yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia itaendelea na jitihada zake kuyashawishi Makampuni ya Simu za Mikoni kuongeza na kuboresha huduma ya mawasiliano ni makubwa na muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. Nanichukue nafasi hii niwaombe waheshimiwa wananchi wote kwamba wawe na subira na shughuli hizi tunazoshughulikia.

**SPIKA**: Wakati tunaendelea napenda Waheshimiwa Wabunge mtambue kwamba Waheshimiwa Kampteni Komba, Msindai, Misanga sasa wamejipanga pamoja na sielewi sijui wamewasiliana na kwa *ZAIN* au kwa kitu gani na Mwinchom ameongezeka hapo hapo. (*Kicheko*)

**MHE. PROF. IDRIS MTULIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana nataka niulize swali moja la nyongeza, naomba nishukuru majibu mazuri ya Naibu Waziri naomba tu kusahihisha kile kijiji kinaitwa Nyaminywili na kwamba wanakijiji wa Mtaza, Nyaminywili na Kipugila wamemsikia Naibu Waziri kwamba Aprili mwakani Ishallha, mambo yatakuwa mazuri.

Kwa vile asilimia 80 ya Watanzania wanakaa vijijini, je ingekuwa jambo la busara sasa kwa Serikali kuzungumza na waweagizaji wa *mobile phones*, walete *long distance mobile phones*.

Kuna tokea suala hili la biashara na gharama katika kupeleka huduma za mawasiliano vijijini, lakini tulipitisha sheria ya kuwasaidia makampuni yote yanayopeleka huduma vijijini kuwafidia kwa gharama zao zile. Je, mpaka sasa ni makampuni mangapi ya simu za mkononi zimepata fidia hizo hasa kwa wilaya ya Rufiji?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, napenda niwahakikishie wananchi wa Rufiji kwamba mawasiliano ya simu za mikononi si *luxury* kwa hiyo yatafikishwa maeneo yote hayo kutoka na hali halisi za makampuni ya mawasiliano ya simu yatakavyokuwa.

Suala la *long distance mobile phones* mimi kidogo linanitatizo kidogo kwa sababu sijui ni zipi kwa sababu mimi najua ukiwa na simu kama, athoraia ambayo ni satellite unaweza ukapata mawasiliano popote ulipo nchini Tanzania. Lakini hizi ni ghali kwa wananchi wetu vijijini kuweza kuzimudu tunachokifanya  hiki sasa ni kuhakikisha kwamba mkondo wa mawasiliano unafika katika maeneo yote na tayari shughuli hii imeanza na nakubaliana naye kwamba 80% ya wananchi wetu wanaoishi vijijini na hawa ndiyo wanaofanya  sisi tuishi mijini kwa sababu wao ndiyo wanao-*produce*, wao ndiyo wanaolima, wao ndiyo wanaofuga kwa wingi na wao ndiyo wanaotutosheleza sisi kwa chakula na wao ndiyo wanaopeleka chakula hiki nje tukapata sisi pesa sisi pesa za kigeni. Kwa hiyo,  ni jukumu letu kuhakikisha kwamba mawasiliano yanaboreka ili na wao waweze kutumia mawasiliano kwa ajili ya kuendeleza nchi hii ya Tanzania.

**MHE. TEDDY L. KASELA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa sehemu ya Mbutu katika jimbo la Bukene inafanana katika ahadi kama ile ya swali la msingi kwamba waliahidiwa kwamba watawekewa mnara pale Mbutu katika kata ya Mambali, na kwa kuwa sehemu kubwa ya wakulima wa Semembela pamoja na Wakamahalanga wanahitaji sana simu na mimi nimekwenda kuweaona hao watu *ZAIN* wakaniahidi kwamba wataleta mnara baada ya kufanya research kwenye sehemu zingine ambazo hawana soko zaidi wameweka mnara lakini hawana soko kubwa kama sehemu hizo nilizozitaja. Je, Serikali inasemaje kuleta mnara ule wa Mbutu na vilevile sehemu zile nilizozitaja?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru Mheshimiwa Teddy kwamba na mimi amenipunguzia kidogo mzigo wa kugombana na makampuni ya simu kwamba yeye mwenyewe alichukua juhudi ya kuwaona. Sasa mimi nitaanzia hapo Mheshimiwa Kasela-Bantu ulipoishia wewe kuendelea kuwashawishi makampuni ya simu waone umuhimu kufika Bukene na maeneo ambayo umeyataja. *(Makofi)*

Lakini nataka niseme kwamba jamani nchi yetu ni kubwa mnara mmoja una-*cost* kuanzia laki tatu mpaka lakini nne dola, sasa kufikisha mawasiliano katika maeneo yote kwa wakati mmoja kwa makampuni inakuwa ni vigumu kidogo lazima tutakwenda kwa awamu na nina hakika hilo ndilo linalofanyika.

Tunapoahidi hapa au wanapoahidi ni kwamba wanaweka zile *business plan* zao na *role out plan* zao pembeni kukidhi mahitaji yale ya haraka tunawapelekea. Kwa hiyo, ukipata wewe ni kwamba mwenzako kule amenyimwa ile nafasi ya mawasiliano.

Lakini tutaendelea kama kawaida kuhakikisha kwamba makampuni haya ya simu yanafika vijijini ambapo wananchi wengi wapo ili wananchi wengi waweze kuyatumia mawasiliano kwa kuleta maendeleo yao na nchi kwa ujumla. Bukene nayo haijasahauliwa. *(Makofi)*

Na. 50

**Askari Walioshiriki vita vya Nduli Iddi Amin**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

Kwa kuwa, ni muda mrefu sasa kumekuwa na malalamiko juu ya kupuuzwa kwa wale askari walioshiriki vita vya Nduli Iddi Amin.

(a) Je, mpaka sasa imehakiki vipi kujua idadi ya askari hao?

(b) Je, Serikali inawasaidiaje wastaafu hao ambao baadhi yao wamekuwa walemavu wa viungo?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, jumla ya mashujaa walioshirikia katika vita ya kumng'oa Iddi Amini ni 28,701 wakiwemo JWTZ 19,762, JKT 470 na majeshi mengine ya usalama 8,469. Serikali haijawahi kumpuuza askari ama mtu yoyote aliyeshiriki katika vita hivyo badala yake imeendelea kuwaona ni mashujaa waliosaidia katika kulikomboa taifa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambau kuwa wastaafu wengi wakiwemo mashujaa wa vita wanapokea pensheni ambazo hadhikidhi hali ngumu ya maisha iliyopo hivi sasa.

Aidha Serikali imechukua hatua ya kurekebisha pensheni ili kukidhi hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu walemavu wa vita waliorekodiwa ni 146, Serikali inawasaidia walemavu hao kwa kuwalipa "*Disability Pension*" na baadhi yao wanahudumiwa kwa kupewa viungo bandia, pikipiki za miguu mitatu na vifaa vya kufanyia kazi na ufundi kama "*TOOL BOX*".

Mheshimiwa Spika, inakabiliwa na changamoto ya walemavu wa vita wanaojitokeza hivi sasa ikiwa ni matokeo ya muda mrefu baada ya kuumia.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru ingawa nimeshtuka kwa sababu majibu aliyoyasema Mheshimiwa Waziri hapo sio ambayo nimeletewa mie kwa maandishi hapa.

Sasa hii dispality ya ajabu sana. Hata hivyo namshukuru kwa majibu yake mazuri ingawa mimi nimetaka kujua wale wengine waliokuwa sio walemavu wanasaidiwaje, kwa sababu askari wengi wapo ambao sio walemavu. Je, wanasaidiwa vipi hawa?

**SPIKA**: Mheshimiwa Khalifa usishituke kwa mujibu wa Kanuni zetu Serikali Mawaziri wanaruhusiwa kuendelea kulihariri jibu hadi litosheleze kwa hiyo ni kwa nia njema tu.

**NAIBU WA WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza naomba nimwombe radhi kwa majibu kutofautiana, ukweli ni kwamba swali hili tumepewa jana mchana na majibu yakawa yameshaletwa kabla sijayatazama kama mwenye dhamana ya kutazama. Kwa hiyo, naomba radhi sana, lakini baada ya kuyapitia ndiyo nikagundua kwamba majibu hayafanani na swali lililoulizwa. Kwa hiyo, kwa haraka nimefanya marekebisho ambayo yanakidhi haja ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba niseme tena kwa wale wastaafu wa kawaida waliotokana vita ile tunaendelea kufuata Sheria kwa kigezo cha *disability allowance* ambacho kinatokana na *Defence Act*, tutaendelea kuboresha Sheria hii ili kukidhi mambo mengine muhimu kwa faida ya Askari wetu hawa.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, ingawa muda wa maswali sasa umefikia ukomo ningeomba tumalize angalau maswali mawili ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na kuahirisha yale mawili ya Wizara ya Fedha.

Kwa hiyo, swali linalofuata ambalo lilikuwa liulizwe na Mheshimiwa Lucas L. Selelii, linaulizwa na Mheshimiwa Nkumba.

Na. 51

**Kero za Ukosefu wa Maji safi na Salama**

**MHE. SAID JUMA NKUMBA (K.n.y. MHE. LUCAS L. SELELII)** aliuliza:-

Kwa kuwa, tatizo la maji vijijini limekuwa sugu na kero kwa kipindi kirefu; na kwa kuwa sera ya maji inaelekeza kuwapatia wananchi maji safi na salama, karibu na maeneo yao; na kwa kuwa, miradi mingi kama ile ya Benki ya Dunia *RWSSP*, *QUICK WINS* na kadhalika, haijakidhi kutatua au kupunguza kero hii.

Je, Serikali ipo tayari kutoa kipaumbele cha pili kwa sekta hiyo baada ya elimu katika Bajeti ijayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ipo haja ya kuongeza fedha za utekelezaji wa miradi ya maji. Hata Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wa Serikali wanaliona na kusisitiza jambo hili, kwa mfano, Mheshimiwa Mbunge atakumbuka kwamba tarehe 24 Julai, 2008, Mheshimiwa Waziri Mkuu, akijibu swali la Mheshimiwa Peter J. Serukamba Mbunge wa Kigoma Mjini, katika kipindi cha

Maswali kwa Waziri Mkuu alisisitiza umuhimu wa Serikali kuongeza Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Hata hivyo kwa kuwa sasa mwongozo wa Bajeti ya 2009/2010 ndiyo umekamilika ni mapema mno kutaja vipaumbele vya bajeti hiyo lakini matumaini yetu ni kwamba Serikali itatega kiasi cha kutosha kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kero ya upatikanaji wa maji vijijini, mwaka 2002 Serikali ilianzisha Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijni katika Wilaya 14 za Rufiji, Kilosa, Mpwapwa, Morogoro, Kiteteo, Handeni, Kilindi, Kongwa, Kondoa, Manyoni, Singida, Iramba, Igunga na Mvomero. Mradi huu uliotekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia ulikuwa kwa majaribio ya utekelezaji wa sera ya maji ya mwaka 2002. Uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wake ndio unaotumika hivi saa kutekeleza programu ya maendeleo ya maji.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa programu ya maendeleo ya sekta ya maji kwa hatua iliyofikiwa hivi sasa utaratibu uliopo ni kwamba Halmashauri zote zinatakiwa kuleta Wizarani mapendekezo yao ya rasimu za mikataba ya ajira za wataalam washauri na Wizara ikisharidhika inapeleka mapendekezo hayo Benki ya Dunia ili kupata kibali cha kuziruhusu Halmashauri kuendelea na taratibu za ajira.

Halmashauri zimefikia hatua mbalimbali katika mchakato wa kutafuta wataalam washauri ambao watafanya usanifu wa miradi ya maji na kusimamia ujenzi wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, wakati Halmashauri nyingine ziko katika hatua za mbele katika mchakato huo Halmashauri 8 za Nzega yanyewe, Ukerewe, Pangani, Tabora Manispaa, Sikonge, Uyui, Igunga na Urambo zimerudishiwa rasimu ili zifanye marekebisho baada ya kufanyiwa mapitio na Wizara kabla ya kuwasilisha Benki ya Dunia. Aidha, Halmashauri nne za Temeke, Ilala, Kinondoni na Rombo hazijawasilisha rasimu zao Wizarani. Kwa sasa ni Halmashauri nane tu za mbeya vijijini, Hai, Moshi Vijijini, Serengeti, Bunda, Mpanda, Lindi Vijijini na Nanyumbu ndizo zimekwishapata ridhaa ya Benki ya Dunia Kusaini mikataba na wataalam washauri.

Nachukua nafasi hii kuzitaka Halmashauri zote ambazo bado hazijawasilisha taarifa zao kufanya hivyo mapema iwezekanavyo kwa kwa kuwa kwa kuchelewesha taarifa zao wanachelewesha pia utekelezaji wa mradi. Wizara yangu iko tayari kupeleka wataalam kuzisaidia Halmashauri hizo katika kuandaa mapendekezo yao. Lengo letu ni kwamba ifikapo tarehe 30 Mei, 2009 washauri wawe wameanza kazi za usanifu katika Halmashuri zote.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa programu ya maendeleo ya sekta ya maji unakadiriwa kugharimu Dola za Kimarekani milioni 951. Kati ya fedha hizo Serikali ya Tanzania itachangia Dola milioni 251 na dola milioni 700 zitachangiwa na washiriki wetu katika maendeleo.

**MHE. SAID JUMA NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwenye elimu kwa kutoa kipaumbele tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa na kwa kuwa tatizo la maji ni kubwa sana hasa nyakati za kiangazi kina mama wanasumbuka sana kutafuta maji vijijini na baadhi ya miradi mingi sana imekwama kutokana na ukosefu wa maji.

Sasa kwa nini Serikali haikubaliani nami kama ambavyo tumeuliza katika swali la msingi kwamba upo umuhimu angalau wa kutoa kipaumbele cha pili cha kuhakikisha kwamba basi sekta hii ya maji inapewa kipaumbele ili kuondoa hili tatizo ambalo limekuwa sugu la ukosefu wa maji katika maeneo mengi nchini?

La pili, kwa kuwa Wilaya ya Sikonge ni moja ya Wilaya zilizorudishiwa rasimu zao kufanya marekebisho na kwa kuwa mchakato huu unachukua muda mrefu sana je, miradi mikubwa kama ule mradi wa Bwawa la Ulyanyama ambao Wilaya ya Sikonge umeuanzisha Serikali itakuwa tayari kuukamilisha haraka iwezekanavyo ili wananchi wa Sikonge waweze kupata maji safi na salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu tafadhali. Lakini huku nikimkumbusha Mkurugenzi wa Halmashauri ya Urambo aharakishe sana, haraka kabisa kufikisha ile rasimu inayotakiwa pale Wizarani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Said Nkumba, kama ifuatavyo:-

Kuhusu kufanya kipaumbele cha pili baada ya elimu kwa upande wa Wizara au Sekta ya Maji mimi sikusema Serikali haikubaliani, nimesema kwamba mchakato wa Bajeti ndiyo hivyo umekamilika nadhani itakuwa ni vibaya mimi nikianza ku-*pre empty* Waziri mwenye dhamana kuanza sasa kueleza utaratibu utakaotumika.

Ndiyo maana nimesema bado ni mapema mno mimi kusema lakini nimesisitiza kwamba hata Mheshimiwa Waziri Mkuu akijibu swali kwa Mheshimiwa Peter J. Serukamba, alionyesha umuhimu na nia ya kuiongezea fedha sekta hii au Wizara hii.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, muda si mrefu tutaingia katika mchakato huo na baadaye tutapata majawabu na nina hakika Serikali iliahidi jambo hili litafanyika.

Kuhusu mradi wa Ulyanyama labda niseme kwa ufupi tu kwamba kwa kuwa Bwawa hilo liko katika utaratibu na linaendelea kujengwa, mimi kama ninavyosema siku sote sipendi miradi viporo iendelee kuwepo. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatoa kipaumbele kwa Bwawa hili likamilike. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa agenda ya wakandarasi katika kutatua tatizo la maji kwa wananchi wa vijijini ni ukweli haligusi hasara hiyo kuwakumba wananchi zaidi ya Watendaji ambao ndiyo wenye wajibu wa kufanya hiyo kazi kwa ukamilifu na wananchi wetu wapate maji.

Je, Serikali haioni iko sababu maalum kabisa ya kupitia upya vigezo hivyo vya mradi wa maji wa Dunia ili kurahisisha namna bora ya kuhakikisha maji hayo yanawafikia wananchi wetu wa vijijini wakiwemo wa kule Matimila, Maweso na Vijiji vingine vya Jimbo la Peramiho?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji alipotoa kauli ya Serikali hapa alieleza hapa utaratibu ambao tumeufanya kuiomba Benki ya Dunia kupunguza angalau baadhi ya masharti, kulegeza ili Halmashauri zetu ziweze kukidhi. Walifanya hivyo na tunachofanya hivi sasa ni kwamba tunaangalia yale ambayo yalilegezwa Halmashauri zetu nazo ziyakidhi.

Mimi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Jenista J. Mhagama kwamba tatizo halipo tu kwenye masharti yale, lipo katika uwezo mdogo katika Halmashauri zetu. Kwa hiyo, hatua ambayo tunaichukua sisi kama Wizara kama nilivyosema katika jibu langu la swali la msingi ni kuwatumia Halmashauri hizi wataalam wetu wa Wizara ya Maji ili wasaidie kutafsiri yale masharti yaliyomo na kuhakikisha kwamba mchakato huu unakamilika na kuwasilisha rasimu mapema.

Kwa hiyo, *weakness* iko katika Halmashauri zetu na sisi kazi hiyo tutaifanya kuwasaidia Halmashauri za Wilaya.

Na. 52

**Upatikanaji wa Maji Safi na Salama na ya Kutosha Vijijini**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ni lengo la Serikali kuhakikisha kuwa upatikanaji wa maji safi, salama na ya kutosha katika maeneo ya vijijini, na kwa kuwa vijiji vya Makawa, Mkoka,

Songambele, Njoge, Mseta na kadhalika Wilayani Kongwa viko katika programu ya *RWSSP* inayofadhiliwa na Benki ya Dunia awamu ya pili:-

Je, Serikali inasema nini juu ya ahadi ya kuvipatia maji vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji na usafi wa mazingira vijijini ulianza kutekelezwa kwa majaribio mwaka 2002 katika wilaya ya 14 nchini ikiwemo Wilaya ya Kongwa. Uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa mradi huo ndio unaotumika katika utekelezaji wa programu ya Maendeleo ya Sekta ya maji inayoendelea kutekelezwa katika Halmashauri zote nchini, kwa lengo la kuwapatia wananchi mijini na vijijini maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia utaratibu wa utekelezaji tuliojiwekea, Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ilichagua vijiji kumi vya Makwa, Mkoka, Songambele, Njoge, Mseta, Mlali, Ngomai, Ng'umbi, Mlanje na Chingwingwiri kuwa katika awamu yake ya pili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatai utaratibu wa utekelezaji tuliojiewekea, Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ilichagua vijiji kumi vya Makawa, Mkoka, Songambele, Njoge, Mseta, Mlali, Ngomai, Ng'umbi, Mlanje na Chingwingwiri kuwa katika awamu yake ya pili ya utekelezaji.

Kama ilivyo kwa Halamshauri zote nchini, mchakato unaendelea kufanywa ili kuwaajiri wataalam washauri watakaofanya usanifu wa miradi na kusimamia ujenzi wake.

Kwa upande wa Halmashauri ya Kongwa, utekelezaji unakwenda vizuri kwa sababu Halmashauri ilikwishawasilisha Wizarani rasimu ya mkataba wa kumwajiri mtaalam mshauri na Wizara baada ya kuridhika imepeleka mapendekezo kwa Benki ya Dunia ili itoe kibali kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kusaini Mkataba wa ajira ya Mtaalam Mshauri. Matarijio yangu ni kwamba mshauri ataanza kazi mwezi Mei, 2009 ili ujenzi wa miundombinu ya maji uanze katika mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyosema awali Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ilipata bahati ya kuwa katika awamu ya kwanza ya majaribio ilivyojumuisha Wilaya 14. Hata hivyo kwa bahati mbaya utekelezaji wake uligubikwa na matatizo mbalimbali ikiwemo uwezo mdogo wa Halmashauri kusimamia utekelezaji, wizi wa vifaa vya miundombinu ya maji, uwezo mdogo wa mkandarasi na wataalam washauri.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004 mji mdogo wa Kibaigwa ulikuwa miongoni mwa Miji tisa (9) iliyokubaliwa kupewa ufadhili wa Serikali ya

Ufaransa kupitia Shirika lake la Maendele la *AFD.* Kwa bahati mbaya Serikali ya Ufaransa haikuweza kutekeleza kikamilifu mradi huo kutokana na gharama kuwa kubwa. Hatua iliyofikiwa kwa mradi wa Kibaigwa ni kukamilika kwa usanifu na makabrasha ya zabuni za ujenzi.

Serikali imeamua kutumia usanifu na makabrasha hayo kutekeleza mradi wa maji wa Kibaigwa kupitia program ya maendeleo ya sekta ya maji. Tayari zabuni ya ujenzi imekwishatangazwa na mchakato wa kumpata mkandarasi wa ujenzi unaendelea. Namwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kongwa waendelee kuwa na subira na imani kwamba mradi huu sasa utatekelezwa.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza lakini nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri kuhusiana na awamu ya pili ya mradi huu utakaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Maswali yangu mawili madogo yatajikita kwenye awamu ya kwanza ambayo ndiyo inamalizikia mwaka 2009. Amekubaliana nami kwamba wakandarasi wabovu, washauri wasiofaa na baadhi ya Watendaji wa Halmashauri ikiwa ni pamoja na Watendaji wa Wizara yake ya Maji wabovu ndiyo wamesababisha utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huu usiende vizuri. *(Makofi)*

Kwa mfano, mashine zote zilizoletwa Kongwa ambazo *procurement* ilifanywa na Wizara ni mbovu hadi hivi sasa hazifanyi kazi na Wizara ndiyo ilifanya *procurement.* Je, ni hatua gani zitachukuliwa kwa Watendaji wa Wizara ambao wamehusika na *procurement* hii ya mashine hizo?

La pili, katika awamu hiyo hiyo ya vijiji 10 katika Wilaya ya Kongwa ambayo 2002/2009 miaka 7 mpaka leo kijiji cha Mautya hakina maji, Manungu hawanywi maji, Iduo hawapati maji, Leganga hakuna maji, Kiteto hakuna maji, Hembahemba hakuna maji, Chamaye hakuna maji, Kongwa mjini bado ni matatizo, katika miradi 10 miradi 7 haifanyi kazi leo, tunapokwenda awamu ya pili awamu ya kwanza haijakamilika. Mheshimiwa Waziri anawaambia nini wananchi wa Kongwa ambao shida ya maji ndiyo kipaumbele chao cha kwanza kuliko chochote kingine? (*Makofi*)

**SPIKA:** Pole sana Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Job Y. Ndugai kama ifuatavyo.

Kwanza kuhusu vifaa ambavyo havifanyi kazi mimi mwenyewe nilitembelea Kongwa na nimezuru mradi ule wote, nimepitia pia baadhi ya makabrasha yaliyotumikana ndiyo maana nimekiri kwamba kweli kulikuwa na udhaifu katika

kusimamia na siyo tu kwa wataalam kutoka Wizara yangu lakini katika mfumo mzima kuanzia katika ngazi ile.

Mheshimiwa Spika, hatua ambazo tunaendelea kuchukua hivi sasa ni kwamba tunachunguza yaliyojitokeza katika hilo kwa sababu mambo kama haya wakati mwingine yanapotokea kuna masuala ya kisheria yanatakiwa yafuatwe. Halafu kuna mambo mengine yanatakiwa tu kufuatwa tu kwa kuelekezana na kufuatana na taratibu za kazi. Nataka nimwahidi Mheshimiwa Job Y. Ndugai kwamba kwa upande wa Wizara kama ikidhihirika kwamba Watendaji wa Wizara yangu ndiyo wame *procure* mashine mbovu na kama wamefanya hivyo kwa makusudi na wala siyo kwa bahati mbaya basi Wizara itachukua hatua, na tutachukua hatua kuwawajibisha hasa tukianza na taratibu zenyewe za kikazi maana yake ziko taratibu za kikazi katika kuwawajibisha Watendaji kama hao. *(Makofi)*

Mimi nafikiri siyo tu kwa Watendaji wa Wizara yangu bali ni pamoja na Watendaji karibu wote ambao wanasimamia miradi ya maji. Tunafanya kazi hiyo kujitahidi kutazama ni wapi ambapo wamefanya makosa. Kuhusu awamu hii ya pili, awamu ya kwanza ambayo pia haijakamilika, nataka nimwahidi Mheshimiwa Ndugai kwamba tuliweka utaratibu tangu miaka miwili iliyopita kwamba wakati tunasubiri hii miradi inayotekelezwa na *Water Sector Development Program* tuliweka utaratibu ule wa *Quick Wins* na kwamba pale ambapo haijakamilika basi tuhakikishe kwamba angalau miradi hii tunaikamilisha. Kwa hiyo, nataka nimwahidi kwamba hatuwezi tukaingia awamu ya pili na miradi mingine haijakamilika tukaiacha hivi hivi tutaitazama na tutaiangalia na tutatafuta ufumbuzi wa kuwasaidia wananchi hawa aliowataja Mheshimiwa Mbunge ili wapate maji wakati awamu ya pili nayo inaendelea. (*Makofi*)

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. GODGREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68(8). Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, alipokuwa akijibu swali langu alisema miongoni mwa Kata ambazo zilifanyiwa utafiti kuhusu ufanisi wa mbolea ya Minjingu alisema zote ziko Jimbo la Mbozi Mashariki na ziko 13.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa taarifa sahihi naomba niweke Kumbukumbu vizuri kwamba siyo Kata zote ziko Jimbo la Mbozi Mashariki, Kata ya Chiwezi na Kata ya Tunduma ziko Jimbo la Mbozi Magharibu. Sasa wananchi wanaposikia haya yanazungumzwa na usahihi haufanywi wanaweza wasituelewe sisi wawakilishi tunaotoka maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, ninataka kuweka Kumbukumbu sahihi. Ahsante sana.

**SPIKA**: Hiyo haihitaji mwongozo imeingia kwenye *Hansard* na itasomeka hivyo na wananchi wa Mbozi ambao pengine wanaangalia nina hakika sasa baada ya kauli yako wameelewa kwa usahihi na ninafikiri Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame amefarijika.

Waheshimiwa Wabunge, leo nimeteleza sikuweza kufikisha maswali yote yakajibiwa lakini ndiyo ubinadamu huo. Kwa hiyo, maswali mawili ya Wizara ya Fedha na Uchumi tutayapangia muda wake wiki ijayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naanza na wageni. Tunao wageni wa Mheshimiwa Waziri wetu wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lawrence K. Masha, nao ni wageni 13 kutoka katika Jimbo lake la Uchaguzi la Nyamagana. Hao wanaongozwa na Bwana Zebedayo Athuman, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Nyamagana, ninaomba asimame. Nadhifu kabisa na suti, unajua tena mtu anayetoka Jiji la Mwanza hawezi kuwa ..….(*Makofi*)

Bwana John Minja ni Naibu Mstahiki Meya wa Jiji la Mwanza, na Bwana Itimbula Katibu wa Mbunge. Karibuni sana kutoka Nyamagana na Mwanza tunafurahi kuwaona hapa, nina hakika Mbunge wenu anawaangalia vizuri. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, ambao ni Mama Lina Mwakyembe mkewe Mheshimiwa, karibu sana Mama! Pamoja naye wapo wawakilishi wa Kata sita za Jimbo la Kyela wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Kata ya Ngana, Ndugu Jacob Sichone.

Naomba wageni wetu wa Kyela wasimame kwa sababu ni utaratibu ingawa hatukuwatajwa wote. Karibuni sana na ahsanteni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye na Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa na Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya, ambao ni Wajumbe 19 wa Kamati ya masuala ya UKIMWI ya Wilaya ya Rungwe wakiongozwa na Waheshimiwa Madiwani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mackson Mwakipunga, Diwani wa Kata ya Lufilyo, ambaye ndiye Mwenyekiti. Karibu sana.

Mheshimiwa D. Kasigila Diwani wa Kata ya Masoko, Mheshimiwa T. Mwakalalile, Diwani Viti Maalum. Basi ningeomba wageni wote wale wa Runge kwa sababu walitajwa ni 19 wasimame na hao Viongozi wao tuwatambue. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Fatma Othman Ally ambao ni wanafunzi 10 na walimu kutoka Shule ya Langoni Jimbo la Dole. Wageni wetu kutoka Zanzibar, karibuni sana na tunafurahi sana kuwaona Ndugu zetu kutoka Zanzibar, mara kwa mara mkija hapa Dodoma, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa James P. Musalika ni Makatibu wa CCM wa Kata za Jimbo la Nyang’wale wakiongozwa na Ndugu Julius Musabila, naomba asimame. Ndugu Zambi Meleka Katibu wa Mbunge na Ndugu Sayi Msaidizi wake. Basi Wajumbe kutoka Jimbo la Nyang’wale naomba wote msimame tafadhali. Karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Juma H. Killimbah kutoka Iramba Magharibi, Mzee Israel Shalua, karibu sana Mzee.

Yupo Meneja Mkuu au Mkuu wa Shirika la Ndege la *Quarter Airways* Bwana Chibole, huduma zenu ni nzuri naomba mziendeleze hivyo hivyo, karibu sana. (*Makofi*)

Wanafunzi 30 kutoka Chuo cha Technolojia cha Mtakatifu Philipo Kongwa Dodoma, hawa watakuwa ni wageni wa Mheshimiwa Job Y. Ndugai, poleni sana kwa tatizo la maji lakini Serikali inalishughulikia. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wanafunzi 50 kutoka Chuo cha Mipango Dodoma, karibuni sana tunawatakia mema katika masomo ili mje muisaidie nchi katika fani hiyo ya mipango.

Basi, sasa matangazo ya shughuli zetu nyingine. Kwanza kutakuwa na kikao cha dharura kifupi cha Kamati ya Uongozi ya Bunge mara baada ya matangazo haya. Kamati ya uongozi Wenyeviti wote ama kama Wenyeviti hawapo basi Makamu Wenyeviti kutakuwa na kikao pale katika ukumbi wangu yaani ukumbi wa Spika mara baada ya matangazo haya.

Kwa tangazo hili basi yale matangazo mengine yote ya mikutano na vikao yazingatie kwamba Wenyeviti au Makamu Wenyeviti wanahitajika kwanza kwenye kikao cha Kamati ya Uongozi ili tumalize agenda za Kamati ya Uongozi.

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo ya Kilimo, Mifugo na Maji, mkutane saa sita mchana katika Ukumbi Namba 227.

Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma (*POAC)* anaomba Wajumbe wakutane leo saa saba mchana katika Ukumbi Namba 231. *(Makofi)*

Mheshimiwa Alhaji Mohamed H. Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu mkutane saa tano asubuhi hii katika ukumbi wa Pius Msekwa. Nadhani kuna mashauriano pengine kuna wadau maana yake ukumbi mkubwa.

Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini mkutane saa saba mchana katika Ukumbi Namba 219.

Mheshimiwa John M. Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo mkutane saa nne unusu, hii ndiyo inagongana na Kamati ya Uongozi hii yaani mara baada ya matangazo haya katika ukumbi namba 231.

Waheshimiwa Wabunge, natumaini ama Mwenyekiti, ama Makamu Mwenyekiti basi atajiunga nasi kwenye Kamati ya Uongozi.

Mheshimiwa Willsona M. Masilingi Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama anahitaji Wajumbe wa Kamati hiyo mkutane saa tano asubuhi na hii nayo inagongana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Labda ni kikao cha pamoja.

Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, anahitaji Wajumbe wa Kamati yake wafanye kikao muhimu na Kamati ya Wananchi wenzetu wenye ulemavu saa saba mchana katika Ukumbi wa sherehe yaani *Basement*.

Kwa hiyo, Kamati ya huduma za Jamii itakutana na Viongozi wa Kamati ya Watu wenye ulemavu saa saba mchana huu katika Ukumbi wa sherehe pale *Basement*.

Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud Mwalimu, Msaidizi wa *Bunge Sports Club* anatangaza kwamba gari la kwenda mazoezini sasa ni tayari na kwa wale wote wanaoshiriki basi wawepo kwenye vituo vyao kuanzia saa kumi na moja alfajiri. Doh! Hakuna hata kuswali tena ni masoezi tu. (*Kicheko*)

Ofisi ya Katibu wa Bunge inawatangazia kwamba kesho kutakuwa na Semina ya Masuala ya Utumishi wa Umma *(PSRP II)* itakayotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Saa 4.00 Asubuhi Ukumbi wa Pius Msekwa; Semina kuhusu Mpango Awamu ya Pili, Mpango wa Kuboresha Utumishi wa Umma ambayo inatolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Semina hiyo itakuwa saa 4.00 asubuhi Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, kama nilivyosema, sisi wa Kamati ya Uongozi tuna Kikao kifupi. Kwa hiyo, namwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Job Ndugai aweze kuja ili kuendeleza shughuli zilizosalia.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**KAULI ZA MAWAZIRI**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Ulinzi na Usalama katika Mkoa wa Mara si ya kuridhisha kumekuwa na matukio ya mara kwa mara ya mauaji ya ukoo, wizi wa mifugo, ujambazi wa kutumia silaha na biashara ya madawa ya kulevya hususani kilimo cha bangi. Matukio hayo yameenea zaidi katika Wilaya za Tarime, Rorya na Musoma Vijijini. Chanzo cha mapigano baina ya koo na koo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapigano baina ya koo na koo yanatokana na sababu nyingi ikiwa ni pamoja na zifuatazo:-

Migogoro ya ardhi hasa kugombani mipaka ya mashamba na malisho ya mifugo. Idadi kubwa ya wananchi wa Wilaya za Tarime na Rorya huishi kiukoo kwenye vijiji. Kutokana na ongezeko la mahitaji ya ardhi katika vijiji, kijiji huvamia ardhi ya kijiji kingine hivyo huzuka mapigano makali baina yao na kusababisha vifo na uharibifu wa

mali. Koo ambazo hupigana mara kwa mara ni Wahunyanga na Wamera, Walyanchari, Waliyanchoka na Wakila na koo nyingine ni Wanyambasi na Walegi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizi wa mifugo. Sababu nyingine ambayo imekuwa ni chanzo cha mapigano biana ya koo na koo ni wizi wa mifugo. Mifugo inapoibiwa mara nyingi husafirishwa kwenda nchi jirani ya Kenya ambako inasadikiwa uuzwa kwa bei kubwa kuliko hapa nchini. Lakini pia hivi karibuni Askari wanaosadikiwa kuwa wa Jeshi la Polisi la Kenya waliingia na Tanzania na kuiba ng’ombe na kuua raia. Aidha, wizi wa mifugo hutokea wakati wa sherehe za kimila kwa ajili ya mahitaji ya chakula cha watu wanaohudhuria sherehe hizo, kipindi hicho vijana wa ukoo mmoja huiba ng’ombe katika ukoo mwingine, hivyo husababisha mapigano baina ya koo na koo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mila na desturi zilizopitwa na wakati. Mila na desturi za baadhi ya makabila zinachochea mapigano baina ya vijana wa koo moja na wa koo nyingine. Vitendo hivyo vinaheshimika miongoni mwa jamii hizo kuwa ni vya kishujaa. Wazee wa kimila ndiyo viongozi na waamrishaji wa mapigano hayo, na wazee hao wana madaraka makubwa katika koo zako na hutoa adhabu kali kwa vijana wanaokwepa kushiriki mapigano. Wazee hao hunufaika na mapigano hayo kwa kupata mgao wa mali zilizoporwa katika mapigano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha bangi ni chanzo kikubwa cha uchumi kwa baadhi ya makabila katika Mkoa wa Mara. Bangi hiyo uuzwa ndani na nje ya nchi imekuwa ni kawaida kwa watu katika maeneo hayo kukodishwa na Wakala kulima bangi na kulipwa fedha nyingi. Pale inapotokea kwa mkulima aliyekodishwa hakufanikiwa kuvuna bangi kutokana na bangi hiyo kuharibika kutokana na ukame au kuharibiwa na vyombo vya dola mkulima huyo hutakiwa kurudisha fedha hizo alizopewa na Wakala wake. Ili kupata fedha ya kurudisha mkulima huiba ng’ombe wa ukoo jirani, wanaukoo walioibiwa ng’ombe hujikusanya na kwenda kupambana ili kurudisha ng’ombe waliobiwa. Katika hali hiyo, vita kubwa hutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madhara ya mapigano ya koo. Kwa mujibu wa takwimu za kipindi cha miaka minane kuanzia mwaka 2001 hadi Machi, 2009 watu wapatao 136 walifariki na zaidi 336 walijeruhiwa, nyumba 2, 421 zilichomwa moto na kuacha zaidi ya kaya 756 zikiwa hazina mahali pa kuishi, na vihenge 673 vya kuhifadhia chakula vilichomwa moto na kuharibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kukabili tatizo la mapigano ya koo. Serikali imekuwa ikijitahidi kushughulikia tatizo hili. Mwaka 2006 aliyekuwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa aliunda Timu ya Wataalam kutoka Idara ya Serikali ili kubaini viini vya mapigano na kupendekeza jinsi ya kumaliza mapigano hayo. Wataalam hao walibaini vyanzo vya mapigano na kutoa mapendekezo. Miongoni mwa mapendekezo waliyoyatoa ni pamoja na kuwashiriki wazee wa mila, kuimarisha Mabaraza ya Ardhi, kuimarisha miundombinu ya barabara, kutoa elimu kwa wananchi ili waache mapigano, kuzishirikisha taasisi za dini ili kueneza dini katika jamii ya makabila yanayohusika na kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama. Mapendekezo hayo yameendelea kufanyiwa kazi kama ifuatavyo:-

Moja, Jeshi la Polisi limeendelea kufanya *operation* za mara kwa mara kudhibiti mapigano ya koo na vitendo vingine vya uhalifu pamoja na kutoa elimu kupitia Mpango Polisi Jamii ili wananchi wafuate sheria za nchi.

Pili, kuzifanya Wilaya ya Tarime na Rorya kuwa Mkoa wa Kipolisi ili kukabiliana ipasavyo na matishio ya usalama, uhalifu na wahalifu.

Tatu, Serikali ya Mkoa wa Mara kupitia TAMISEMI imefanya kampeni mbalimbali kushirikiana na Taasisi nyingine kama vile madhehebu ya dini, wanasiasa na Wizara ya Elimu na kuwashawishi wananchi kuachana na mapigano.

Nne, vyombo vya ulinzi na usalama vinaendelea kudhibiti hali ya kuzagaa kwa silaha ndogo ndogo za kiraia na kivita.

Tano, vikundi vya ulinzi wa jadi yaani Litongo vimeanzishwa kwa lengo la kuwafuatilia wezi wa mifugo.

Sita, mkutano wa ujiramwema baina ya vyombo vya dola vya Tanzania na Kenya vimeendelea kufanyika ili kuimarisha mahusiano miongoni mwao, na mnamo tarehe 21 Aprili, 2009 ujumbe wa Jeshi la Polisi ukiongozwa na ndugu Robert Marumba Mkurugenzi wa Upelelezi ulikwenda nchini Kenya kuongea na viongozi wa Jeshi la Polisi Kenya kuhusu namna ya kusaidia na kuzuia mapigano ya koo, kilimo cha bangi, wizi wa mifugo na wizi wa magari.

Saba, Mabaraza ya Ardhi ya Kata yameendelea kuboreshwa ili yaweze kuamua kesi za migogoro ya ardhi ipasavyo.

Nane, Kamati za Ulinzi na Usalama za Kata za Vijiji ambazo zilikuwa hazifanyi kazi zimeanza kufanya kazi inavyopaswa.

Tisa, Serikali kupitia kitengo cha Maafa imekuwa ikitoa misaada ya kibinadamu kuwasaidia walioathirika kutokana na mapigano ya koo.

Kumi, baadhi ya koo zilizokuwa na uhamasa zimerejesha mahusiano mema baina yao.

Kumi na moja, wananchi wameanza kutumia mazungumzo kama njia ya kutatua matatizo badala ya vita.

Kumi na mbili mashamba ya bangi yameendelea kuharibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nimetembelea Mkoa wa Mara zaidi ya moja kujionea hali halisi ilivyo. Mara ya mwisho nilitembelea Wilaya ya Tarime tarehe 27 Machi, 2009 na kuzungumza na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mkoa na Wilaya ya Tarime. Mbunge wa Jimbo la Tarime, Viongozi watendaji wa Tarafa, Kata na Vijiji na wazee wa kimila. Niliwasihi washirikiane na Serikali katika kukomesha mapigano hayo.

Aidha, Jeshi la Polisi limeanza Operesheni Komesha Uhalifu Mkoani Mara kuanzia tarehe 25 mwaka 2009 kwa kuongeza askari na vitendea kazi chini ya operesheni hiyo Askari zaidi wataongezwe mwishoni mwa mwezi huu wa Aprili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mikakati ya muda mfupi na muda wa kati Serikali pia inaendelea kufanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya NUU ambayo ni pamoja na:-

Moja, kuviongezea uwezo vyombo vya ulinzi na usalama katika bajeti zao ili viweze kuwa na vitendea kazi vya kutosha katika Wilaya hizo.

Pili, kutengeneza barabara za mpakani ili maeneo yaweze kufikika kwa urahisi na kuviwezesha vyombo vya dola kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Tatu, kuviimarisha vituo vya mpakani vya Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kudhibiti magendo kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini ya Serikali kuwa hatua hizi zitasaidia kurejesha hali ya utulivu na amani Mkoani Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mhesimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kauli hiyo iliyotolewa.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea kwa ajili ya kujiandaa vizuri ni wataarifu kwamba tutakapofikia hapo mbele kidogo tutamalizia wachangiaji wa hoja ya jana kuhusiana na Maazimio ya Bunge Kuhusu Haki za Watu wenye Ulemavu na wachangiaji wetu ili wajiandaa vizuri watakuwa ni wanne kama alivyoeleza Mheshimiwa Spika, jana jioni. Tutaanza na Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo atakuwa mchangiaji wa mwisho. Katibu kwa hatua inayofuata.

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Raslimali za Maji wa Mwaka 2009 *(The Water Resources Management Bill, 2009)***

**Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2009 *(The Water Supply and Sanitation Bill, 2009)***

*(Miswada Miwili ya Sheria ya Sherikali iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni*

*kwa Mwaka wa Kwanza)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu kwamba Miswada hii Miwili ya Sheria moja ikiwa Usimamizi wa Rasilimali za Maji na mwingine wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira yote ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, alikwishalieleza Bunge kwamba imeletwa kwa Hati ya Dharura kutoka kwa Mheshimiwa Rais. Kwa maana hiyo wiki ijayo tutajadili Miswada hii inayohusu Maji wakati wowote kati ya Jumatatu hadi Jumatano kutegemeana na Kamati ya Uongozi itakavyopanga ratiba. Kwa hiyo, nawaeleza haya ili muweze kujiandaa kwamba kuna Miswada hii inayohusua maji. Miswada miwili itakayokuja wiki ijayo. Katibu kwa hatua inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

### Azimio la Bunge la Kuridhia Mkatable wa Nyongeza wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu
### *(The Optional Protocol to Covnetion on the Right of the Persons with Disabilities)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Namwomba Mheshimiwa Riziki Lulida awe mchangiaji wetu wa kwanza kuhusiana na Azimio la Bunge kuhusu Haki za Watu Wenye Walemavu. Mheshimiwa Lulida.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia kupata nguvu za kuweza kuwepo sasa hivi na kuweza kuchangia hoja hii iliyoko mbele yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nimefurahishwa sana napenda kumpongeza Waziri wa Afya na Usatawi wa Jamii Mheshimiwa David Mwakyusa. Pia napenda kumpongeza Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, tatu napenda kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya ndugu Blandina Nyoni kwa kazi nzuri aliyoifanya na kuhakikisha kutuletea hoja ambayo imekokotoa na kuleta ufanisi mkubwa na kuleta faraja kubwa maana kila kilichoandikwa humu ndani kweli kinaonekana kimefanyiwa kazi vizuri na kuhakikisha walemavu kama kweli utekelezaji utapatikana basi faraja kubwa itapatikana kwa walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vile vile kutoa pongezi kwa vyama na shirikisho mbalimbali vya walemavu hasa nikimpongeza Ndugu Mandesi na pili napenda kutoa rambirambi zangu kwa Khalifan K. Khalifan ambaye tulikuwa naye katika kuhakikisha maandalizi ya mwisho yanafanyika kule *New York* lakini sasa hivi Mwenyezi Mungu amemchukua amekwenda katika mbele za haki Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema ndugu Khalfan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli pamoja na sifa zote tulipokwenda New York tulipewa sifa ya kwanza Tanzania ambayo tulipongezwa na nchi mbalimbali kuonyesha kuwa nchi ya Tanzania imeweza angalau kutoa Wabunge walemavu kuwa wawakilishi ndani ya Bunge hili pamoja na kuwa hawajatosha lakini angalau tumeonyesha mwongozo na mwelekeo kuwa tunawajali walemavu.

Nchi nyingi ambazo waliona maajabu haya walituuliza kwanza Nigeria tuelekezeni ilikuwakuwaje mpaka ninyi mkapata nafasi za uwakilishi wa walemavu katika Bunge, Afrika hii ni mojawapo ni Tanzania peke yake ambayo imeonyesha mwelekeo mkubwa wa kuhakikisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano walemavu wapo. Kwa kweli lazima tushukuru na tumpongeze Mheshimiwa Rais na Chama cha Mapinduzi kwa kuliona hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi tulizopewa lakini napenda kuonyesha dosari moja ambayo sasa hivi inabidi ifanyiwe kazi na lilikerebishwe. Hoja ya ukatili na vitendo vya waovu wanavyofanyiwa walemavu. Kwa kweli imetutia dosari kubwa sana Tanzania kuona tunakuwaje nchi yenye amani, nchi yenye utulivu, nchi yenye demokrasia baadhi ya watu wanatuchafulia kuonyesha vitendo viovu dhidi ya walemavu. Sasa hivi tunashuhudia walemave wakiteswa majumbani, walemavu wakinyanyaswa, walemavu wakichinjwa kwa imani za kishirikina. Ninaona viongozi, Wabunge, watu wa dini Mashehe, Maaskofu, Mapadri hii iwe changamoto kubwa kuhakikisha hili zoezi la kuhakikisha utovu au uove wanaofanyiwa walemavu katika kutendewa mambo ya ukatili inatokomea kabisa tusilisikie kabisa likiendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima nimpongeze Mbunge mwenzangu mama Mkanga jana ametoa hoja nzito maana yake mpaka mimi hapa nimefilisika cha kuongea sina. Amejitahidi mama Mkanga kutoa hoja zake kwa ukamilifu na kwa uangalifu sana lazima nimpongeze Mheshimiwa Mkanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuzungumzia Ibara ya 10 haki za wanawake na watoto. Sasa hivi walemavu tunawaona wengi wa walemavu wana watoto ndani ya nyumba zao. Lakini wanaume wengi wanaozaa na walemavu hawaoni kama wana haki ya kujitambulisha kwamba mimi nimezaa na mlemavu anaona ni haki ya kumzalisha lakini anamwambia mlemavu kuwa wewe nimezaa na wewe lakini ukinitambulisha nitakuua. Hii hali inasikitisha sana. Hii hali ya kujikuta unazaa na mlemavu halafu unamtekeleza si nzuri hata kidogo. Lakini nashukuru sasa hivi Wizara ya Afya ifanye kile njia kuhakikisha *DNA* zinapatikana katika kila Mikoa wale watakaothibitika kuwa wanawakataa wale watoto wapimwe na adhabu za kisheria zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala ambalo ni kero kubwa ambalo linawakuta walemavu mojawapo ni ajira. Kuna walemavu wamesoma wana elimu nzuri wana *masters*, zinapotokea ajira walemavu wanaomba ajira. Kwa vile hawajamuona anakuwa *short listed* na akajiona jina lake limechaguliwa. Lakini pale tu anapofika kwa mwajiriwa kuona na kumhisi yule mlemavu basi anaanza kumchukua pale

pale kuwa huyu sasa ni tatizo ndani ya *society* yangu. Hivyo atachukiwa yule mtu hataajiriwa tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa ushauri mmoja endapo mlemavu atakuwa *short listed* na akaonekana amefika pale kwenye kusajiliwa basi wapewe nafasi ya upendeleo aingia *direct* katika kuajiriwa ili na yeye aweze kujikwamua katika ajira na inawezekana vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuko katika mchakato wa bajeti. Mchakato huu wa bajeti ni kipindi muafaka sasa hivi kuhakikisha bajeti hii inaongezwa rasmi katika kundi maalum la walemavu wapate fungu la kutosha angalau liweze kuanza kuwasaidia na liweze kuwasaidia kwa kuanza kuwapelekea katika sehemu mbalimbali katika idara za ustawi wa jamii Mikoani ili angalau na wao wapate huduma.

Muda wote upande wa ustawi wa jamii aidha hata huyu Afisa Ustawi wa Jamii hayupo au fungu la fedha halipo hivyo linawapa tabu mno sana tujiulize tulipokaa hivi sasa hapa tuna furaha zetu, tuna maisha mazuri, lakini wenzetu walemavu wako katika mazingira magumu sana. Tusijione kama tumekaa hapa kama watu wazima mungu siku moja angeamua humu ndani tu tukaenda majumbani tukarudi asubuhi hatuna meno wote vibogoyo basi tungekuwa na dhiki kubwa sana. Kila mmoja wetu angekimbia hapa kwenda kutafuta meno kuja kubandika kwa sababu hii hali haiwezekani.

Kwa mtazamo huu tuwaone na wenzetu vile vile wana dhiki kubwa sana wanahitaji kufarijiwa na sisi wananchi, sisi viongozi na tusiwaone watu kama hawa hawastahili. Nao wanastahili kama watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningefurahi zaidi kama tungepata na sisi vile vile msaada kwa walemavu kuhakikisha vifaa vyao wanavyoviagizia kutoka nje iwe miwani, fimbo, baiskeli hata magari yao ya Bajaji visitozwe ushuru kabisa hii itawasaidia walemavu angalau kujikwamua katika kutembea katika usafiri na vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyozungumza kwa muda mrefu kuwa mengi yamezungumzwa lakini nitazungumza suala la miundombinu. Miundombinu kwa walemavu imekuwa ni tatizo kubwa sana. Leo hii majengo yanajengwa Dar es Salaam mpaka ghorofa ya saba lakini hakuna *lift*. Je, mlemavu anakuwa na shida kule juu kwenda kutafuta huduma hivi bila kuwa na *lift* na mazingira kama hayo atakwendaje?

Barabara zetu hazikutengenezwa kwa ajili ya kuwasaidia walemavu. Kila kilichoandaliwa kiliandaliwa kwa watu wa kawaida. Ni wakati muafaka sasa hivi kuhakikisha Serikali inaliangalia tena kwa kutekeleza maana unapokuta leo tunataka kuridhia azimio la Bunge na mwisho wake Muswada wa sheria utaletwa, je, utekelezwaji utatekelezwa? Hili ndiyo la msingi. Tuhakikishe utekelezaji unatekelezwa ili walemavu wajikute na wao wasaidiwa na wanawekewa mazingira ambayo baadaye haitawasumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuja upande wa afya. Leo hii kuna wachache kama asilimia 2 watakuwa walemavu wanajiweza. Lakini asilimia iliyobakia 98 walemavu

hawajiwezi. Ningeomba Bunge lako tukufu lilione hili na lilijadili hili wapewe huduma bure ya matibabu. Huduma bure hii ya matibabu itawaondolea kero na adha ya kununua madawa. Wao wawe *special* au kundi maalum ambalo linakaa pale wakienda hospitali wapate huduma ya hali ya juu na kuweza kuhakikisha kuwa hawa watu hawahitaji tena kusumbuka sumbuka. Lakini ukienda mahali tayari ameshakuja mlemavu. Tatizo hawajawaona hawa watu kama wanahitaji msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuwa na mengi ya kuongea ila ningeomba kauli mbiu kuwa utekelezaji upewe kipaumbele. Mwisho kabisa kuhakikisha Muswada huu unakuja upesi ili lipitishe hawa watu wenye Ulemavu wapate kusaidiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki Lulida kwa mchango wako. Kabla sijamwita Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge, kupitia kwenye *pigeonhole* zenu kati ya leo Ijumaa na kesho Jumamosi kwa ajili ya kupata rasimu za ile Miswada ya Maji kwa ajili ya maandalizi ya mjadala wa wiki ijayo.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuleta hoja hii tuweze kuiridhia. Lakini vile vile niwashukuru watendaji kwa kazi kubwa waliyofanya ili kuonyesha tunawajali ndugu zetu walemavu kutokana na hali zao zilivyo na wao hawakujitakia lakini ni mambo ya Mwenyezi Mungu mwenyewe alivyopenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingi zimekwishajadiliwa zimeungwa mkono mimi nitakuwa na machache tu ya kusisitiza kwa Serikali ili kuweza kuboresha hali ya walemavu kwa ujumla. Kwanza niunge mkono hoja hii iliyo mbele yetu na kubwa ninaloliona mimi ni kwamba walemavu wanahitaji kuwezeshwa. Ni watu wenye akili timamu wao ni binadamu, wenye kasoro tu kidogo ambazo zinawakosesha uwezo wa kufanya mambo mengine ambayo binadamu mwingine wa kawaida anaweza kufanya. Sasa ili waweze kutimiza malengo hayo ya kuwezeshwa zaidi ni vifaa.

Vifaa hivi sasa hivi vimeboreshwa kutokana na teknolojia inavyoendelea duniani. Teknolojia hii imerahisisha kutengezwa vifaa ili na wao walemavu waone wepesi wa kufanya shughuli zao. Lakini tatizo linalojitokeza ni kwamba inajulikana wazi kwamba vifaa hivi vina gharama kubwa sana. Leo ukitaka mkono wa bandia uko wa aina tofauti. Kuna mkono wa bandia kuonyesha tu kwamba kuna mkono lakini mkono ule pengine usiweze kufanyakazi ukaweza ukamsaidia katika shughuli zake. Lakini sasa hivi teknolojia imekwishaendelea mkono wa bandia unafanyakazi kama mkono mwingine kwa asilimia 80. Sasa hivi ni vifaa ambavyo wananchi wetu wanavihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini gharama zake ni kubwa sana na siyo kwamba watashindwa kutumia kwa sababu wao wanaelewa na wana akili timamu na wasome na wakieleweshwa wanaelewa haraka sana. Sasa niishauri Serikali, Serikali ina taratibu ya misamaha ya kodi. Tukipitia hesabu za Serikali, misamaha ya kodi inayotolewa ni mikubwa sana. Mwaka 2006/2007 misamaha ya kodi imefikia asilimia 30 ya bajeti ya mwaka ule.

Lakini ukija ukitazama ni misamaha gani iliyotolewa ambayo imeweza kuleta manufaa kwa wananchi lakini utakuta misamaha mingine imetolewa kwa kuwanufaisha watu kwa sababu ambazo siyo za muhimu sana lakini tu kwa sababu sheria imeona kwamba wapewe msamaha. Lakini tunasahau kwamba kuna walemavu ambao wanastahili kabisa kwamba wapewe msamaha katika vifaa ambavyo vitawezesha wao kufanya shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba vifaa hivi vipitie Serikali kwa utaratibu aidha iwe ni *MSD* ili waweze kudhibiti bila kuachiwa wafanyabiashara wengine kuagiza vifaa halafu kupandisha bei wakiweka gharama ambazo siyo halisi. Lakini Serikali yenyewe inajua kwamba vifaa hivyo tulivyovinunua bei yake ni hii angalau basi yule mlemavu aidha anunue mwenyewe au asaidiwe yule atakayemsaidia ionekane kwamba hivi vifaa anamudu viweze kumsaidia binadamu mwenzake. Magongo yale ni ghali, baskeli zao ni ghali, mikono ya bandia, miguu ya bandia ni ghali. Sasa hivi vitu vyote vinawasaidia wao kurahisisha maisha yao. Kama Serikali itatoa misamaha hii itakuwa ni misamaha *genuine* kabisa kwamba matumizi yake ni halali kwa binadamu ambaye kwamba ni Mtanzania tunahitaji kumsaidia. *(Makofi)*

Lakini isitoshe walemavu wengi walioko vijijini kwa matumizi yao ya faragha kama kwenda *toilet* kuna vifaa vingine maalum mahsusi kwa ajili yao hivi ndio havinunuliki kabisa. Lakini haina maana kwamba yuko kijijini hastahili kuwa na choo ambacho kitakuwa na *flash* ili kumrahisishia yeye hii sio sahihi na wala sio haki vitu kama hivi vinatakiwa vifike mpaka vijijini hatimaye aone kwamba kuishi kusiwe ni adhabu kwake. Lakini ameishi duniani kwa sababu Mwenyezi Mungu amemleta duniani, lakini basi na yeye atazamwe na nani atakayemtazama kwamba kumrahisishia maisha yake kule vijijini yanakuwa ni rahisi na wepesi kwa sababu katika maisha ya binadamu suala la binadamu kwenda chooni ni lazima na usipokwenda utaumwa utakuwa na maradhi. *Yes!* kwenda chooni ni *necessity* ni lazima uende ili afya yako iendelee kuwa nzuri.

Lakini vifaa vya walemavu kwa ajili ya kwenda chooni tunaviangaliaje? Tunaviona labda si vitu muhimu lakini ni muhimu sana kwa maisha ya binadamu na wao wasitazamwe kwa hali hiyo kule kule watengenezewe vyoo vya aina hiyo ili waweze kuendelea na maisha bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika elimu wale ambao wasioona wengi wanapoteza kupata taaluma kwa sababu ya vifaa vya kusomea, lakini teknolojia imerahisisha hiyo na wapo wanaosoma kwa utaratibu huo, lakini ni mijini. Tunafanya utaratibu gani wa kuondoa kodi ya vifaa kama hivyo tuwapelekee mashule na kuwe na madarasa maalum na walimu maalum kwa ajili ya kuwasaidia, tukiwaacha hivi hivi watakuwa ni binadamu ambao hawakusoma, ni ujinga unakuwa ni mzigo kwa familia, unakuwa ni mzigo kwa Serikali yenyewe na yeye kama binadamu anastahili asome lakini kwa kutokuwa na macho ya kuona au kwa kutokuwa na masikio ya kusikia haina maana kwamba yeye

asitengenezewe utaratibu mzuri ili apate haki sawa kama Katiba ya Jamhuri ya Muungano inavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa masuala ya afya yameongelewa na mambo mengine mengi yameongelewa. Nilitaka kusisitiza katika hilo na kuweka mkazo Serikali sasa hivi iweke utaratibu na kutenga bajeti maalum kwa ajili ya misamaha ya kodi kwa ajili ya vifaa vya walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Rished Abdallah nichukue fursa hii pia kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba wale ambao wangependa kuchangia Muswada wa Bima ambao utafuata baadae waendelee kuleta maombi yao kwa Katibu wa Bunge hapa mezani.

Sasa namwita Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niongeze sauti yangu katika mkataba huu. Naomba kusema kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, tumeujadili Muswada huu kwa kina lakini hata hivyo ningeomba sana nitoe machache kuhusiana na Mkataba huu. Awali ya yote nilitaka sana kuipongeza Serikali kwa kuleta Mkataba huu mapema lakini nilitaka nitoe historia ya Tanzania *actually* tangu wakati ingali Tanganyika jinsi iliyotimiza wajibu wake katika kuangalia kwamba maisha ya watu wenye ulemavu yanaboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nionyeshe tu kwamba elimu, ajira na nafasi za uongozi kwa watu wenye ulemavu katika nchi yetu imetolewa tangu miaka ya 1960. Kwa mfano Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ndie yeye wa kwanza alifungua njia kwa kumpa Uwaziri mtu mwenye ulemavu kwa jina la Dereck Bryson alikuwa Waziri katika *cabinet* ya kwanza na Waziri huyu alifanya kazi kwa uadilifu mkubwa alikuwa kimbilio la hekima na alikuwa Mbunge wa Kinondoni tangu mwaka 1961 hakuna aliyechukua kiti chake mpaka Mwenyezi Mungu alivyomwita 1980 akiwa bado Mbunge na Waziri bora. Kwa hiyo ninasema hivi miaka ya 1960 mtu mwenye ulemavu alikuwa Mbunge na alikuwa Waziri. Naomba Serikali ichukue historia hii na kumchagua Mbunge mlemavu awe Waziri katika Serikali sasa kwa sababu kuna *presidency*, hiyo ndio silka ya nchi yetu tangu tupate uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande mwingine ninaomba nizungumze na watu wenye ulemavu kuwaambia tu hamko peke yenu kwamba na sisi *any time* tutakuwa walemavu na mimi naomba nitangaze hapa kwamba bila ya Serikali yetu na Bunge hili kunigharamia kwenda kutibiwa miguu na mimi vile vile ningekuwa na nyie, naomba tuipongeze Serikali yetu jamani, wapigieni makofi. Hawa watu wenye ulemavu kuna historia ni watu wenye uwezo mkubwa, wenye kipaji kikubwa, vipaji vya aina mbalimbali tazameni historia ya mtawala mmoja wa Kimarekani *President* Abraham Lincon alikuwa mtu mwenye ulemavu lakini alitawala kwa uwezo mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Dereck Bryson ambaye alikuwa Waziri wa Serikali ya Tanzania tangu mwaka 1961 mpaka 1980 alipokufa alikuwa na uwezo mkubwa sana. Sasa hivi hapa ndani watazameni Wabunge wetu na michango yao. Jana tumemsikia Mheshimiwa Margareth Mkanga uwezo mkubwa tu na nampongeza kwa hotuba yake ya jana, sijui Mheshimiwa Rais atamchagua kuwa Waziri, ingekuwa jambo zuri. Tumemsikia Mheshimiwa Zulekha, tumemsikia Mheshimiwa Bujiku Sakila, tumemsikia leo hii Mheshimiwa Riziki Lulida hawa ni watu wanaonyesha vipaji vya hali ya juu katika nyanja za siasa. Katika nyanja za sanaa wale wapenda muziki mnamkumbuka kabisa bwana mmoja anaitwa Steven Wander na nyimbo zake zile. Kwa hiyo inawezekana kabisa wale watu wenye ulemavu wakafanya mambo makubwa, makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu tunaupitisha leo kutilia mkazo mambo ambayo Watanzania tayari wanafanya. Ninalotaka kuomba sasa ni kwamba ndugu zangu watu wanaoishi na ulemavu wazidi kujitahidi sana waweze kujikwamua katika nyanja zote za maendeleo ya wananchi. Vile vile kwa wafanyabiashara na ndugu zangu Tanzania ninaomba nimtaje na kumpongeza ndugu yetu Bwana Reginald Mengi yeye amejiwekea utaratibu mkubwa sana wa kula *lunch* mara moja kwa mwaka na walemavu katika mji wa Dar es Salaam. Tunaomba wafanyabiashara wenye uwezo wamuige ndugu Mengi wawasaidie kuwakomboa na kuwaweka karibu watu wenye ulemavu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu naiomba Serikali izidishe utoaji wa elimu kwa jamii ya watu wenye ulemavu tuna maana kwamba waongeze shule nyingi za walemavu zenye zana nyingi zote, zana hasa ma-*brella* yale na vitu hivi vya kuongeza uwezo wa kusikia *hearing aids* na mambo mengine na wafundishe walimu wengi wa shule hizi. Tunaomba vile vile elimu iongezwe kwa wakunga wa jadi. Katika historia ya mwendo wa magonjwa ulemavu unatokea katika vizazi kati ya asilimia saba na kumi.

Lakini yako makabila na wakunga wa makabila hayo wanawamaliza hawa pale pale wanapozaliwa. Kwa mfano tungekuwa tunataka maelezo kwa nini makabila mengine hatuwaoni vilema hata mmoja, makabila ya watu warefu tu wanatembea tu saa zote, haiwezekani lazima wakunga hawa wanawaminya hawa wakati wanazaliwa. Kwani naomba Serikali iongeze elimu kwa wakunga wa jadi wasiwaminyeminye hawa watu mwisho wakakosa hata kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuongeza sauti yangu katika nguvu na shughuli kwamba Serikali ifanye kuzuia ukatili kwa wenzetu wenye ulemavu wa ngozi. Vile vile ninaomba sana tutazame upande wa umaskini na hali ya kipato cha watu wenye ulemavu. Serikali ijitoe muhanga katika hili iweze kufanya mipango madhubuti ili itoe mitaji kwa masharti nafuu kwa walemavu wenye uwezo wa kufanya shughuli za kibiashara au shughuli zozote zile na tunaomba vile vile wapate mafunzo ya ujasiriamali tuweze kuwabadillisha watu wenye ulemavu ili waingie katika mfumo wa uchumi mkubwa wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante sana na naunga hoja hii mkono. *(Makofi)*

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa na mimi fursa ya kuchangia. Awali ya yote nianze kumpongeza Waziri wa Wizara ya Afya, Naibu Waziri Wizara ya Afya, Ofisi yao yote, Serikali kwa ujumla kwa kuweza kuleta Azimio hili la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye ulemavu. Lakini pia nichukue fursa hii kuwapongeza Wabunge na wadau wote waliohusika hadi kufanikisha Maazimio haya kuletwa hapa na tuweze na sisi kuyaridhia. Kwa kweli umuhimu umezungumzwa sana na unajulikana. Mimi binafsi nimeona kwa kweli ni afadhali Maazimio mengine au masuala mengine yoyote hayana umuhimu kuchangia kama hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Wabunge na Watanzania wote wanaosikiliza tumshukuru Mungu kama wewe umeamka uko salama kwa kila hali umshukuru Mungu ni kwa neema tu. Sio kwamba wewe ni bora zaidi, sio kwamba wewe ni mwema zaidi ni kwamba ni neema ya Mungu tu umekuwa ulivyo. Nadhani nikisema hivyo wale ambao wanaelewa wataelewa kwamba kwa kweli suala hili si la kufanyia mzaha.

Katika kuangalia Mkataba ambao tumepewa nakala ukurasa ule wa 25 katika ile *article* 34 kipengele cha 4 pale *infact* ni kipengele chote cha 34 Mkataba unazungumzia kutakuwa na Kamati Maalum, nadhani tayari ipo na kwa sasa hivi nadhani wako 12 kama nimeulewa vizuri lakini jinsi nchi zitakavyoongezeka hadi kufikia 60 na kadhalika watakuwa 18.

Nimesema hayo kwa sababu kwa kweli ukiangalia ni vyema kabisa Tanzania tukawemo katika wale 18. Nasema hivyo kwa maana jinsi ambavyo unaingia karibu zaidi na mamlaka ambayo inayohusika hasa Kimataifa tutaweza kupata manufaa zaidi. Mimi naomba tujitahidi sana, ndugu zetu wahusika kama wataona kwamba kunahitajika hata *lobbing* au kupita kwa njia nyingine kutoa msukumo lakini angalau wakati unapofika na taratibu zilipoandaliwa basi na sisi tuweze kuwemo humo.

Tukubaliane kwamba sheria ije mapema ili tuweze kuwa na vigezo vyote ambavyo vitaturuhusu kuingia ili na sisi tuwe kule mwanzo kabisa katika suala hili. Lakini pale pale katika hicho kipengele ukiangalia ukurasa wa sita wamezungumzia kifungu cha 4 pale kipengele cha 3 kinazungumzia nchi wanachama wahusishe watu na watoto wenye ulemavu katika ngazi zote kuanzia uundaji na utekelezaji wa sheria na sera zinazohusika, hapa napenda nizungumzie kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana taratibu zinavyoendelea tuwafikirie sana wale watu ambao wako mpaka ngazi ya chini *grassroot*, vijijini huku kuna vizingiti vingi vya mila, vya desturi na mambo mengine mengi. Kwa kweli najua jitihada nyingi sana zimefanyika kupitia vyombo mbalimbali ambavyo vinahusika na walemavu, lakini bado naomba nisisite kwamba kule vijijini hali ni tofauti.

Kilindi pale nikisema napenda mara nyingi kuongelea Kilindi kwa sababu ndio naielewa vizuri bado kuna kazi ambayo inatakiwa ifanyike. Wananchi wenye ulemavu, wanafunzi, miundombinu wenzangu wameshaizungumzia lakini unakuta kwa kweli ni tatizo pale mtoto anapokwenda choo cha ujumla shuleni kwa sababu hakuna vyoo vilivyotengwa kwa ajili ya walemavu.

Majumbani ukipita namfahamu kuna mama mmoja hadi amefariki juzijuzi alikuwa ni mlemavu anaishi mwenyewe alikuwa na mtoto mmoja naye alifariki lakini mazingira aliyokuwa anaishi yule mama alikuwa anatambaa bahati nzuri Mbunge wake ambaye ndio mimi nazungumza niliweza kumsaidia saidia. Lakini wako wangapi kama wale, je tunaweza tukawafikia wote. Kwa kweli ninaomba sana jinsi mnavyoendelea kujipanga mkumbuke msibaki huku mijini au wale wanaoonekana kuna maeneo ambayo yako ndani sana ambayo kwa kweli yanahitaji kutambulika.

Lakini vile vile nilipenda niongelee hawa walemavu walioko mijini kwa mfano wale ambao mara nyingi mnatembelea Dar es Salaam kuna mmoja yule ana mikono midogo miwili inaning'inia juu mtu kama yule hana cha kufanya hata ukisema afanye nini. Hao walemavu wa mjini pale tunaona wanazunguka wengine wanashindwa hata kuja mijini hao wanafikiriwa na nani, kweli wanatazamwa na kama wangetazamwa wangekuwa na hali zile walizonazo. Mimi nilikuwa naomba sana jinsi ambavyo tunaendelea ninaomba kwa sababu suala hili tumeliwekea kipaumbele basi na wale nao sasa tuanze kuacha kuwaona barabarani, tuanze kuona wanapatiwa huduma mbalimbali ili tuone kweli kazi inafanyika.

Lakini vile vile kuna aina nyingine mtu amesaidiwa ana baiskeli ni mlemavu labda wa viungo vya miguu lakini unakuta anaacha baiskeli kando au tayari ameshasaidiwa ana viungo ana mguu wa bandia, mkono wa bandia anaung'oa anauweka kando hapo hapo ya barabara anaanza kuomba na anapita akiombaomba. Kwa kweli jamani naomba sana matatizo yapo lakini jinsi ambavyo tumepanga sasa tufanye kazi hii basi iende kwa wote kusiwe na makundi maalum ambayo yanaonekana kusaidiwa zaidi kuliko wengine. Lakini kupitia fursa hii ninaomba sana sheria itakapotungwa ndugu zetu wenye ulemavu tusaidiane na sisi ambao Mungu ametusaidia kidogo tuko wazima mpaka sasa tusaidiane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mashirika au Asasi za Serikali ambazo zinatumia majina ya walemavu kujipatia fedha, lakini ukiangalia hazikidhi na wala hazifanyi shughuli zile. Unakuta kwa mfano Wilaya kama ya Kilindi hakuna hata Shirika moja ambalo linashughulika na walemavu lakini ukija ukiangalia kwenye Mashirika mengine au Balozi zingine unakuta Kilindi wanahudumiwa na kadhalika huu nautoa tu ni mfano. Sasa nadhani wako wengi kama hawa ambao wanatumia. Juzi mtu mmoja ananipigia simu anasema bwana wewe Mheshimiwa Shellukindo ulaji tuanzishe Shirika la kwetu kwa ajili ya walemavu wenye ngozi kuna hela mahali fulani nimetoka wameniambia. Jamani naomba narejea tena ni kwa neema tuko tulivyo ninaomba sana sheria iangalie kwa makini suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye hoja yangu ya mwisho naomba niseme kwa dhati kwa sababu maeneo ya upande huu kidogo nina uelewa nayo. Dhamana hii imekabidhiwa Wizara ya Afya kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii. Jamani tukubaliane Ustawi wa Jamii ni wapi Mwenyekiti utaniwia radhi kwanza sijui kama hata wananchi wengi wanaelewa hasa majukumu ya Idara ya Ustawi wa Jamii, wanajua kuna chuo lakini Idara ya Ustawi wa Jamii inafanya nini mara imechanganywa na Maendeleo ya Jamii, mara hivi kwa kweli mimi najiuliza sana *dynamism* hakuna wala huoni ule utendaji kazi wa Idara ya Ustawi wa Jamii kama Idara.

Sasa jukumu hili ni zito jamani na ni kubwa na kama kweli tunataka *seriousness* mambo yaende nadhani tuangalie tena ni sehemu sahihi ambapo tumeweka suala hili. Maafisa Ustawi wa Jamii wenyewe Mawilayani, Mikoani wapo, wanafanya nini? Kwa kweli naona tusiweke kitu tu mradi tumekiweka kitu kwa sababu kinafanana halafu pasiwepo. Nawafahamu watu wengi sana wanamaliza Chuo cha Ustawi wa Jamii hata kupata kazi wanaishia kuwa ma-*sociology* sijui wanakwenda wapi?

Lakini sasa tunasema tunakabidhi suala hili kwenye Ustawi wa Jamii, jamani tusije tukawa tunapitisha vitu vizito vyenye umuhimu katika maeneo ambapo kwa kweli utekelezaji wake utakuwa ni mgumu. Naomba liangaliwe tena Ustawi wa Jamii kwanza inaweza ikabaki pale lakini basi Serikali iangalie itoe changamoto iweze kuona utendaji ule unakwendaje? Bajeti yake ikoje, wale watu utaratibu wao wa kazi ni upi na majukumu yao ya kazi ni yapi na yanafanyika. Lakini jambo ni msingi sana kuangalia upya walemavu kwenda Ustawi wa Jamii mimi bado nina alama ya ulizo *question mark*, tuangalie kama tunafanya kitu sahihi, lakini sikatai lakini nasema changamoto kwanza paboreshwe ndio tuweze kwenda pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kusema kwamba fedha zitengwe kwenye Idara ya Afya upande wa Ustawi wa Jamii, kwa ajili ya walemavu mimi nakubaliana. Lakini ili kazi iende kwa pamoja huku ambapo kwa sababu tunajua bajeti za Wizara zinavyokuwa na *ceiling* halafu baadae zinakuwa zinapunguzwa na kadhalika na yakija mambo mazito najua vipengele ambavyo huwa vinapunguzwa mara nyingi ni vile ambavyo vinaonekana haviendi haraka. Kwa hiyo, najua pale patapunguzwa lakini niseme pia tusisitize basi kwenye Halmashauri zetu tuwe na fedha zimetengwa kwa ajili ya masuala hayo hayo. Wataalamu wanaohusika pia wawepo kwenye Halmashauri ili tuweze kwenda pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya ya kwangu ni hayo machache nilitaka kutoa angalizo hilo na hayo mengine lakini narudia tena kuwapongeza Wizara kwa kuleta suala hilo naunga mkono hoja.

Lakini pia niwaambie ndugu zetu walemavu kwa kweli kabisa tuko pamoja nao kwa kila hali wasione kama wameachwa lakini walemavu wasiwe na makundi, kundi ambalo ni la aina hii na la kati na la chini hapana wote twende pamoja mlemavu ni mlemavu na anahitaji huduma sawa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Wataalamu wote wa Wizara hii, kwa kuweza kuleta mkataba huu ndani ya Bunge letu kwa ajili ya kuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zetu wenye ulemavu walikuwa wanaulizia sana mkataba huu ambao una mambo mengi yanayotetea haki zao za msingi. Ndugu zetu hawa wamekuwa wakipata manyanyaso mengi kutokana na hali zao. Yapo mambo mengi kama suala la Elimu, ndugu zetu wamekuwa hawapati Walimu wa kutosha hata vifaa vya kufundishia na hii inachangia kukosa elimu bora na hata kukosa ufahamu wa mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na Walimu na vifaa, majengo ya shule hizo na vyoo siyo rafiki kwa ndugu zetu na inawawia vigumu kutumia sehemu hizo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengi ambayo naamini Bunge lako Tukufu likisharidhia mkabata huu, utakuwa mwanzo mzuri wa kutekeleza na kurekebisha mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ningeomba niungane na Wabunge wenzangu, kuomba sasa Sheria ya watu wenye ulemavu itungwe na kuletwa Bungeni ili tuweze kuiptisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niungane na Kamati kwa ushauri walioutoa wa kuanzisha hatua na mikakati ya usalama wa kijamii kwa watu wenye ulemavu na wale wanaoshughulikia matatizo ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii na naunga mkono Azimio la Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watoto Wenye Ulemavu.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio hilo na kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote. Pia naipongeza Kamati husika na wadau wote.

Mchango wangu upo katika majengo (Miundombinu). Serikali ianze kufanyia kazi hasa barabara na majengo ya ghorofa, wakandarasi wafuate mahitaji ya walemavu kwani wanapata shida sana. Sheria itamke wazi kuwa, endapo jengo halikidhi mahitaji ya walemavu, basi hatua zichukuliwe za kisheria pamoja na kuzuia kutumia jengo hilo. Tatizo la walemavu wa ngozi (*Albino*), Sheria iwe na mkazo mkubwa zaidi ili kunurusu maisha yao hasa wale wahusika wa biashara hii; mfano, wanganga wa jadi, wafanyabiashara wa madini na wale wanaoishi na walemavu (walezi na wazazi).

Mwisho, nalitakia Bunge liridhie haraka na kisha Mheshimiwa Rais aweze kusaini mapema.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio la Mkataba huu. Katika kipengele cha elimu, naiomba Wizara kwa kuzingatia Azimio hili, isaidie Halmashauri ambazo zina mikakati ya kuwapatia shule maalumu walemavu pindi wanapojitokeza. Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, imeboresha majengo ya shule ambayo ilikuwa *Middle School* na kuifanya shule maalumu kwa ajili ya walemavu wenye matatizo ya kutosikia na kutoona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara iisaidie Halmashauri hii, jinsi ya kuweza kuwapatia vifaa vya kufundishia ili kuepuka usumbufu wa kutafuta shule za aina hii, ambazo ni chache na inayotambulika ni ya Buguruni tu, ambayo haitoshelezi mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Napenda kutoa pongezi kwa Wizara ya Afya, kwa kuleta Azimio hili. Nachukua nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Afya, Mheshimiwa Profesa Mwakyusa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dokta Aisha Kigoda, Katibu Mkuu na Wataalamu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Azimio hili linahusika na haki za walemavu ni vyema ikaeleweka kwamba, walemavu wengi huishi katika mazingira magumu, hasa wale waishio makambini kama vile Kambi ya Ipuli. Katika Manispaa ya Tabora kuna walemavu wengi wasiojiweza, tunapoingia mikataba ni vyema tukaangalia na makazi yao, kwani wana haki pia kupewa nafasi ya kulindwa na mkataba huu. Kwa kweli haki za binadamu kwenye kambi hiyo haipo kutokana na mazingira yalivyo, hususan chakula ni kibaya sana. Wapo walemavu ambao hawana viungo vya miguu na mikono; naomba ufafanuzi wa kina wa kambi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kwa kweli tatizo hilo ni kubwa kiasi kwamba, mara kwa mara ukienda hukutana na matatizo. Afya zao na usafi wa mazingira haufai, hawapewi chakula kwa wakati na kusababisha kutoka nje kuomba omba kwa kuwatuma watoto wao au vijukuu kwa kuwa wao hawaoni wala hawatembei. Majengo wanayoishi ni mabovu na hakuna hata vyoo. Kwa kuwa Waziri alifika, naomba maelezo ili niweze kupeleka kwa walemavu hao kwa kutumia Bunge lako; Naibu Waziri ndiye aliyefika kwenye kambi hiyo.

Chuo cha Rwanzali, kilifungwa na hakina majengo mazuri na mpaka sasa hakitumiki. Naibu Waziri, alikitembelea Chuo cha Ustawi wa Jamii kilichopo katika Manispaa, ingawa watumishi wenye sifa za kuendesha wapo kwani ni cha walemavu. Shule ya msingi ya wasiojiweza ambao wana ulemavu wa kutosikia, mtindio wa ubongo, pia hupata matatizo ya kutopata huduma ingawa ilianzishwa na Pentekoste na kushindwa kuiendeleza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Azimio hili liingie katika kuliona hili ili walemavu waweze kutendewa haki, kwa kupewa elimu na afya, kwani watoto hao hutia huruma wanapokosa msaada. Shule hii ipo katika Manispaa ya Tabora. Kwa kuwa

Halmashauri za Manispaa hazina uwezo ni vyema Wizara ikatafuta wafadhili ili waendeshe au kuchangia miradi ya walemavu, ambao tayari wamekuwa kwenye makambi au vyuo hapa nchini.

Mwisho, naomba Wizara izungukie maeneo hayo kwa kutuma wataalamu wake. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio ni zuri; likipitishwa litasaidia walemavu ambao wengi wapo vijijini. Ninachosema, Azimio hili likishapitishwa, Wizara iharakishe kuwafikia walengwa walipo sehemu zote. Kama tunavyojua, kuna baadhi ya watu wanatumia vibaya pesa za watu wenye UKIMWI, wanafaidika nazo na si walengwa. Walemavu watendewe haki. Sasa hivi hawa ndugu zetu ndiyo wanaotafutwa sana, pamoja na uonevu mbaya sana, walemavu wengine wapo majumbani mwetu kwa kukosa vitendea kazi na wengine wengi wapo mashuleni lakini hawana vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru Azimio hili kuja, ingawa limechelewa kwa sababu hata hawa ndugu zetu wasingekuwa wanapata matatizo mengi, ikiwa ni pamoja na Walimu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio hili.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Mkataba huu ni muhimu mno kwa Taifa letu, hasa ukizingatia nia na madhumuni yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wenye ulemavu kwa muda mrefu wamekuwa wakinyanyaswa na kunyanyapaliwa eti tu kwa ajili ya ulemavu wao. Ieleweke wazi kuwa, watu hawa wana uwezo mkubwa sana kiakili na ndiyo maana wale waliobahatika kupata elimu, wamefanikiwa sana na hata kufikia *PhD* na hata Uprofesa; tena si kwa njia ya *online* kama baadhi ya wenzetu wasio na ulemavu wanavyofanya. Hii ni ishara tosha kwamba, wakiwezeshwa wanafanya maajabu

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wenye ulemavu wamekuwa wakidhalilishwa sana hasa katika masuala ya uzazi. Imeonekana wazi kwamba, kundi hili halistahili kuwa na watoto na ikitokea mwanamke mlemavu anapokwenda *clinic* kwa ujauzito, anatukanwa matusi mazito na maneno ya kejeli kama hee na wewe unabeba mimba? Lazima ieleweke ulemavu hauna uhusiano wowote na *biological needs,* yaani *sexual feelings*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia ni jinsi gani ombaomba wengi wakiwa ni watu wenye ulemavu na sababu kubwa ni ukosefu wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujongeaji *(accessibility)* ni tatizo kubwa mno kwa watu wenye *physical disabilities,* lakini cha ajabu hata majumba yanayojengwa sasa hivi hayana njia za watu wenye ulemavu. Suala hili linawapa tabu hata kuwazuia kufanya shughuli zao eti kwa kuwa tu wanashindwa kufika!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna methali isemayo hujafa haujaumbika; sote tukilitambua hili, basi tunaweza kuona umuhimu wa mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukosefu wa visaidizi na mazingira rafiki na unyanyapaa, wenye ulemavu wengi wamekuwa wakibaguliwa na hata kukosa ajira. Waajiri wengi wanaona ni hasara kumwajiri mlemavu, kwani anaweza kuchelewa kazini au ule mtazamo hasi kwamba mlemavu hana uwezo kiakili na kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunajua matatizo na dhamana inayowakabili albino hapa Tanzania, hali iliyopelekea Tanzania kuonekana nchi ya ajabu sana katika uso wa dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wamekuwa wakiwaua kikatili na hata wengine kukatwa viungo. Baadhi ya familia zenye watoto hawa zimeomba ulinzi Serikalini, lakini bado hili ni tatizo na tunaomba Serikali iwatazame kwa jicho la huruma na la kibinadamu zaidi.

**MHE. MAIDA H. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuleta Azimio hili kwani limekuja wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa wenye ulemavu bado unyanyapa upo nchini kuanzia vijijini hadi mijini. Kuanzia ulemavu wa ngozi, macho, viungo na mengineyo, unyanyapaa unakuwepo katika sehemu mbalimbali za ajira, ulinzi na usalama, uhuru wa kutoa maoni na maamuzi katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, kwa kuweka saini mkataba wa nyongeza unaohusiana na watu hawa mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa sasa ipo haja ya kuleta sheria rasmi inayohusiana na watu hawa, baada ya kupitishwa Azimio hili.

Itakapoundwa sheria, itawalinda wale wote ambao watahusika kwa njia moja au nyingine kuwadhalilisha, kuwaudhi, kuwaua watu hawa na kuwa na haki ya kutembea kifua mbele katika nchi yao.

- Itakapoundwa sheria watakuwa na uhuru wa kwenda popote kutafuta ajira.

- Kuwa na uhuru wa kuishi popote bila kuishi kwa wasiwasi wale wanaouawawa bila kuwa na makosa ya aina yoyote.

- Kuwa na uhuru wa kutafuta elimu mahali popote.
- Kuongezeka kwa nafasi za uongozi kupitia makundi hayo.

- Kuendeleza kupatiwa nyenzo zaidi kwa wale wasiojiweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya, pamoja na Naibu wake. Naipongeza pia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kwa kuweza kuujadili kwa kina mkataba huu hadi kufikia kuletwa Azimio hili hapa Bungeni leo hii. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa jinsi alivyowasilisha kwa lugha nyepesi Azimio hili na kusikika na Watanzania wote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa maandishi na napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wao, kwa kuleta Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulamevu *(The Convention on the Right of the Persons with Disabilities*) na kuridhia Mkataba wa Nyongeza wa Kimataifa kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu *(The Optional Protocol to Convention on the Right of Persons With Disabilities).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naunga mkono Azimio hili na nyongeza yake. Naipongeza Serikali hivi sasa kwa kuliangalia kwa karibu kundi la jamii hii. Yapo mambo ya kufuatilia kwa karibu hasa katika kuwawezesha kiuchumi na kielimu, kwa sababu kundi hili hivi sasa wengi bado wapo majumbani, wafuatiliwe kupitia Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kitu kibaya kama unyanyapaa. Elimu itolewe kwa umma juu ya upendo ili kuboresha na kulinda utu na haki za watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza ya (*The Optional Protocol to Convention on the Right of the Persons With Disabilities*) pia imeridhiwa na nchi kutambua na kutoa haki za watu wenye ulemavu na makubaliano yote yatekelezwe kwa wakati. Hivi sasa kundi hili limepata matumaini sana kwa jinsi linavyoshughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilete Muswada wa Sheria ili lengo zima likamilike na utekelezaji wake uwe wa kisheria na jamii hii ya watu wenye ulemavu waishi kwa kupata huduma stahili, upendo na amani.

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, tunaishukuru Serikali kwa kusaini na leo hii kuridhia mikataba hii miwili muhimu, juu ya haki za watu wenye ulemavu. Kwa kweli hatua hii ni ya kupongeza na inaonyesha nia thabiti ya Serikali ya CCM, kutekeleza kwa vitendo Ilani ya Chama ya mwaka 2005, ambayo imeweka bayana masuala ya watu wenye ulemavu katika Ibara ya 106 na 123.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa Mikataba hii ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, lengo la Mikataba hii ni kukomesha aina zote za ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu katika nyanja zote za kimaisha na kiuchumi.

Pili, kuitaka Serikali kuweka masuala ya haki za watu wenye ulemavu katika Sheria za nchi ikiwemo Katiba na kuondoa sheria zinazowakandamiza.

Tatu, kuwataka wadau muhimu kama vile Serikali na sekta binafsi kuyapa kipaumbele masuala ya watu wenye ulemavu katika shughuli zao kama vile miradi ya maendeleo, upatikanaji wa habari na utoaji wa huduma muhimu kwa umma.

Nne, kuhimiza umuhimu wa kutoa elimu ya haki za watu wenye ulemavu ili kuinua uelewa wao.

Tano, kuwataka wafadhili wa maendeleo kuyaweka masuala ya walemavu katika misaada wanayoitoa kwa Tanzania.

Sita, kutambua lugha ya alama kwa viziwi katika mawasiliano pamoja na maandishi ya nukta nundu (*Braille*) kwa wasioona.

Saba, kuhimiza uundwaji wa chombo cha Kitaifa ambacho kitaratibu na kufuatilia utekelezaji wa mikataba hii nchini Tanzania.

Nane, kuundwa kwa Kamati ya Kimataifa itakayosimamia na kuratibu ufuatiliaji wa haki za watu wenye ulemavu duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, naomba Serikali iharakishe kukamilisha hatua ya tatu, ambayo ni kutungwa sheria ya nchi, itakayotumiwa na watu wenye ulemavu, kudai haki katika vyombo vyetu vya kusimamia na kutoa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umecheleweshwa sana na haijulikani ni lini Serikali itauleta hapa Bungeni kuujadili. Mheshimiwa Waziri anaombwa na jamii ya watu wenye ulemavu kusema ni lini Muswada utaletwa Bungeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kila la kheri.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia kuwa wazima na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii, kuishukuru Serikali kwa kuleta Maazimio haya mawili kwa pamoja, ingawa yamechelewa kidogo kwani Maazimio haya ni muhimu sana, hayahitaji kucheleweshwa hata kidogo kwa kuwa yanagusa maisha ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hasa lililonisababisha kuchangia Maazimio haya ni kuiomba Serikali kwamba, baada ya kuyaridhia Maazimio haya, ihakikishe kuwa, inayatekeleza na si kuyaridhia tu na baadaye ianze kuleta visingizio kuwa bajeti ni finyu au tupo kwenye mchakato.

Hili ni jambo linalohusu maisha ya watu na watu wenyewe wengi wao hawana uwezo; hivyo basi, wapewe kipaumbele ili waweze kusaidiwa. Sasa isiwe kama ilivyo sasa, kuwasaidia walemavu ni hisani na siyo wajibu wa Serikali. Sasa Serikali iyatekeleze Maazimio haya kikamilifu ili watu wenye ulemavu nao wapatiwe stahili zao kama zinavyotajwa katika Maazimio yenyewe. Sina haja ya kuzitaja hapa kwani zimeelezwa vizuri sana kwenye Maazimio yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mengi kwa leo, isipokuwa maelezo yangu hayo mafupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayaunga mkono Maazimio haya yapite na baadaye sheria yake iletwe haraka ili tumalize tatizo hili la watu wenye ulemavu. Ahsante.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninapenda kuwapongeza wale wote wanaosaidia watu wenye ulemavu wa viungo. Kumsaidia mwenzio ni uungwana. Kwanza, nianze na Rais Kikwete, ambaye alimteua Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, ambaye anatoa mchango mkubwa kwa walemavu na vile vile Rais anawasaidia sana walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Marais wa Awamu zote zilizopita, wamesaidia sana walemavu kwa hali na mali. Taasisi za watu binafsi na Mashirika ya Dini ambayo yamesaidia sana walemavu ni kama ifuatavyo:-

(i) Ndugu Reginald Mengi, amewasaidia sana watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali kwa kuwapatia misaada mbalimbali. Tunamshukuru sana.

(ii) *NGO* ya *EOTF* ya Mama Anna Mkapa, imesaidia sana wale walemavu kwa kuwapa baiskeli za walemavu wa viungo. Ahsante sana.

(iii) Kanisa la *Christian Mission Fellowship,* linaloendeshwa na Archbishop Mgullu Kilimba, Dar es Salaam, limesaidia sana baiskeli na linaendelea kusaidia na hivi sasa linaendelea kutoa baiskeli za walemavu wa viungo. Ahsante sana.

(iv) Taasisi, *NGO* na Mashirika yote ya Dini ambayo hapa sikuyataja, kwa kweli ninawashukuru sana kwa misaada yao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nichukue nafasi hii, kuwalaani wale wote wanaopokea misaada ya walemavu wa viungo, halafu hawapeleki kwa wahusika au walengwa. Hiyo ni dhuluma na ni ufisadi mwingine, tuache. Misaada yao tuwapelekee wenyewe tunapokabidhiwa. Endapo wakigundulika ambao hawapeleki kwa walengwa, tunaomba Serikali ichukue hatua na sheria zichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Wizara ya Elimu izisaidie shule za watoto wenye ulemavu mbalimbali. Wafikirie pia suala la ufundi mashuleni, kwani walemavu wanapenda sana masomo ya ufundi. Endapo kuna shule za msingi zimejengwa pamoja na shule za walemavu, tunaomba mgao wao wa pesa za MMEM wapewe tofauti, kwani tunataka dhana ya utawala bora ifanyike. Kwa mfano, Shule ya Msingi ya Nyangao,

Lindi na Shule ya Msingi ya Watoto Wenye Ulemavu Nyangao Lindi, pesa zao za MMEM zisiwekwe kwenye mfuko mmoja; kila shule iwe na *account* yake. Hilo ni ombi lao ambalo wameniomba mimi nilipowatembelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazazi wenye watoto wenye ulemavu wa viungo wawapeleke shule, wasiwafiche. Siku hizi kuna kila utalaamu wa kumfanya mtoto huyo aweze kusoma. Watoto wote wasioona, wasiosikia, wasiosema, wasioweza kutembea, wote wapelekwe shuleni, siyo aibu tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali itoe nafasi za upendeleo kwa walemavu wa viungo katika uongozi Serikalini, kuanzia ngazi za chini hadi juu (Serikali za Mitaa, Kitongoji, Kijiji, Kata, Jimbo na Ubunge). Kwa Wabunge waliopo sasa ni nafasi zilizotolewa kwa upendo wa Rais kumteua Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir na upendo huo huo kuwateua Wabunge wawili wa Viti Maalum Wanawake. Vilevile tunaahitaji Wabunge Wanaume.

Kwa hiyo, tunasema nafasi tatu za Wabunge ni za CCM tu. Tunaiomba Serikali kwa makusudi, itoe nafasi maalum bila kujali jinsia kwa Wabunge, vilevile kwa ngazi za chini ambako kuna Wananchi ili waweze kuwatetea wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba tusawaidie watu wenye ulemavu.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia napenda kutoa pole nyingi sana kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba, ambaye alikuwa mmoja wetu katika Kamati ya Huduma za Jamii.

Nampongeza Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na pia Wafanyakazi wa Wizara hii, kwa kuleta Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kutunga sheria ambazo zatalinda hali na maisha ya walemavu na kuhakikisha kuwa, sheria hizi zinajali na kuhakikisha walemavu wanapata uhuru wa kuishi.

Hali za binadamu ni kwa watu wote wakiwemo walemavu, wanawake, watoto na kadhalika. Unyanyapaa ni udhalilishaji mkubwa wa binadamu, kwa maana hiyo naomba Sheria zitakazowabana wale wanaowanyanyapaa wenzao zitungwe, pale wanapojulikana kufanya ukatili, adhabu kali zitolewe katika eneo hili. Kwa mfano, watu wanaopigwa na kukatwa viungo vyao, kama vile kukatwa mikono, miguu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uuaji ni kosa la jinai, kwa maana hiyo adhabu ya kifo inastahili kutolewa kwa wauaji. Walemavu wa ngozi wameushtua sana ulimwengu mzima, kwa kukatwa viungo vyao hata kuuawa, kwa sababu za ushirikina. Jambo hili limeleta aibu kubwa sana katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu katika Azimio hili ni yafuatayo:-

Kwanza, walemavu wote watambuliwe mahali walipo na wanapoishi.

Pili, Serikali na Jamii kupata idadi ya walemavu katika Mikoa na kuwa na Kamati husika katika Wilaya.

Tatu, Walemavu wote kupatiwa huduma muhimu katika jamii kama vile elimu, ajira na kadhalika.

Nne, Serikali kuendelea kuwasaidia walemavu wapate miradi na pia wapate mikopo yenye riba nafuu katika kupunguza umaskini.

Sita, Serikali ijitahidi kuwapatia viungo bandia, vitakavyopatikana kwa bei nafuu na hata vingine wapewe bure hasa kwa walemavu wasio na uwezo wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaunga mkono hoja na kumpongeza Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo ulemavu wa aina mbalimbali; upo ule unaoonekana lakini yote ni upungufu. Ni naomba nijikite kwenye ulemavu uliofichika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walemavu kama waliofanyiwa opereshini ya kukatwa titi/matiti, walemavu waliopasuliwa moyo; walemavu waliobadilishiwa figo, walemavu wenye jinsia mbili na kadhalika; Watu hao wanasaidiwaje kwenye jamii bila kuwazidishia machungu kwa kuweka wazi ulemavu wao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sheria itakapokuwa inatungwa, mambo hayo ya usiri yazingatiwe. Ahsante.

**MHE. MCH. DR. GETRUDE P. RWAKATARE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niungane na wanzangu wengi, kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote, kwa kazi nzuri wanazofanya na waliyoiandaa. Suala la walemavu linatuhusu sote kwa sababu hujafa hujaumbika; sote tunaweza kuwa walemavu kwa ajali, ugonjwa au njia yoyote ile.

Ninaunga mkono hoja mia kwa mia ila nashauri yafuatayo:-

(i) Mauaji ya Albino yakomeshwe;
(ii) Walemavu wawezeshwe kiuchumi;
(iii) Mama cheza waongezeke ili wasambazwe hadi kwenye ngazi za hospitali za wilaya; na
(iv) Mwisho ninaomba sheria kuhusu walemavu ikamilishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafashi hii, kwa njia ya maandishi, kuipongeza Serikali kwa kuleta Maazimio ya Bunge ya Kuridhia Mikataba yote miwili. Kabla sijaanza kutoa maoni yangu, natamka rasmi kuwa, kwa moyo mkunjufu, naunga mkono Maazimio yote mawili. Hivyo basi, naomba niaze kutoa maoni yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu, serikali imeamua kuleta ili Bunge lijadili kisha iwe sheria ya kulinda haki zao. Ninaomba Serikali ifuatilie kwa karibu sana, kuona kuwa haki za msingi zilizoainishwa zinatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa shule za viziwi na mabubu sasa hivi zipo; ni vyema sensa ifanyike wapatikane watu wote wenye ulemavu wa aina hii ili wapatiwe elimu, iwasaidie kuishi maisha bora yenye kuwasiliana na Watanzania wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiojificha kuwa, watu wote wenye ulemavu wa viungo hupata tabu sana; mfano, hushindwa kujihudumia kusogea sehemu moja hadi sehemu nyingine. Kwa kuwa ni haki yao ni vyema Serikali kuhakikisha kila mlemavu anapatiwa huduma, sambamba na ulemavu wake; mfano, kama hana mkono atengenezewe mkono wa bandia, kwa wale wasiotembea watengenezewe magongo na baiskeli ili waweze kutembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwa kujenga shule za watu wenye ulemavu wa macho. Hivyo basi, watafutwe wenye umri wa kwenda shule wapelekwe shule wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hata wenye ulemavu huweza kuvunja sheria au kutokutendewa haki na mtu yeyote; ni vyema kuwe na watu wa kuwasemea sambamba na ulemavu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wenye ulemavu wengi wanakosa ajira, kwa sababu tu ya kuwa na ulemavu. Ninaiomba Serikali kupitia Azimio hili; ni vyema iwe tayari kuwapa ajira watu wenye ulemavu ilimradi wanazo sifa, sambamba na wale wasio na ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiopongeza serikali kwa kutenga nafasi za Wabunge wa Viti Maalum, Kundi La Walemavu. Hivyo basi ni vyema taasisi mbalimbali za serikali na sekta binafsi, kutenga nafasi za watu wenye ulemavu ili na wao waweze kutoa michango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba itungwe sheria inayohusu watu wenye ulemavu. Serikali iendelee kuangalia upatikanaji wa fursa na stadi kwa watu wenye ulemavu. Vilevile ni vyema kuwepo na mikakati ya kulinda usalama wa kijamii wa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kwa kusema kuwa, ninaunga mkono Maazimio haya yote mawili.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza Wizara ya Afya kwa kuleta Azimio hili, kwa manufaa ya watu wote wenye Ulemavu, ndugu jamaa na wote tunaoitwa walemavu watarajiwa.

Azimio hili kwangu mimi naliona ni letu sote tuliomo humu, linatuhusu kwa njia mbalimbali. Mimi nashauri kuwa, kazi iliyo mbele yetu ni kuiomba Serikali iandae kwa haraka sheria yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo yangezingatiwa kwenye sheria hiyo ni pamoja na:-

(a) Haki ya kupata huduma za afya, elimu na ajira kwa upendeleo maalumu;

(b) Haki ya kulindwa na kujenga utu miongoni mwao.

(c) Haki ya kutoa maoni, kujieleza na kuhamasisha jamii ili wajue wajibu wao katika kuishi vizuri na walemavu kwa amani na utulivu; na

(d) Kuweka ndani ya sheria ili sekta binafsi na asasi mbalimbali za mashirika na madhehebu ya dini zisiwabague walemavu katika kutoa huduma zao kwa usawa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, sheria itoe nafasi ya adhabu kali kwa wale wote watakaoonekana wanavunja kwa makusudi, maelekezo ya sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia nikawa mzima nikaweza kuchangia mikataba hii miwili iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa mikataba hii imechelewa, lakini hatimaye imekuja na jambo muhimu ninaloliomba, uletwe Muswada wa Sheria kwani mikataba hii bila ya sheria haiwezi kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ijipange vizuri ili kuhakikisha kuwa, maudhui yote haya yanatekelezwa kwa vitendo sio kubakia makaratasini tu. Mikataba hii kama itatekelezwa sawa sawa, itaweza kuwakomboa ndugu zetu wenye ulemavu na vile vile itakuwa tumewawekea misingi mizuri, kwani ulemavu unaweza kuja wakati wowote kwa binadamu kwani kabla hujafa hujaumbika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali izidi kujitahidi kuwapatia wataalamu wa kutosha watu wenye ulemavu, kuanzia madaktari wa viungo, manesi na walimu wanaoweza kuwafundisha alama zote zinazoendana kwa mujibu wa ulemavu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanjari na hayo, wapatiwe elimu bure na vifaa kwani vitu hivi ni ghali sana. Kutokana na hali ya wenzetu hawa kuwa ni wanyonge na hawana uwezo; Serikali iwaangalie kwa jicho la rehema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali izidishe jitihada zake kwa kuwasaidia kuwalinda watu wenye ulemavu wa ngozi, kwani na wao wana haki ya kuishi na kupata mahitaji yao kama watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na vilevile naunga mkono hoja hizi zote mbili zilizokuweko mbele yetu ili kutoa nafasi ya kufanyiwa kazi na kutekelezwa. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri ya Kuridhia Azimio la Bunge la Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu pamoja na Mkataba wa Nyongeza wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea nami naomba nichukue nafasi hii kutoa salamu zangu za pole kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Tanga kwa wananchi wa Jimbo la Busanda kwa kumpoteza mpendwa wao Mbunge mwenzetu marehemu Kabuzi Faustine Rwilomba. Lakini wao walimpenda ila Mwenyezi Mungu alimpenda zaidi kwa hiyo tunaomba Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi roho yake. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kabla sijaendelea nitamke kwamba naunga mkono hoja iliyowasilishwa. Nashukuru sana kwa Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ambayo imeletwa mbele yetu kwa kweli hii inaonyesha kwamba kweli Mkataba huu ulikuwa una umuhimu sana kama walivyoeleza kwa maana hiyo sisi tunashukuru kwa vile itatusaidia sana wakati tutakapokuwa tunaleta Muswada wetu hapa unaohusu watu wenye ulemavu. Sasa nitachangia kwa kujibu hoja za Wajumbe baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia na mwisho Mheshimiwa Waziri naye atakuja kumalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii Dr. Haji Mwita Haji alikuwa ametoa hoja kwamba kuwepo na sheria itungwe inayohusu watu wenye ulemavu na pia akasema kwamba kuweka mikakati na kuhimiza sekta binafsi, asasi na Mashirika ya Kidini, kuwekeza katika utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi kwa watu wenye ulemavu.

Wizara tayari imeshaandaa Muswada wa Sheria ambao upo katika mchakato wa kuwasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri na unatarajiwa kuwasilishwa kwenye Mkutano

wa Bunge mwezi Oktoba, 2009. Katika kuweka mikakati kupitia sera ya watu wenye ulemavu, sekta binafsi na Mashirika ya Dini yanahamasishwa katika utoaji wa huduma za jamii ikiwa ni pamoja na huduma za watu wenye ulemavu. Lakini vile vile Mheshimiwa Dr. Haji alisema kuongeza ubunifu wa stadi na upatikanaji wa fursa kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vya watu wenye ulemavu vinafundishwa stadi mbalimbali kulingana na mahitaji ya soko kwa hiyo hili suala Wizara inaendelea kulifanyia kazi. Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali vile vile na Mheshimiwa Shoka Khamis Juma wamesema Serikali iandae kutekeleza ibara zote za Mkataba na iandae *action program*. Serikali itaunda Kamati ya Utekelezaji wa Mikataba na kila jitihada itafanywa kuhakikisha utekelezaji ni timilifu. Mpango wa utekelezaji utaandaliwa na kutekelezwa na Waheshimiwa watakaopata fursa ya kuuona.

Mheshimiwa Margareth Mkanga na Mheshimiwa Zulekha Yunus, Mheshimiwa Bujiku Sakila wao kwa ujumla wao napenda niwapongeze kwa kweli kwa michango yao mizuri sana ambayo wameitoa walipokuwa wanachangia na wenyewe walikuwa wanazungumzia suala la Sheria ya Watu Wenye Ulemavu kwamba iwasilishwe kama alivyokuwa amesema Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii. Kama nilivyosema kwamba sasa hivi tuko katika hatua nzuri na Mwenyezi Mungu akitujalia Oktoba, 2009 basi tutaweza kuujadili hapa na hatimaye itakuwa sheria kamili hivyo yote haya mambo yatakuwa yameingizwa katika hayo.

Mheshimiwa Margareth Mkanga na Mheshimiwa Bujiku Sakila vile vile Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy, Mheshimiwa Getrude Rwakatare na Mheshimiwa Mwanne Mchemba wao wamezungumzia wataalam wa Ustawi wa Jamii ambalo hili pia nimeona Mheshimiwa Beatrice Shellukindo pia amelitaja wataalamu wa Ustawi wa Jamii kwamba hawatoshi lakini vile vile wamezungumzia kuhusu suala la wacheza viungo na wataalamu wa lugha ya alama wanatakiwa waongezwe ili kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba wataalam hao wanaongezwa. Kwa mfano, mwaka 2006 Maafisa Ustawi sita waliajiriwa na mwaka 2008 waliajiriwa Maafisa Ustawi 20 na mwaka huu wametangaza nafasi 15. Hao wataalamu wa Ustawi wa Jamii kweli kabisa ni kwamba hawatoshelezi lakini sasa hivi Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na TAMISEMI kwa kushirikiana tumeamua sasa kila Wilaya iwe na Afisa Ustawi.

Lakini vile vile tumezungumza Wizara ya Afya pamoja na TAMISEMI ili kuhakikisha kwamba katika ngazi za Kata kuweze kuwepo pia na Wasaidizi wa Ustawi yaani ambao wataitwa *Welfare Assistants* ambao watafanya katika ngazi ya Kata. Kwa hii inamaanisha kwamba ni lazima pia kuwepo na wanafunzi ambao watakuwa wanafuzu katika vyuo husika.

Kwa hiyo, hao wataalam napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba wataalam ambao ni wa Ustawi wa Jamii nafasi zipo na kama za kuajiriwa na wenyewe wanaweza wakaajiriwa wakati wowote. Kwa hiyo tungeomba vile vile pia

Halmashauri zetu pale ambapo wanaona hawapo basi waombe katika Utumishi ili waweze kuletewa hawa Maafisa Ustawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile lipo suala la wataalam wa alama nadhani hili litabidi Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Ufundi wao ndio watachukua hili ili waweze kuhakikisha kwamba hawa wataalam wanapatikana ili waweze kikidhi katika yale maeneo ambayo kweli kabisa wanahitajika. Kwa sababu haiwezekani mwanafunzi akiwa anafundishwa wakati haelewi anahitajiwa wataalam kama tunavyoona pale kwenye galary. Lakini suala la wachezesha viuongo, nakubali kabisa ni wachache na chuo tulichonacho sasa hivi ni KCMC na sasa hivi kwa kweli ni wanafunzi wachache ambao wanafuzu kutoka chuo kile.

Lakini nichukue labda nichukue nafasi hii kwamba sisi kama Wizara tunajukumu la kuwaelimisha wananchi au wale wanafunzi ambao wanamaliza shule kidato cha nne na cha sita ili wajue kwamba wengi wanaonekana kwamba hawapendi hili somo kwenda kulisomea aidha hawaoni labda umuhimu wake lakini sisi kama Wizara basi tutachukua jukumu kuweza nkujitangaza zaidi ili tuweze kudahili wanafunzi wengi zaidi, ambao tutawapeleka katika ngazi za mikoa lakini vilevile tutawapeleka katika ngazi za Wilaya.

Ni kweli kabisa tunakiri kwamba hawa wachezesha viungo ni wachache sana. Lakini vilevile tunampango wa ku-review mitaala ili kuhakikisha kwamba hawa wachezesha viuongo na wenyewe wanamaliza mafunzo kwa muda mfupi zaidi ili tuwapate wengi.

Mheshimiwa Margret Mkanga, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Riziki Lulida, wamezungumzia kuhusu ujongeaji kwa watu wenye ulemavu lakini vilevile wamezungumzia majengo ya shule ambayo si rafiki lakini vilevile wamezungumzia maeneo kwamba majengo ni marefu hakuna lift lakini pia unakuta hata wale watumiaji wa fimbo kwa mfano fimbo nyeupe, unakuta hawakutengewa mahali pa kuweza kutumia zile fimbo zao wakati wanapokuwa wanatembea.

Wizara imepokea ushauri huo na itaufanyia kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na suala la ujongeaji limezingatiwa katika Serikali ya maendeleo na huduma kwa watu wenye Ulemavu na Muswada wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu itajitokeza hiyo. Kwa hiyo vilevile tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili katika yale mashule na watu wa miundombinu waweze kutoa muongozo wa shule zijengwe namna gani ili ziwe rafiki kwa watumiaji hawa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mkanga na Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy wamesema Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza bei ya nyenzo na kujimudu, lakini hili pia nimeliona pia amelizungumzia Mheshimiwa Rished, Wizara imepokea ushauri huo na itawasiliana na Wizara ya Fedha na Uchumi kuona utekelezaji wa kupunguza bei ya nyenzo za kujimudu.

Mheshimiwa Mkanga pia alisema Sheria ya watu wenye Ulemavu izingatie haki

ya kuishi kwa watu wenye ulemavu. Ushauri huu umepokelewa na suala la haki ya kuishi kwa watu wenye ulemavu itazingatiwa katika Muswada huo. Mheshimiwa Sikila amesema utekelezaji wa mikataba hii uzingatie utamaduni wa watanzania, tunakubaliana nae na ushauri huu tumeuzingatia kwenye utekelezaji wa Mikataba hii itazingatia taratibu na utamaduni wa nchi yetu.

Mheshimiwa Riziki Lulida, tunashukuru kwa pongezi zake, lakini na yeye amezungumzia kuhusu masuala ya ukatili dhidi ya walemavu, akazungumzia haki za watoto wa kike na wanawake na haki za wale ambao wanazalisha akinamama walemavu halafu wanakataa.

Lakini sasa nafikiri na yeye mwenyewe amesema ile sheria ya vinasaba vya binadamu DNA nadhani hapa ni mahali pake lakini vilevile tutaendelea kutoa elimu ili watu waweze kuona kwamba kuzaa na mtu mlemavu si kitu cha aibu kwa sababu mtu mwenye ulemavu ni binadamu kama mtu mwingine na ana mahitaji yake ya kibinadamu kama mtu mwingine yoyote. Lakini pia amezungumzia kuhusu mambo ya ajira nafasi za upendeleo, ushauri tumeupokea, bajeti ya ustawi na vifaa vya kujimudu kama alivyosema vyote hivi tutavizungumza na muswada wa Sheria utazingatia hilo.

Mheshimiwa Rished amesema kwamba kodi za vifaa na misamaha, lakini pia amesema ni bora kama vifaa hivi vikapitia MSD na pia alizungumzia masuala ya miundombinu na vifaa mashuleni. Hili nasema kwamba Wizara tunazingatia ushauri huu lakini pia tutashirikiana na Wizara ya Fedha kuweza kuona misamaha na suala la kupitisha vifaa Serikali tutakaa tuone ni utaratibu upi mzuri ambao tutaweza ili kuhakikisha kwamba yote haya yanalenga vifaa vya kutumia viweze kuwa na bei ndogo.

Mheshemiwa Idris Mtulia alituelezea historia akatuambia kwamba ikiwezekana achaguliwe Mbunge Mlemavu aweze kuwa Waziri. Hii ni nzuri. Lakini mamlaka ya kuteua Mawaziri ni ya Mheshimiwa Rais kwa hiyo tunamwachia Mheshimiwa Rais mwenyewe atatumia busara zake anavyoona kadri inafaa. Watu wanaoishi na walemavu wasaidiwe elimu zana na kadhalika. Hili tumesema tutashirikiana na Wizara ya Elimu kuweza kuona, kwa hiyo tunapokea ushauri.

Mheshimiwa Shellukindo alitoa pongozi tunazipokea na akashauri kwamba tuhakikishe katika ile Kamati Maalum ya Kimataifa basi Tanzania tuwemo; ni kweli ni wazo zuri kwa hiyo kama sisi tumeridhia na kwa sababu tunajua kwamba tuna watu wengi wenye ulemavu basi tutaangalia kila mbinu tuweze kuona kwamba na sisi tunaingia katika hili. Lakini vilevile anasema kwamba huu utendaji uhusishe na watu waliokuwa katika kule kwenye grassroot na mimi ndiyo nafikiri Mkataba ndivyo unavyotueleza kwa sababu tutauridhia basi na Sheria itakapokuja basi tutaona ni jinsi gani wale watu wa ngazi ya chini wanaweze kufikiwa.

Lakini vilevile amezungumzia wale watu wenye ulemavu kwa faida yao kwa kweli si kitengo kizuri na mimi nachukua nafasi hii pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge tukemee kwa sababu hawa wenzetu sio kama tuwafanye ni stepping radar, tuwatumie kama walemavu lakini pesa tunatumia kwa mambo mengine. Wale wote

ambao wanapata misaada kupitia kwa wafadhili mbalimbali basi ni bora kuwe na utaratibu mzuri ili ziwefikie walengwa.

Pia Mheshimiwa Mbunge alizungumzia kuhusu dhamana ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hasa kazi ya Ustawi wa Jamii. Kama nilivyosema mwanzo kwamba tunampango wa kuwapeleka Maafisa Ustawi mpaka katika ngazi za Kata. Kwa hiyo Mhushimiwa Mbunge tuweze kuvuta subira tuweze kuona ni jinsi gani nzuri ili tuweze kutufikisha kwa hatua kwa sababu kwanza walikuwa Wizara ya Afya sasa wote tunawasogeza kwenda TAMISEMI kutoka TAMISEMI na wenyewe wataendelea mpaka kwenye zile ngazi za Kata.

Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Maida H. Abdallah, Mheshimiwa Zulekha Yunus, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Ania Chaurombo, Grace Kiwelu, Khadija Al-Qassmy wamesema itungwe sheria ya watu wenye ulemavu itakayowezesha kudai haki zao na kupata huduma pia wapate upendo na amani. Hili nafikiri nimeshalijibu. Lakini Mheshimiwa Maida na Mheshimiwa Janeth Kahama wamesema watu wenye ulemavu wapewe uhuru wa kuishi. Ushauri umepokelewa na suala la haki ya kuishi kwa watu wenye ulemavu linazingatiwa katika Muswada wa Watu wenye Ulemavu linazingatiwa lakini vilevile limeongelewa katika Mkataba huu. Mheshimiwa Chilolo na Maida Abdallah, wamesema kuongezeka kwa nafasi za uongozi katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshaanza kuongeza nafasi za watu wenye ulemavu katika nyanja mbalimbali kwa mfano Waheshimiwa Wabunge sasa hivi wapo wanawawakilisha watu wenye ulemavu, lakini nadhani tutoe tu wito; kwa sisi Chama cha Mapinduzi hili tunalizingatia ndiyo maana mmewaona wako hapa, kwa hiyo tunawaomba na wale wenzetu kwenye vyama vingine basi na wenyewe wafikirie kuona kwamba wanazingatia hili kupata wawakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti naendelea kwa sababu nimepata ruhusa kwaMheshimiwa Waziri; kwa hiyo wenzetu na wenyewe wafikirie jinsi ya kuongeza uwakilishi katika nyanja za siasa. Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo na Mheshimiwa Maida, na Mheshimiwa Janeth Kahama na watu wenye ulemavu wapatiwe nyenzo za kujimudu, Wizara inatoa nyenzo za kujimudu kwa watu wenye ulemavu ingawa haitoshi kwa kweli tunakubali jitihada zinafanyika kuhakikisha kwamba huduma hii inaboreshwa kwa kushirikiana na Wizara pamoja na mashirika binafsi na watu wengine ambao wanaweza wakajitolea.

Mheshimiwa Yunus na Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Kiwelu wamesema watu wenye ulemavu wapewe elimu, ajira lakini Mheshimiwa Lulida nae alesema wapewe kipaumbele wanapokuwa katika short listing lakini wamezungumzia upatikanaji wa fursa na *study* kwa watu wenye ulemavu lakini vilevile haki za watu wenye ulemavu kwa vyombo vya sheria yani katika Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inatoa elimu kwa watoto wenye ulemavu, mpaka sasa kuna jumla ya shule tatu za

wasioona, shule kumi za viziwi, shule sita za wenye ulemavu wa akili, shule saba za wenye ulemavu wa viungo na shule sita za viziwi wasioona.

Kadhalika kuna vitengo 34 kwa ajili ya viziwi, vitengo vya 34 kwa wasioona na vitengo 147 kwa watu wenye ulemavu wa akili. Lakini vilevile suala hili litazingatiwa katika Miswada ya watu wenye ulemavu na ndiyo maana huu mkataba tumeleta kwenu Waheshimiwa Wabunge ili kuweza kuona kwamba haya yote yanakuwa inclusive na kuweza kuyasimamia vizuri baada ya kuridhia Mkataba huu. Mheshimiwa Getrude Rwakatale na Mheshimiwa Janeth Kahama wamesema watu wenye ulemavu watambuliwe mahali walipo na wanapoishi na Serikali na jamii kupata idadi ya watu wenye ulemavu katika mikoa na kuwa na Kamati husika katika Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya sensa ya watu wenye ulemavu mwaka 2008, takwimu zinaonyesha kwamba idadi ya watu wenye ulemavu ni 2,547,362, lakini vilevile nakubali kabisa wapo pengine watakuwa hawakufika kwa sababu wazazi wengine wanaficha wale watoto wenye ulemavu ambapo kiasi kwamba pengine haijawezekana. Lakini bado tutaendelea kuhakikisha tuna update data zetu na kujua kwamba walemavu ni wangapi ili kujua kwamba tunawapangia mikakati namna gani ili waweze kupata hizo huduma. Watu wenye ulemavu wapewe miradi na mikopo yenye riba nafuu katika kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miradi limezingatiwa kwenye Muswada wa Sheria ya watu wenye ulemavu. Kuhusu suala la mikopo Serikali itafanya uhamasishaji kuhusu utoaji wa mikopo kwa wananchi wote wakiwemo watu wenye ulemavu hii sasa ni *multisectral* kwa hiyo tutashirikiana na Wizara ya Afya na Wizara nyingine ambazo zinashughulika na masuala ya mikopo kuweza kuona kweli walemavu na wenyewe wanapatiwa mikopo ambayo inariba nafuu.

Mheshimiwa Zelekha, Haji aliwataka wafadhili wa maendeleo kuyaweka masuala ya walemavu katika misaada wanayoitoa kwa Tanzania. Lakini vilevile alizungumzia uundwaji wa chombo cha kitaifa cha uratibu na utekelezaji wa mikataba hii. Lakini vilevile amesema wadau wa maendeleo na sekta binafsi wayape kipaumbele masuala ya watu wenye ulemavu katika mipango ya shughuli zao. Ushauri tumeupokea kama Wizara kwa hiyo tutawasiliana na Hazina kuona namna ya utekelezaji lakini Serikali itaunda Kamati ya Utekelezaji baada ya mikataba hii na vilevile wadau wa maendeleo na sekta binafsi watashirikishwa katika utekelezaji wa sheria pamoja na haya tunayaridhia.

Mheshimiwa Sevelina Mwijage, na Mheshimiwa Shoka wamesema uboreshaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu. Serikali imepitisha Sera ya maendeleo na huduma kwa watu wenye ulemavu na itaendelea kufanya kila linalowezekana ili kuboresha maisha ya watu wenye ulemavu. Hii sera ya maendeleo ya huduma kwa watu wenye ulemavu yenyewe tukiiweza kuifikisha mpaka katika maeneo ya kule kwa wananchi basi wale wanaotoa huduma tutahakikisha kwamba wanatoa huduma kwa kuzingatia sera inavyozungumzia.

Mheshimiwa Rwakatale, Mheshimiwa Janeth Kahama, Mheshimiwa Margerth Mkanga Mheshimiwa Yono Kevela wamezungumzia kuhusu ulinzi wa kulinda watu wenye ulemavu wa ngozi hatua dhidi ya mauaji na wauzaji wa vioungo, mila potofu na ushirikina. Wote tunafahamu ni jinsi gani Serikali inavyokemea na kulifanyia kazi. Kwa hiyo, juhudi za kitaifa na za kimataifa zitaendelea kufanyika na sheria ambayo tutaileta hapa basi itazungumzia haya yote kuona ni jinsi gani hawa wahusika wanachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Ania Chaurembo, alikuwa amezungumzia kuhusu elimu kwa umma kuondoa unyanyapa; kweli kabisa tunakubali kwamba walemavu wananyanyapaliwa kwa hiyo Serikali itaunda Kamati ya utekelezaji ya Mkataba huu lakini vilevile Sheria italizingatia hili. Mheshimiwa Shoka alisema kwamba kusaidia wenye ulemavu isiwe kama hisani. Bali iwe ni lazima. Ni kweli kabisa ndiyo maana tumelete azimio hili tuweze kuliridhia na Sheria ambayo itahakikisha kwamba huu mkataba wa nyongeza ndiyo ule ambao sasa utakuwa unalizingatia hili. Kwamba lazima huduma zao zipatikane na ndiyo maana sisi kama Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tumesema kutakuwa na bajeti badala ya kutoa ruzuku. Kwa hiyo mkataba huu utakuwa umezingatiwa.

Mheshimiwa Susan Lyimo amesema kwamba kuzalilisha walemavu hasa wakati wa uzazi, lugha za kejeli wanapokuwa wanajifungua. Watu wenye ulemavu wana haki ya kuzaa na kufaidi mahitaji yao ya kimwili kama watu wengine. kwa maana hiyo mlemavu kupata ujauzito wala si kitu cha ajabu kwa sababu na yeye kama mlemavu akizaa mtoto tena itakuwa ni vizuri kwa sababu atamsaidia jinsi ya kuishi vizuri.

Lakini niseme tu lugha za kejeli si kwa walemavu tu katika vituo vya kutolea huduma. Kwa maana hiyo Serikali inaendelea kukemea kwa wale wote wanaotoa lugha chafu katika vituo vya kutolea huduma, si kwa walemavu tu lakini unapokuwa unatoa huduma kwa mtu yoyote anayefika kupata huduma hauruhusiwi kikanuni kutoa lugha yoyote ile ya kejeli. Hivyo basi sisi kama Wizara ya Afya kama wasimamizi wakuu wa sera tutahakikisha kwamba wale wote tunaomba tushirikiane na Halmashauri zetu kwa sababu wanawajua waache mara moja na hatua ziendelee kuchukuliwa kwa wale wote watakaokuwa wanatoa lugha za kejeli. Lakini vilevile tutawaomba na hawa wenzetu au wawe walemavu na wale wengine watusaidie basi kutuletea hizi taarisa hasa wanapoona kwamba suala hili linakuwa tatizo kule sisi hatutasita kuwashukulia hatua.

Mheshimiwa Fatma Mikidadi ametoa pengizi kwa viongozi awamu zote nne kwa kujali walemavu na taasisi mbalimbali lakini hii pia waheshimiwa wote wamezungumzia na kuwapongeza watu binafsi na watu wenye taasisi mbalimbali na NGO's na kadhalika kwa kutoa misaada kwa watu wenye ulemavu. Lakini vilevile kulaani wale wanaopokea misaada ya watu wenye ulemavu na kuitumia nafikiri Mheshimiwa Beatrice Shellukindo amelizungumzia hilo na umuhimu wa kuwatambua walemavu ili waweze kwenda shule nadhani haya tuliyazungumza mwanzo kwa hiyo ushauri huu tunauchukua na tunendelea kusisitiza kwamba mtu yoyote mwenye ulemavu kusoma ni haki kama ilivyo kwa mtu mwingine kwa hiyo anatakiwa asome na wale ambao wanatumia walemavu kama chambo cha kuweza kupatia fedha zao binafsi waache mara moja.

Mheshimiwa Mchemba, alizungumzia kuhusu kambi ya kutunza walemavu makazi yake ni mabovu ametaja Ipuli kule Tabora, lakini ametaja katika shule za mwanzoni na kadhalika. Hili limekuwa likizungumzwa sana hapa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu makambi. Lakini Wizara ya Afya inamkakati mkubwa kuweza kuhakikisha kwanza tunataka makambi yote Tanzania nzima ili tuweze kuyaona tuangalie tunawalemavu wangapi ambayo wanakaa katika makambi yale na kama ni lazima kuwa na kambi yote yawe mengi au tuweze kuyafanya ni machache watu waweze kuwekwa. Kwa hiyo, hilo Wazira inalifanyia kazi kuweza kuona na hii itaongeza tija jinsi ya kuwatubu badala ya kuwahudumia badala ya kuwa Tabora, Manyara, Singida na mikoa mingine nadhani hii tukifanya sasa naona mtuachie ili sisi tufanye huu utafiti wetu tuweze kuona kwamba haya makambi ya walemavu ni vipi tutayafanya ili yaweze kutoa tija kwa wale watu wanahudumiwa. Nakubali kabisa kwamba hali ni mbaya lakini tunaendelea wakati tukifanya hiyo *research* tunaendelea kuyafanyia ukarabati kwa kadri fedha itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii lakini nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao hiyo itatuboreshea sana Muswada wetu naomba kusema kwamba naomba kuunga mkono hoj ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Dr. Aisha Kigoda. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri Wa Afya na Ustawi wa Jamii Prof. David Mwakyusa.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru meza yako kwa kunipa nafasi hii kwa mara nyingine ili niweze kuhitimisha hoja yangu ambayo niliwasilisha hapa Bungeni jana. Nimefarijika sana kuona Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia hoja hii na nimefarijika kwamba wote wameunga mkono ikiwemo Kambi ya Upinzani.

Aidha, nitakuwa mnyimi wa fadhila ikiwa sitashukuru makundi mbalimbali ya watu wenye ulemavu ambayo yamejitokeza kwa wingi hapa kuanzia jana nilipowasilisha hoja hii ya maazimio haya mawili. Leo tunaona wengi zaidi wamekuja niseme tu kwamba wananipa nguvu kwa *sababu* hapo nitakapoleta Sheria Wabunge wengi watajua kwamba ninawadau wengi. *(Makofi)*

Maazimio haya yamevutiaq jumla ya wachangiaji 27, kati yao 10 wamechangia kwa kuzungumza na wachangiaji 17 walichangia kwa maandishi. Angalizo tu ni kwamba kati ya hawa 27 wanaume ni wanane na 19 ni wanawake. Tafsiri yake siijui lakini inaelekea kwamba wanawake wanamoyo wa huruma zaidi kwa kundi hili na nawashukuru waendelee na moyo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo desturi naomba niwatambue waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni kama ifuatavyo. Mheshimiwa Dr. Haji Mwmita Haji, akizungumza kwa niaba ya Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Zulekha Yunus, Haji, Mheshimiwa Bujiku

Sakila, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo na Mheshimiwa Dr. Aisha Omar Kigoda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia kwa maandishi kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Zelekha Yunus Haji, Mheshimiwa Janeth Bina Kahama, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Daina Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Shoka, Khamis Juma, Mheshimiwa Susan Anselim Lyimo, Mheshimiwa Getrude Rwakatale, Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi. Naomba niwashukuru wote kwa michango yenu na karibu utakuta yote yalikuwa yanazungumzia hay ohayo na niahidi tu kwamba yote yatachukuliwa katika Sheria kufuatia jinsi tutakavyoileta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamesema kwamba Mkataba huu wameusubiri kwa muda mrefu na mimi nakiri kwamba kwa muda mrefu toka ulipotishwa New York mwaka 2007, lakini tulitia saini awamu ya kwanza halafu tummemshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutia sainiu mkataba wa nyongeza mwezi Septemba mwaka jana.

Namshukuru Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba mikataba hii imeletwa hapa Bungeni kwa hati ya dharura ni kwa sababu wote tuliona umuhimu na taratibu za kupita mpaka ifike hapa ilipokuwa ndefu wakaruhusu kwamba ije hapa mapema kabla ya taratibu zingine kwisha. Niwakumbushe, Wabunge wenzangu kwamba katika kuridhia mikataba hii Serikali imejiwekea commitment fulani. Kwamba inaungana na wananchi wanachama kuwatambua watu wenye ulemavu kama ni sehemu muhimu katika jamii. Kwamba tunawajali, tunawapenda na kwa maana hiyo wanastahili kupata haki na kupewa fursa sawa na watu wasio na ulemavu.

Suala la bajeti limejitokeza na hata jana wakati wa mawasilisho yangu nililizungumzia kwamba tutakapokuwa na Sheria itabidi shughuli zinazohusu ustawi wa watu wenye ulemavu ziwekwe wazi na kwa mujibu wa taratibu za Serikali Bajeti inafuata shughuli na kwamba isiwe hisani. Kwa maana hiyo basi bajeti itakuwa wazi na kwa malengo ambayo yameainishwa nini tunataka kuwafanyia hawa wenzetu.

Niwatoe wasiwasi hasa Mheshimiwa Shellukindo ambaye anafikiri kwa mawazo yake ustawi wa jamii pale ilipo labda si sawa. Lakini mimi nasema kwa upande wa bajeti hata ikienda miundombinu, ikienda elimu au mahali popote, tutambue nini tunataka kuwafanyia na zitolewe pesa ambazo zitasimamiwa vizuri zipewe tija kwa ustawi wa hawa wenzetu wenye ulemavu na hizi fedha zitakaguliwa kwa utaratibu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushe vilevile wengi wamesema Serikali ilenge zaidi katika kuwawezesha badala ya kutoa ruzuku hiyo tunakubaliana nayo, na katika

Sheria ambayo iko katika hatua nzuri ni kwamba kutakuwa na pendekezo kwamba kuwe na mfuko wa watu wenye ulemavu na hii itasaidia pale watu wanakuja NGO pesa zinatolewa wala huwezi kujua nani kapewa nani katoa, lakini tukiwa na mfuko utakwenda kuhudumia na mipango ambayo inaendana na mipango ya Serikali.

Pia nazidi kukumbusha ustawi wa watu wenye ulemavu ni jukumu la kila mtanzania. Tumekumbushwa vilevile kwamba wasio na ulemavu sasa ni walemavu watarajiwa. Kwa hiyo, elimu isambazwe tena kwa nguvu ili kuongeza uelewa kwa wananchi na kumekuwa na mifano hapa walemavu wengine kwenye maeneo mengine hakuna walemavu unajiuliza wanakwenda wapo, hilo ni tatizo ambalo wote tunalijua lakini vilevile elimu ya kuzuia ulemavu. Kama maeneo ambayo tunaweza tukazuia nadhani itakuwa vizuri tufanye hivyo ili kupunguza idadi. Pia tumeahidi katika Sheria kutakuwa na chombo cha ndani cha kuratibu na kutathimini utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *session* ya pili ya mkataba huu ni ule wa nyongeza kiingereza wanaita *optional protocol* ambayo inamaana ni hiari na hii ndiyo kidogo imecheleweshа Muswada kuletwa hapa. Kwa sababu *optional* inamaana nchi inayoridhia ina uhuru wa kukubali hii sehemu au kutokubali. Kwa sababu hii inabana zaidi.

Sehemu hii ni katika kudumisha demokrasia na uwazi kwa sababu umoja wa Mataifa Umeunda Kamati ya kuruhusu uundwaji wa Kamati ya Kimataifa kuweza kuhoji na kuchunguza malalamiko na watu ambao wanaona wameathirika katika nchi fulani baada ya taratibu zote kushindikana ambayo imeridhia; basi malalamiko yakiifikia hii Kamati inapewa uwezo wa kuweza kuihoji nchi, kutafuta maelezo hata ikibidi kutuma wataalam wake kuja kuchunguza. Sasa yote haya katika Mikataba hii miwili ni kwamba haina nguvu ya kisheria ndiyo maana kumekuwa na haja ya kutunga Sheria.

Wengi wamezungumzia nyumba zetu zinavyojengwa maghorofa, barabara na maeneo ambayo wenzetu wenye ulemavu hawawezi kuyatumia kwa fursa sawa kama sisi wengine. Kwa mfano, wajenzi kupitia vyama vyao, tumewaandikia kama wakala kuwaomba waangalie maeneo lolote lile wanalofanya wajue kuna watu wenye ulemavu. Kwa hiyo wajue kwamba katika jamii kuna watu wenye ulemavu. Lakini hii mikataba kama nilivyosema haina nguvu ya kisheria, lakini sheria itakapotungwa mambo kama haya itabidi yawekwe ili mtu ambaye hatekelezi basi anavunja sheria. Kwa wakati huu hawajavunja sheria kwa sababu hakuna sheria yoyote.

Mheshimiwa Naibu Waziri ametueleza na nisisitize kwamba sheria ipo katika maandalizi na imefika hatua nzuri na nia yetu ni kwamba katika Bunge la mwezi Oktoba tuilete hapa na ili kupunguza majadiliano maudhui mengi yaliyotokana na michango tutayawekwa kwenye sheria na naimani kwamba hii michango imetusafishia ili tuwe na sheria ambayo inafikra na mawazo na michango na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo machache niliyokuwa nayo ya kusema, nishukuru na kama nilivyosema jana, wachangiaji wengi wamekuwa wakizungumza habari za walemavu, nadhani ni mazoea, lakini tujaribu kuzoea kuwaita watu wenye ulemavu. Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Nyongeza wa Kimataifa kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu (The Optional Protocol to Convention on the Rights of the Persons with Disabilities) lilipitishwa na Bunge)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Bima wa Mwaka 2009
***(The Insurance Act, 2009)***

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Bima *(The Insurance Act, 2009)* sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Dr. Abdallah Omary Kigoda, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri wakati Kamati ilipokutana mjini Dodoma kwa muda wa siku mbili, tarehe 22 na 23/4/09. Nawashukuru pia wadau na wataalamu wote walioshiriki na kutoa michango yao iliyofanikisha Muswada huu.

Napenda niwatambue wadau hao kama ifuatavyo:- Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha na Uchumi – Zanzibar, Umoja wa Makampuni ya Bima Tanzania, Umoja wa Madalali wa Bima, Umoja wa Mawakala wa Bima, Benki Kuu ya Tanzania na Taasisi ya Bima. Napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba, tumezingatia michango ya Kamati ya Fedha na Uchumi na ile iliyotolewa na Wadau mbalimbali wa sekta ya bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Muswada huu yanatokana na mabadiliko yanayoikabili sekta ya bima duniani kote. Kama tunavyofahamu, Sheria ya Bima inayotumika hivi sasa ilipitishwa na Bunge na kuanza kutumika zaidi ya miaka kumi iliyopita. Sheria hii imeonekana kutokidhi matakwa ya mabadiliko ya sasa.

Hivyo basi, Muswada huu unapendekeza kutunga sheria mpya ya Bima ambayo inafuta sheria ya sasa ya Bima ya mwaka 1996 Sura 394. Sheria hii mpya itawezesha sekta ya bima nchini kufanya shughuli zake kwa ufanisi na kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika Kimataifa.

Sheria mpya itazingatia mabadiliko yaliyojitokeza na kuondoa upungufu wote uliobainika katika sheria ya sasa. Upungufu huo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kupungua kwa thamani ya viwango vya mitaji ya kuanzisha Makampuni ya Bima na viwango vya ukwasi kutokana na kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania;

(ii) Baadhi ya vifungu vya sheria kutokidhi viwango vya kimataifa kuhusu utaratibu na usimamizi wa soko la bima kama ilivyoainishwa na Taasisi ya Kimataifa iitwayo *International Association of Insurance Supervisors*;

(iii) Ukosefu wa mfumo wa kushughulikia rufaa za makampuni ya bima, madalali na mawakala wa bima wasioridhishwa na maamuzi ya Kamishna wa Bima;

(iv) Bodi ya Taifa ya Bima kutokuwa na mamlaka ya kutosha kusimamia Idara ya Bima na kushauri katika masuala ya kisera na utendaji wa soko la Bima;

(v) Ukosefu wa mfumo wa kushughulikia malalamiko ya wateja wa bima wasioridhishwa na maamuzi ya Makampuni ya Bima kuhusu malipo ya madai yao ya Bima;

(vi) Sheria kutobainisha dhana ya uwajibikaji wa makampuni ya bima hususan ulipaji wa madai na muda maalumu kwa wateja wa bima kulipia ada ya bima hivyo kuathiri ufanisi wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu huo, Sheria inayopendekezwa itaiwezesha sekta ya Bima kusimamiwa ipasavyo kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya usimamizi wa soko la bima na hivyo kuchangia kasi ya ukuaji wa uchumi wa Taifa. M ambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuundwa kwa chombo cha kushughulikia malalamiko ya madai ya Wateja wa Bima ili kurejesha imani ya wananchi katika biashara ya bima hapa nchini;

(ii) Kuanzishwa Baraza la Rufaa, chombo ambacho kitakuwa cha kusikiliza rufaa za makampuni ya bima, madalali na mawakala dhidi ya maamuzi ya Kamishna wa Bima. Kwa sasa malalamiko dhidi ya uamuzi wa Kamishna wa Bima huwasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha au Mahakamani. Chombo hiki hakitakuwa cha kudumu bali kitatakiwa kukaa pale tu migogoro itakapojitokeza;

(iii) Kuipa nguvu zaidi kiutendaji na udhibiti Idara ya Bima kwa kuifanya kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Masuala ya Bima na hivyo kujenga imani kwa wadau wote wa sekta ya bima nchini kuhusu uimara wa usimamizi wa soko;

(iv) Kuimarisha Bodi ya Taifa ya Bima kwa kuipa mamlaka zaidi ya kufanya maamuzi na kusimamia soko la bima nchini;

(v) Kumpa mamlaka Kamishna wa Bima ya kufanya ukaguzi katika makampuni ya bima ili kuimarisha udhibiti wa masuala ya bima na hivyo kuzuia kuporomoka kwa sekta ya bima;

(vi) Kurekebisha viwango vya mitaji ya uanzishwaji wa makampuni, madalali na mawakala wa bima ili thamani ya mitaji yao iendane na kushuka au kupanda kwa thamani ya shilingi;

(vii) Kutenganisha biashara ya bima za maisha na bima za mali na ajali ili kukidhi viwango vya kimataifa;

(viii) Kuimarisha viwango vya ukwasi ili kuyapa uwezo makampuni ya bima kulipa madai ya wateja wao haraka na kwa usahihi zaidi;

(ix) Kuweka utaratibu wa kutangaza kwa umma taarifa za fedha za makampuni ya bima ili kuendana na dhana ya utawala bora tofauti na ilivyo sasa;

(x) Kuimarisha uwekezaji wa mali za makampuni ya bima ili kumlinda mkata bima;

(xi) Kupunguza muda wa mwisho wa kulipa madai ya wateja wa bima kutoka siku sitini za sasa hadi siku arobaini na tano ili kuongeza uwajibikaji kwa watendaji wa sekta ya bima na hivyo kuleta ufanisi; na

(xii) Kulegeza masharti ya kujiandikisha uwakala wa bima ili kuweka mazingira mazuri yenye lengo la kurahisisha kuanzishwa kwa bima za watu wa kipato cha chini kama vile wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo wadogo na pia wanachama wa bima za matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu kumi na mbili:- Sehemu ya Kwanza yenye Kifungu cha 1 – 3 inahusu utangulizi, kama vile jina la Sheria, tarehe ya kuanza kutumika na tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika katika sheria.

Sehemu ya Pili, inahusu Kifungu 4 – 14 ambavyo vinapendekeza kuanzishwa kwa Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa shughuli za bima, kazi zake, uteuzi wa Kamishna na Naibu Kamishna wa Bima, Uanzishwaji wa Bodi ya Taifa ya Bima na kazi zake. Aidha Kifungu cha 13 kimefanyiwa marekebisho ili kurahisisha na kuweka uwiano katika uteuzi wa wajumbe wa Bodi.

Sehemu ya Tatu ya Muswada huu inahusu Kifungu cha 15 – 51 ambavyo vinapendekeza usajili wa Biashara ya Bima kwa ujumla. Kurekebisha viwango vya mitaji ya uanzishwaji wa Makampuni ya Bima, thamani ya mitaji kuendana na kushuka au kupanda kwa thamani ya Shilingi na kuimarisha viwango vya ukwasi. Kumpa

mamlaka Kamishna wa Bima kufanya ukaguzi katika makampuni, kutangaza taarifa za fedha za makampuni ya Bima na kuanzisha Kamati za ukaguzi wa fedha na zile za uwekezaji. Aidha, Kifungu cha 40(4) na (5) kimefanyiwa marekekebisho kwa kuzingatia maoni ya Wadau na utaratibu wa Mwenyekiti na Mkurugenzi kuweka saini kwenye taarifa za Fedha inapendekezwa ufanywe kwa kipindi cha nusu mwaka badala ya robo mwaka.

Sehemu ya Nne inahusu Kifungu 52 – 57 ambavyo vinapendekeza kuwepo kwa umoja wa kitaaluma wa makampuni ya Bima *(Association)* na Mamlaka ya Kamishna katika kusajili umoja huo. Aidha, sehemu hii inapendekeza kuwepo kwa mahesabu yaliyokaguliwa kwa kila kampuni inayounda umoja huo.

Sehemu ya Tano ya Muswada huu inahusu Kifungu cha 58 – 60 ambavyo vinapendekeza kuwepo kwa masharti ya haki kwa mtu wa tatu *(third party)* dhidi ya Kampuni ya Bima wakati imefilisika, haki ya mwenye Kampuni kutoa taarifa kamili kwa mwathirika na jinsi madai yake yatakavyopatiwa ufumbuzi hata baada ya Kampuni husika kufilisika.

Sehemu ya sita inahusu Kifungu cha 61 – 78 ambavyo vinapendekeza masuala ya usajili wa madalali na mawakala wa Bima. Sehemu hii pia inapendekeza kuwepo kwa mitaji kwa Madalali na Mawakala wa Bima, mamlaka ya kukagua mitaji hiyo na pia uhalali wa kufutiwa usajili kwa madalali na wakala wa Bima. Aidha sehemu hii inaainisha utaratibu wa kuweka wazi Hati ya kufanyia shughuli za Bima.

Sehemu ya Saba yenye Kifungu cha 79 – 84 inapendekeza kuwepo Bima Mtawanyo kati ya makampuni ya bima yaliyosajiliwa Tanzania na Mashirika ya Kimataifa ya Bima mtawanyo ambayo Serikali ya Tanzania imewekeza. Pia sehemu hii inaainisha adhabu kwa makampuni yatakayokaidi kuwasilisha viwango vya ada ya bima kwa mashirika hayo.

Sehemu ya Nane ya Muswada huu inahusu Kifungu cha 85 – 121 ambavyo vinaweka masharti ya biashara ya bima ya maisha.

Sehemu ya Tisa ya Muswada huu inahusu Kifungu cha 122 – 126 ambavyo vinapendekeza kuundwa kwa chombo cha kushughulikia malalamiko ya madai ya wateja wa Bima, kuanzishwa kwa Baraza la Rufaa ambalo litakuwa ndicho chombo cha kusikiliza Rufaa za Makampuni ya Bima, madalali na mawakala dhidi ya maamuzi ya Kamishna wa Bima.

Sehemu ya Kumi inahusu Kifungu cha 127 – 129 ambavyo vinapendekeza vyanzo vya fedha za Mamlaka ya Usimamizi wa Bima pamoja na utaratibu wa kutayarisha ripoti ya fedha na kuiwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana ndani ya muda uliopangwa.

Sehemu ya Kumi na Moja inahusu Kifungu cha 130 – 159 ambavyo vinapendekeza masharti ya ujumla kama vile malipo ya madai kwa waathirika wa ajali,

muda wa kulipa madai, muda wa kuwasilisha malipo kutoka kwa madalali kwenda kwa Makampuni ya Bima na maadili ya kazi kwa madalali.

Sehemu ya Kumi na Mbili na ya mwisho inahusu Kifungu cha 160 – 168 ambavyo vinapendekeza adhabu kuhusu makosa mbalimbali yanayoweza kutokea chini ya Sheria inayopendekezwa, kumpa Kamishna wa bima mamlaka zaidi ya udhibiti wa soko na pia kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana kutunga Kanuni mbalimbali chini ya sheria inayopendekezwa. Aidha sehemu hii inapendekeza kufutwa kwa Sheria ya sasa ya Bima Sura 394.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba muujadili Muswada ulio mbele yenu na baadaye Bunge liweze kuupitisha kuwa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwasilisha maelezo yako kuhusu Muswada husika ambao uko katika Order Paper ya leo. Muswada huu wa Serikali ni Muswada wa Sheria ya Bima wa mwaka 2009 *(The Insurance Finance Hill, 2009)*. Muswada umewasilishwa hapo na umeungwa mkono.

Sasa kwa taratibu zetu anayetakiwa kufuata hapa ni Msemaji wa Kamati iliyochambua Muswada huu na Msemaji huyo huwa anapewa nusu saa. Baadaye anafuata Msemaji wa Upinzani, nusu saa na utaratibu mwingine wote kuendelea.

Kwa vile muda uliobaki hautoshi kikanuni kwa ajili ya Kamati husika iliyochambua Muswada huu, basi kwa nafasi hii naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 Jioni ya leo Ambato tutaendelea na hatua nyingine za Muswada huu.Naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.45 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti ( Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, naomba niwape taarifa ambayo imetufikia muda mfupi uliopita, nayo ni taarifa ya kifo.

Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Bunge inasikitika kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kwamba aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi - Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye, amefariki dunia kwa ajali ya gari saa 12.00 asubuhi katika *Bus* la *RM Investment* lililokuwa likisafiri kutoka Bukoba kuelekea Dar es Salaam. Ajali hiyo imetokea katika eneo la Berega Mkoa wa Morogoro.

Mwili wa Marehemu umehifadhiwa katika hospitali ya Misheni ya Berega Mkoani Morogoro hivi sasa. Taratibu za mazishi zinaendelea kupangwa na familia ya Marehemu, Waheshimiwa Wabunge watajulishwa pindi zitakapokamilika. Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amina.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Bima wa Mwaka 2009
***(The Insurance Bill, 2009)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. ANDREW J. CHENGE K.n.y MHE. ABDALLAH O. KIGODA-MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi Mbele ya Bunge lako Tukufu baada ya kukamilisha kazi ya kuchambua Muswada wa Sheria ya Bima *(The Insurance Act, 2009).* Kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge Na. 86(5) Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikiri kwa niaba ya Kamati kwamba muda uliokuwepo wa kuwezesha Kamati kuchambua Muswada ulikuwa ni mfupi.

Hata hivyo, pamoja na muda kuwa finyu, Kamati imeweza kuchambua Muswada wa Sheria ya Bima, 2009 *(The Insurance Act 2009).* Kamati imekutana hapa Mjini Dodoma kwa siku mbili tarehe 22 na 23, Aprili, 2009. Katika Vikao hivyo, Wajumbe wa Kamati pamoja na Wadau wamejadili Muswada huo kwa makini na kubaini kwamba Muswada umezingatia mambo mengi muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhika kwamba Muswada huu utahakikisha kuwa soko la Bima hapa nchini linaboreshwa kwa ajili ya kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo muhimu yaliyojitokeza na kujadiliwa na Kamati; ni pamoja na ushiriki wa wadau katika mchakato wa kuandaa na kuchambua Muswada. Suala la ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika mchakato wa kuandaa na kuchambua Muswada huu lilijitokeza. Wadau waliofika mbele ya Kamati wameeleza kuridhishwa kwao na jinsi walivyoshirikishwa katika mchakato mzima wa utayarishaji wa Muswada huu. Kamati inaipongeza kwa dhati Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kuwashirikisha wadau wote muhimu katika mchakato wa kuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo na maudhui ya Muswada; Kamati imejadili malengo na Maudhui ya Muswada huu. Kimsingi Kamati inakubaliana kabisa na maudhui ya Muswada huu, ambapo madhumuni makubwa ya Muswada huu ni kutunga sheria mpya ya Bima ya mwaka 2009 inayokidhi mahitaji na matarajio ya soko ya Bima nchini kwa wakati huo na kufuta sheria ya sasa ya Bima ya Mwaka 1996 Sura, 394. Muswada huu umezingatia mapungufu yote yaliyobainika katika sheria ya Bima ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapungufu makubwa yaliyopo katika sheria iliyopo sasa ambayo ni kero kubwa kwa wananchi ni pamoja na wakata Bima kutolipwa kwa wakati Bima zao zinapoiva, utaratibu mrefu wa kupata malipo ambao hautekelezeki kirahisi pamoja na mapungufu mengine kadhaa wa kadhaa. Kutokana na kupitwa na wakati kwa sheria ya Bima ya sasa, Kamati inaunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuleta Muswada huu ili Muswada huu ukikubaliwa na Bunge lako Tukufu, sheria iweze kukidhi matarajio ya wateja wa bima na wananchi kwa ujumla, pamoja na kulinda na kudhibiti soko la Bima hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa chombo cha kushughulikia malalamiko ya madai ya wateja wa bima; suala la uanzishwaji wa Chombo cha kushughulikia malalamiko ya madai ya wateja wa Bima lilijadiliwa kwa kina na Kamati yangu.

Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Muswada ya kuwa na Chombo cha kushughulikia Malalamiko ya Wateja wa bima ili kurejesha imani ya wananchi katika biashara ya bima hapa nchini. Kamati yangu inaiomba Serikali kuweka kipaumbele katika utendaji kazi wa chombo hiki pindi chombo hicho kitakapoundwa.

Aidha, ni matumaini ya Kamati yangu kwamba Chombo hicho kitaweka utaratibu ambao utamhakikishia mkata bima kupata haki yake kwa urahisi kwa lengo la kuboresha maisha yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzisha baraza la rufaa la Bima (*The Insurance Appeals Tribunal)*; eneo lingine ambalo lilijadiliwa kwa kirefu na Kamati yangu ni lile la kuanzisha Baraza la Rufaa la Bima (*The Insurance Appeals Tribunal*).

Baraza hilo litakuwa linasikiliza rufaa zitakazowasilishwa mbele ya Baraza hilo na makampuni ya bima, madalali na mawakala wa Bima dhidi ya maamuzi ya Kamishna wa Bima, ambazo kwa sasa huwasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha. Ni Matumaini ya Kamati yangu kwamba Baraza la Rufaa la Bima litafanya kazi nzuri na kutoa tija katika kusikiliza malalamiko yatakayoletwa mbele yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuanzishwa kwa vyombo hivyo muhimu ni maoni ya Kamati hii kwamba uamuzi wa Serikali ya kuipa nguvu zaidi kiutendaji na udhibiti Idara ya Usimamizi wa Bima (*Insurance Supervisory Department)* kwa kuifanya kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa masuala ya Bima *(Tanzania Insurance Regulatory*) ni jambo muhimu sana.

Aidha Kamati inapendekeza kuwa Serikali ione umuhimu wa kuimarisha Bodi ya Taifa ya Bima kwa kuipa mamlaka zaidi ya kufanya maamuzi na kusimamia soko la bima nchini. Kumpa mamlaka Kamishna wa Bima kufanya ukaguzi katika makampuni ya bima ili kuimarisha udhibiti wa masuala ya bima na hivyo kuzuia uwezekano wa kuporomoka kwa sekta ya bima nchini nalo ni suala muhimu sana ambalo Kamati inaliafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utungaji wa kanuni *(regulations)* suala lingine lililojadiliwa na Kamati yangu ni pamoja na umuhimu wa utungaji wa Kanuni za kutekeleza Muswada wa Sheria unaopendekezwa unaotekelezwa kwa ufanisi.

Kamati ilibaini kwamba utungaji wa kanuni ni muhimu sana katika kutekelezwa sheria kikamilifu. Hivyo, Wajumbe walikubaliana kwamba ni lazima kanuni zitungwe, mapema iwezekanavyo kwani kuna maeneo mbalimbali ambayo Kamati ilibainisha ambayo yanahitaji kanuni kutungwa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa bodi ya Bima ya Taifa; suala lingine lililojadiliwa kwa kina ni kuhusu wajumbe wa Bodi ya Bima ya Taifa. Kamati ilijadili suala la wajumbe wa bodi ili uteuzi uzingatie sura ya Muungano.

Kamati imeridhishwa na marekebisho ya jedwali yaliyofanywa na Serikali ambayo yamezingatia suala hilo. Ni maoni ya Kamati pia kwamba suala la uwiano wa jinsia nalo litazingatiwa katika utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya kuwawezesha watanzania katika kuendesha biashara ya bima; suala lingine ambalo lilijadiliwa kwa kina na Kamati ni kuhusu kuwawezesha watanzania kuendesha biashara ya bima nchini. Watanzania wengi wamekuwa hawajihusishi kikamilifu katika biashara hii ya bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, Kamati imeridhishwa na mapendekezo ya Muswada huu kwa sababu Muswada una vifungu kadhaa ambavyo vinaweka utaratibu wa kuwawezesha Watanzania kushiriki katika biashara ya bima. Kwa mfano kifungu 16(1) kimeweka sharti kwamba hakuna kampuni yoyote ya bima itakayosajiliwa hapa nchini ambayo theluthi moja ya hisa zake haiko mikononi mwa watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, kifungu hicho cha Muswada vilevile kinaweka sharti kwamba bodi za makampuni yote ya bima nchini theluthi moja ya wajumbe wa bodi hizo lazima wawe Watanzania Kamati inaipongeza serikali kwa hatua hizi za makusudi ilizozichukua kwa kuwapa upendeleo wa pekee watanzania ili washiriki katika soko na biashara ya bima nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani, naomba kuchukua fursa hii kwa niaba ya Kamati ya Fedha na Uchumi kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari na Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara yake kwa ushirikiano wao mkubwa waliotupa wakati Kamati hii ikifikiria Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nawapongeza wataalam wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali na wataalam wake kwa ushirikiano wao katika kufanikisha kazi hii.

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati kabisa wadau wote walioshiriki katika mchakato wa kujadili Muswada huo. Kwa kiasi kikubwa Kamati yangu imetumia maoni na ushauri walioutoa katika kufanikisha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa namna ya pekee kumshukuru Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda - Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha - Makamu Mwenyekiti, kwa kuendesha vikao vya Kamati kwa ufanisi mkubwa. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati Ndugu Anselm Mrema na Ndugu Lawrence Robert Makigi kwa kuihudumia Kamati kwa makini na ufanisi mkubwa ikiwa ni pamoja na kushiriki katika maandalizi ya taarifa hii.

Kwa heshima, sasa naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi walioshiriki kuchambua Muswada wa sheria ya Bima 2009 *(The Insurance Act 2009*) kwa kuwataja majina:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda - Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamza Mwenigoha - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Benilith Mahenge, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Maulidah Anna Komu, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Danas Nakei, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Dr. Omary Mzeru Nibuka na Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Fatma Abdulhab Fereji, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Mossy Mussa, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba na Mheshimiwa Richard Ndassa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba kukushukuru wewe binafsi, Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wenzako wa Bunge na Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah kwa ushirikiano wenu mnaotupa katika kutekeleza shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile hii ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu tangu nipate mitihani mbalimbali ambayo Mwenyezi Mungu ameniletea, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa ujumla ambao kwa njia moja au nyingine wameniletea salamu za pole na kunitakia kheri, mimi yote hayo nayachukua maana ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

Pia nichukue nafasi hii kwa moyo mzito sana kutoa salamu zangu za rambi rambi kwa taarifa ya msiba mzito ambayo tumeipata sasa hivi ya aliyekuwa Mbunge Mwenzetu

Mheshimiwa Phares Kabuye, Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya napenda kuiwasilisha taarifa hii kwa kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Tunakushukuru sana Mheshimiwa Andrew Chenge ambaye umekuwa Msemaji wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa yale uliyoyawasilisha na sisi tupo pamoja na nawe kwa yale majaribu makubwa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, na atakapomaliza Msemaji wa upinzani atakayekuwa msemaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa ili aweze kujiandaa.

**MHE. HALIMA J. MDEE K.n.y MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED- KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI NA MSEMAJI MKUU WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Bima wa mwaka 2009 *(The Insurance Act,2009).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kusema kwa uchache maoni ya Kambi ya Upinzani, ningependa kwa masikitiko makubwa kuipa pole familia ya Mheshimiwa Kabuye kwa msiba mkubwa uliowapata, kwa ufupi ni kwamba tupo pamoja na ninyi japokuwa tupo mbali leo hii tukiwa Dodoma lakini tunaamini utapatikana uwakilishi mahususi kwa ajili ya kuhudhuria msiba husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu, kwa kuwa mzima, mwenye afya njema na kwa kusimama mbele ya Bunge hili ili kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Bima wa mwaka 2009, kwa mujibu wa kanuni za Bunge, kanuni ya 86(6) Toleo la mwaka 2007.

Kambi ya Upinzani inatambua umuhimu wa Muswada huu ambao kama ukitekelezwa kikamilifu na wananchi kueleweshwa juu ya umuhimu wa Bima utasaidia kwa kiasi kikubwa kuwafanya watanzania waepukana na umaskini wa ghafla unaoletwa na majanga mbali mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kama ilivyoainishwa na Muswada husika, Muswada huu una malengo ya kufuta sheria ya Bima sura ya 394 ambayo kimsingi ilikuwa imepitwa na wakati kwa malengo ya kutunga sheria mpya ya Bima ya mwaka 2009.

Kwa kutambua mapungufu yaliyojitokeza siku za nyuma,sheria hii mpya inakusudia kuanzisha mamlaka ya usimamizi wa shughuli za Bima, kama ilivyoainishwa na vifungu 5(1) na (2) na 6(1) na (2) . Lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa shughuli za Bima zinaendeshwa kwa ufanisi ,uhalali ,usalama na kuhakikisha kuwa uhusiano kati ya makampuni ya Bima ,madalali na mawakala unasimamiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kwamba uwepo wa mamlaka hii utasaidia kwa kiasi kikubwa kuweka nidhamu katika shirika letu 'mfu' la Bima , ambalo liko katika mchakato wa 'kufufuliwa' ili kuweza kudhibiti kuendelea kuporomoka kwa mtaji wake wa kufanyia kazi ambao kwa miaka minne iliyopita umekuwa ukishuka kutoka salio kiasi cha salio hasi la shilingi za kitanzania Bilioni 31.1 hadi kufikia salio hasi bilioni 58.7. Katika kipindi hiki uwiano wa mali na madeni *(current ration*) ulionyesha kuwa wastani shirika lilikuwa na uwezo wa kulipa shilingi 15 kwa kila deni la Sh.100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu kwa ujumla umechelewa kuletwa kwani kutokana na jinsi taslia nzima ya Bima *(Insurance Industry)* inavyofanyakazi ni wazi kwa njia moja au nyingine tulitarajia kuwa sheria kama hii ingeishaletwa zamani jambo ambalo lingehamasisha watanzania wengi kuwemo katika taslia hii ya Bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokana na ukweli kwamba Muswada huu unawalinda watanzania ambao wamo katika biashara hii ya Bima. Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa wazawa/watanzania wengi ili wavutiwe kuingia kwa kuwezeshwa zaidi kielimu kwani bila kuielewa vizuri biashara ya Bima si rahisi kuingia na kufanya biashara. Aidha sambamba na hilo wazawa wapatiwe mitaji ya kuwawezesha kuwa *"active participants in insurance industry"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu wa Bima kwa unalenga kuinua watanzania, hivyo basi itakuwa si haki kwa watanzania pale ambapo Shirika la Bima la Taifa ambalo ni asasi ya Watanzania kwa asilimia mia moja likiwa linachechemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Serikali kufanya jitihada za maksudi ili kuliboresha kwa kuweka mtaji wa kutosha na kulipa madeni yake yote, kwa njia hii tuna uhakika shirika hili litakuwa shindani katika soko zima la bima na litajiendesha kibiashara zaidi kutokana na mtandao wake ulivyo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sambamba na hilo tunaitaka Serikali kama itafuata ushauri wetu huo iundwe Bodi ya Wakurugenzi ambayo itakuwa na wajumbe wachache kwa lengo la kupunguza gharama za kuendesha bodi hiyo, na ipewe masharti ni kwa muda gani mtaji uliowekwa utakuwa umerejeshwa Serikalini.

Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa kadri mtaji unavyokuwa mkubwa ndivyo shirika linapokuwa na uwezo wa kuwa na bidhaa mbalimbali kwa lengo la kuwavutia wateja zaidi kwani wanakuwa na wigo mpana wa kuchagua. Hivyo, tunazihamasisha Kampuni za Bima kujitahidi kuwa na motisha na wigo mpana wa bidhaa *(Insurance Products)* wanazotoa kwa wananchi ili kusaidia kuwaongezea mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baada ya kuyasema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Halima Mdee kwa kuwasilisha maoni hayo ya Kambi ya Upinzani, na kama nilivyosema mwanzo sasa naomba nimwite

Mheshimiwa Dokta Juma Ngasongwa ili awe msemaji wetu wa mwanzo atafuatiwa na Mheshimiwa Mwinchumu Msomi.

**MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuwa mchangiaji wa kwanza mchana wa leo, pia naomba na mimi nijiunge na wenzangu kwanza kutoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba ambaye alipatwa na mauti akiwa India, naomba Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi roho yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nami nishiriki katika kutoa pole kwa familia ya Mzee mwenzangu Phares Kabuye kwa kifo ambacho kimempata leo asubuhi tena Mkoani kwetu, mimi kama mwana Morogoro naomba kutoa rambirambi hizi lakini vile vile kusema kwamba msiba huu umetugusa sana.

Baada ya kusema mambo haya mawili naomba sasa nimpongeze na kumshukuru ndugu yangu Mstapha Mkullo kwa kuwsilisha Muswada huu, lakini zaidi naomba nimshukuru na kumpongeza mdogo wangu Omar Yusuf Mzee kwa kuwasilisha Muswada huu.

Zaidi naomba nimshukuru na kumpongeza mdogo wangu Omar Yusuf Mzee kwa umahiri amahiri alioufanya wakati akiwasilisha Muswada huu mbele ya Kamati na Mbele ya Bunge hapa, bahati nzuri na mimi nilishiriki kama mdau ingawa mtani wangu pale Andrew Chenge hakunitaja lakini na mimi nilikuwemo katika siku zote zile mbili, kwa sababu ni jambo ambalo lilikuwa linanitia hamasa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru na kumpongeza pia ndugu yangu Ramadhani Kija na Kamishna Kazora na watendaji wenzake ambao walitoa maelezo ya ufasaha kabisa wakati tukijadiliana kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie mambo mawili tu kwanza ni kuhusu kutetea au kutambua nafasi ya wateja, kuwatetea wateja katika huduma hii ya Bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku nyuma kulikuwa na matatizo makubwa sana hasa kwa wateja Walimu, wanajeshi na polisi ambao wamechangia katika Bima zao za maisha na zimeiva lakini kupata fedha ilikuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kwamba Muswada wa sheria hii inaweka vifungu ambavyo vitalinda maslahi ya wateja, vifungu hivi ni vizuri na kimoja ni kile cha 131 ambacho kinalazimisha makampuni ya Bima walipe wateja wao baada ya siku 45 hili ni zuri sana na kifungu cha 148 ambacho kinatoa fursa kwa mteja kwenda Mahakamani ina matatizo kidogo, kwa sababu Mahakama hizi nadhani zitakuwa zaidi katika Mikoa.

Sasa kwa mtu wa Malindi ambaye ni kilomita 450 kutoka Malindi kuja Morogoro hizo safari za kufungua kesi mahakamani kwenda na kurudi zitakuwa za gharama kubwa sana mwisho wake hata Bima yenyewe hata idai tena maana hela zote zitaishia mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani labda huduma ya Mhakama ya Bima inaweza ikasaidia sana kwa sababu tulioupata kwenye Tume za Haki za Binadamu na Utawala Bora tumegundua kwamba hawa jamaa wanafanya mambo haraka na wanapunguza urasimu. Lakini Mahakamani unaweza kuchukua mwaka mzima unadai.

Mfano mmojawapo ni kesi yangu ya uchaguzi ya mwaka 1995 mpaka leo haijaisha, sasa leo mimi ni Mbunge namaliza kipindi cha tatu, sasa uendeshaji wa kesi za Mahakama kwa kasi hii hautaweza kuwasaidia wateja wadogo hawa ambao tunataka tuwatetee kwa nguvu zote.

Kwa hiyo, mimi nasema lazima hata hizi mahakama kama zitakuwepo, basi zipelekwe zaidi kwenye ngazi ya Wilaya ili mashauri haya yafanyike karibu zaidi na wateja kuliko ilivyo sasa. Hili lilikuwa wasiwasi wangu mkubwa katika sheria hii.

La pili, ambalo ni kubwa zaidi linahusu uwezeshaji wananchi kiuchumi. Unatambua kwamba, kwanza, Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ipo katika Ilani ya Mwaka 2005, ingawa imeanza zamani zaidi; imeanza katika Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 1995. Suala la uwezeshaji lilikuweko, lakini ya mwaka 2005 limeipelekwa juu zaidi kwa kuwa kama jambo la msingi namba mbili. Namba moja ni lile la kujenga uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea.

Hili la uwezeshaji wananchi kiuchumi likawa la pili na mimi nafurahi sana katika jambo hili kwamba, sheria hii kwa kupitia hiki kifungu cha 16 ambacho amekitaja mwenzangu hapa; kinaweka fursa nzuri ya kuwawezesha Watanzania kushiriki katika biashara ya bima na kinatamka kabisa kuwa na asilimia 33, 35; jambo hili zuri sana. Vile vile limekwenda mbali, sheria pia inasema kwamba, hata kwenye bodi za wakurugenzi za makampuni nao asilimia 30, 35 wawe Watanzania; jambo hili ni zuri sana.

Mimi nasema suala la kutekeleza Sera hii na Sheria ya Uwezeshaji ya Mwaka 2004 linakwenda pole pole. Wizara ya Fedha ambayo ndiyo wanaosimamia hata sheria hii sasa, kwa sababu Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lipo chini yao, naona pale mambo hayakwenda vizuri. Sheria ipo wazi kabisa pale kwamba, lazima tutoe fedha za kutosha na taasisi zimependekezwa kuundwa mojawapo ambayo inaitwa *entrepreneurship development institute*, kwa ajili ya kusaidia wawekezaji kwa msingi wa uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Kwa hiyo, jambo hili naomba litiliwe mkazo, haiwezi kutosha kuliendesha hili kwa mtindo wa mtu mmoja kuwa na furaha. Hapa tunaweza kusema, labda Wizara waliona furaha au kwa sababu ya *pressure* ya wadau, ndiyo maana wakaweka asilimia theluthi moja ili iwe sehemu ya miliki ya Watanzania; ni jambo zuri. Lazima sasa tuwe na mkakati mzuri wa kutekeleza sera yenyewe ya mwaka 2004, lakini pia tutekeleze vizuri Sheria ya Mwaka 2004. Sera ile ilitolewa mwezi Februari, 2004 na sheria ikatungwa katika kikao cha Novemba, 2004 na Mheshimiwa Rais, alitia saini tarehe 19 Januari, 2005. Mimi nafuatilia hivi kwa sababu zamani nilikuwa mdau katika suala hili la uwezeshaji na naendelea kuwa mdau mpaka sasa.

Kwa hiyo, naomba hili nalo litiliwe mkazo, kwa sababu bila kutilia mkazo suala hili hatuwezi kupata maendeleo ambayo tunayatarajia. Uzoefu wa duniani upo Malaysia pale, uzoefu wa uwezeshaji wananchi kiuchumi upo Afrika Kusini. Afrika Kusini walipopita ile *Black Economic Empowerment Policy*, ambayo wao wanaiita BEE, kulikuwa na kuweka *percentage* namna hii. Hii ndiyo tahadhari ambayo nataka kuiweka kwa Wizara kwamba, kuna watu wajanja wenye makampuni makubwa, wakaweka watu kwamba jamani Dkt. Juma Ngasongwa na huyu Mwantumu Mahiza wana hisa katika kampuni hii, lakini kusema kweli hawana hisa mle, wamewekwa tu pale. Ushahidi huo upo Afrika Kusini, hata Malaysia upo. Kwa hiyo, ni muhimu hili kuliendeleza zaidi. Haitoshi kusema tu viwango bila kwenda ndani, maana yake mnaweza mkasema kweli hiki mna theluthi moja au mbili au wananchi kumbe haipo kwenye theluthi.

Kwa hiyo, ni muhimu kulitazama na kuliwekea mkakati mzuri na kulikagua, labda Kamishna wa Bima atakuwa analitazama hili mara kwa mara kama sehemu ya kazi zake. Sijaliona kwenye Muswada, labda mtakapoandaa zile kanuni basi mambo hayo pia yatazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kukushukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kuchukua fursa kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu juu ya Muswada wa Bima ulio mbele yetu.

La pili, naomba ku-*declare interest* kwa sababu mimi ni miongoni mwa watu ambao nimo kwenye shughuli hizo za bima na kanuni zetu zinasema unapofikia kwenye mchango wa aina hiyo, lazima u-*declare interest.* Pamoja na hayo, Muswada huu ni mzuri na umekuja kwa wakati muafaka, ambapo utawezesha Watanzania kushiriki katika shughuli za bima kwa uwazi na kwa mafanikio makubwa kabisa. Muswada huu ukipitishwa, Tanzania tutakuwa nchi ya pili katika Afrika ambao tutafanana na wenzetu wa Afrika ya Kusini. Kwa hiyo, nikiwa mdau, naomba sana Waheshimiwa Wabunge waupitie, wauchangie vizuri na wauboreshe, hatimaye tuweze kuupitisha ili shughuli zetu za bima ziweze kufanya kazi vizuri nchini.

Hali kadhalika, Muswada unatoa nafasi nzuri kufanya kazi kwa uwazi kabisa. Hapo mwanzo shughuli hizi nyingi zilikuwa zikitolewa maamuzi na Kamishna wa Idara ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Nchini. Kwa kupitisha sheria hii, kutakuwa na mambo mengi ya uwazi ambayo Mheshimiwa Kamishna amepunguziwa.

Kutokana na Muswada huu, ninaomba kila mmoja kwa maana ya wawekezaji kwenye Sekta ya Bima na wale ambao wanawekeza kwenye bima, wanachama watakuwa na haki ya kusikilizwa kwenye Kamati mbalimbali za rufaa na kutakuwa na mahakama ndani ya bima. Kwa hiyo, hili ni jambo bora; ni jambo ambalo kwa kweli Wananchi wa Tanzania tuitikie na Wabunge tuitikie ili hatimaye sheria hii iweze kufanya kazi katika Serikali yetu.

Naipongeza sana Wizara ya Fedha, naipongeza vile vile Idara ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Nchini, kwa marekebisho ambayo hapo awali yalikuwa na urasimu mkubwa; ya uteuzi wa Naibu Kamishna wa Idara ambaye mwanzoni ilikuwa lazima apate ridhaa ya ndugu zetu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa jinsi nilivyousoma Muswada huu, nimeona sasa moja kwa moja atakuwa akiteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, naipongeza sana Wizara kwa kuliona jambo hilo ambalo ni la msingi kabisa, kwa sababu itawiana na taasisi nyingine za Muungano ambazo zinafanya kazi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama vile Uhamiaji, *TRA*, *TICRA* na kadhalika.

Katika Muswada huo sijaona kipengele ambacho kinaelezea kuundwa kwa idara ndani ya mamlaka; sijui pengine itaelezwa kwenye kanuni lakini niliona ni muhimu kutaja idara ambazo zitakuwa chini ya mamlaka hii, ambazo zitakuwa chini ya Bodi ya Mamlaka ya Bima Nchini. Hali kadhalika, sijaona pia sehemu ambayo inatoa mamlaka au kipengele ambacho kinazungumzia kuundwa kwa Kamati ndogo ndogo ndani ya mamlaka itakayoundwa. Kwa hiyo, naomba hilo nalo liangaliwe au vinginevyo labda litaingia kwenye kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika nimetazama kwenye Muswada sikuona uendeshaji wa mamlaka utakuwaje, nilitaka kujua hilo. Je, utaendeshwa kikanda au utakuwa unafanya kazi kwa kila mkoa? Hilo nalo nadhani lingekuwa bayana katika Muswada huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Muswada huu pia nimeona kuna sehemu ya kuunda Bodi ya Mamlaka ya Bima Nchini, lakini sikuona ukomo wa Wajumbe wake; yaani idadi ya Wajumbe ambao watahusika kuteuliwa kufanya kazi ya mamlaka. Ningeomba suala hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka nchi yetu hivi karibuni au miaka ya hivi karibuni, tumekumbwa na sakata la Shirika la Bima la Taifa (*NIC*). Ninavyoelewa ni kwamba, idara hii imeshiriki kwa karibu sana katika kuisimamia *NIC* ili kurudisha hadhi yake; hali kadhalika kusimamia taratibu zote za ulipaji wa madeni mbalimbali. Ninaelewa kwamba, idara ni moja kati ya Wajumbe wanaosimamia uboreshaji wa Shirika la Bima la Tanzania. Ninaomba sana waendelee na juhudi hizo ili hatimaye wanachama wenye haki na wajibu wa kulipwa mafao yao waweze kulipwa kwa wakati muafaka na kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa sana, nimeona Muswada huu wa Sheria umeigusa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi juu ya maisha bora kwa kila Mtanzania. Kwa maana ya kwamba, Muswada huu ukipita na kuwa sheria, utawezesha Watanzania kuendesha biashara ya bima. Jambo hili hapo awali halikuwepo, lakini ndani ya Muswada huu limejitokeza na ni jambo la kufurahisha kabisa na linakwenda sambamba na Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya kuweka maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hayo, ninaelewa idara ina jukumu kubwa la ukaguzi wa taasisi hizi za bima. Itakapopita sheria hii, Mamlaka isimamie vizuri suala la ukaguzi katika taasisi zinazofanya shughuli za bima nchini. Ukaguzi wa taasisi hizo ni muhimu na utawezesha kujua na kuelewa uwezo na uendeshaji wa taasisi hizo. Kwa hiyo, naomba idara hii kwanza, ipewe nguvu za kutosha kabisa kwenye shughuli za ukaguzi na uimarishwe ukaguzi ili taasisi hizo zifanye kazi kwa ufanisi unaokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna balaa pia la wizi wa *sticker* za bima; idara hii ina dhamana ya kusimamia *sticker* za bima. Kwa hiyo, ninatoa wito au ninaiomba mamlaka itakayoanzishwa, kusimamia ukaguzi wa mara kwa mara wa *sticker* za bima na ikiwezekana kuweka adhabu kali kwa wale ambao watakumbwa na tabia hii ya wizi wa *sticker* za bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba pia idara na mamlaka hapo baadaye kuimarisha utendaji huko Zanzibar, kwa maana ya kuweka wafanyakazi wenye elimu ya kutosha; na vile vile kuipa nyenzo ofisi ya usimamizi wa shughuli za bima nchini na kuweka vifaa vya utendaji wa mamlaka au idara hiyo iliyopo Zanzibar ili kumuwezesha Mkurugenzi kufanya shughuli zake za bima kwa ufanisi mzuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa zaidi ni elimu juu ya bima kwa Watanzania. Hili ni jukumu muhimu sana, itakapokuwa mamlaka na ndugu zangu waliopo sasa hivi wahakikishe Watanzania wanaelimishwa juu ya shughuli za bima na faida zake. Mambo haya yapo sana mijini.

Kwa hiyo, naiomba sana idara na mamlaka itakayokuja wahakikishe kwamba, elimu ya shughuli za bima inatolewa. Watanzania waelimishwe na baadaye wajiunge na shughuli hizi ili kupata faida inayokusudiwa kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, nakushukuru sana. Kama nilivyosema mwanzo, mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary kutoka Baraza la Wawakilishi, karibu sana.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kidogo tu katika Muswada huu ambao ni muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina pingamizi na Muswada huu, lakini ningeliomba nipate ufafanuzi juu ya vipengele fulani, ambavyo ninahisi kidogo vina matatizo, ambayo yanaweza yakaleta mkanganyo kidogo wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia, nianze ukurasa wa 12 wa Muswada huu. Katika ukurasa wa 12 kwenye *interpretation* hapa kuna neno ambalo limetafsiriwa, yaani *marriage* wanasema "*marriage shall have the same meaning assigned to it by the Law of*

*the Marriage Act or any other law."* Sasa sina uhakika kama *definition* hii imezingatia masuala ya ndoa katika mila nyingine. Zanzibar kwa mfano, kwa sababu sheria hii ina-*apply* mpaka huko na *Zanzibar Marriage Act* ni sheria ambayo inatumiwa kwa *Civil Marriage*, lakini mambo mengine yote yanashughulikiwa katika dini zinazohusika. Sasa je, *definition* hii itatosheleza kwa mujibu wa utaratibu uliopo hapa? Hilo ni suala la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 14 vilevile kifungu cha 4(2) wanasema: "*For the purpose of subsection (1) and generally under this Act ...*" Sasa mimi swali langu ni kwamba; kwa nini tukatumia *and generally under this Act,* kwa sababu sheria hii inahusu pande zote mbili za Muungano? Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria tuseme kwamba, *for the purpose of this Act* basi, yaani ina-*cover* sheria nzima, lakini hili neno *generally,* hapo baadaye litaleta matatizo. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Naibu Waziri anipe maelezo kuhusu kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika ukurasa wa 61 vilevile kifungu cha 98 pale wamezungumzia *life policy* ambazo zimekuwa *effected by married persons*. Sasa hii inategemea *definition* ya *marriage* ambayo tumeitoa katika *interpretation* na ikiwa yale niliyoyaeleza kule yatakubalika. Kwa hiyo, lazima kifungu hiki kibadilike kwa mujibu wa tasfiri hiyo nyingine, ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ataitoa, yaani kuzingatia ndoa nyingine ambazo hazimo katika *Marriage Act* au katika *Civil Marriage Laws*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija katika ukurasa wa 64, kifungu cha 101, napo kuna matatizo vilevile. Ukitazama kifungu cha 101(1)(b) kinasema "*Before or during marriage, a woman effect or cedes for the benefit of her husband*." Sasa sheria nyingine ikiwa ni *before marriage,* hakuna *husband*. Sasa ikiwa tumesema *before or during marriage* halafu tunayemzungumza hapa ni *husband,* nafikiri hii ni *wrong* kwa sababu kwa sheria nyingine, kwa mfano ya Kiislam, *before marriage* itakuwa hana mume au hana mke. Kwa hiyo, nafikiri kifungu hiki nacho kinataka ufafanuzi zaidi.

Halafu katika ukurasa wa 84 kifungu cha 131, kinatoa muda wa malipo ya *claims* zile. Sasa hapa muda wake ni siku 45, lakini baada ya kupita siku 45 na ikiwa huyu mhusika wa Bima hajalipa, anaweza akaomba kwa Kamishna na Kamishna kwa mujibu wa kifungu hiki ni anaweza akatoa *extra time*.

Ninachofikiria ni kwamba, hii *extra time* lazima tuiweke bayana, kwa sababu inaweza ikawa zaidi ya siku 45 wakati umekwishampa siku 45, sasa *extra time* hii ni *vague.* Tuweke kwa mfano, *within twenty one days* au siku zozote ambazo tutahisi kwamba zinafaa. Kwa hiyo, hiyo, itamdhibiti zaidi huyu mhusika wa Bima. Zaidi ni kwamba, katika hizi *extra time* ambazo amepewa, ikiwa hajafanya malipo basi wanasema kwa mujibu wa kifungu cha 131(3) ni kwamba, ikiwa imefika ile *extra time* na bado hajalipa, basi huyu mtu atakuwa *considered* katika suala la *bad faith*. Sasa *bad faith* ina matatizo, kwa sababu hawakusema hapa inatokana na kosa lipi ambalo limewekwa katika kifungu cha 166 katika *penalties.*

*Penalty* ya *bad faith* hapa wamesema ni *five million* tu, lakini ikiwa shughuli zile za *Insurance* pale zinazidi *five million* halafu mtu akafanya makusudi akajiingiza katika *bad faith* akalipa *five million;* je, nani anaipata hasara si mteja? Mteja akipata hasara ni tatizo na tutawaumiza wananchi wetu. Kwa hiyo, mimi ninadhani *penalty* ile irekebishwe ili ilingane na ile *bad faith* aliyofanya; ikiwa kafanya *bad faith* kwa mtu ambaye malalamiko yake au *claims* zake ni zaidi ya milioni 20; kwa hiyo, *penalty* ile isiwe milioni 5 iwe zaidi ya milioni 20 ili kumtia adabu zaidi. Vinginevyo, kila mtu au kila mhusika wa *Insurance* atakwenda katika kifungu hiki cha *bad faith* kwa kujua tu kwamba, atalipa milioni 5 badala ya milioni 20 au milioni 30 ambazo anadaiwa. Kwa hiyo, nafikiri hii ina matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi sikuona katika sheria hii haya matatizo yanayofanywa na *Insurance Companies* wakati wa ku-*claim,* kwa sababu wakati mwingine mteja anakwenda anazungushwa na hao wahusika wa Bima; anaambiwa njoo kesho, njoo kesho kutwa na mwisho anaambiwa aende Mahakamani. Akienda Mahakamani, tunajua *system* za Mahakama zilivyo hivi sasa, inaweza ikachukua miaka mitatu kesi inaendelea tu. Kwa hiyo, tutakuwa tunamtia adabu huyo mtu kwa kisingizio cha Mahakama. Sasa ninafikiri tungeliweka kifungu au tungeliongeza kifungu ambacho kinawadhibiti watu wa namna hii ili hao wateja au wananchi wetu waweze kuwa na imani zaidi katika utaratibu mzima wa Bima kama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo kwamba, ninakubaliana na Muswada huu, lakini nilikuwa naomba nipate ufafanuzi wa vifungu hivi ili sheria yenyewe iweze kuwa nzuri na iwe na maslahi kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, ahsante sana kwa maoni yako na moja ya mambo ambayo umeyazungumzia ni kwamba, kule Zanzibar siyo rahisi *before marriage* pakawa na *husband*. Nataka nikwambie tu kwamba, huku Bara mara kadhaa watu wanaalikwa kwenye harusi ambapo mtu anamuoa mkewe. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna karatasi ambayo imekuwa ikizunguka; ni *Schedule of Amendment* ambayo imetoka; hivyo ni vizuri mkaipitia ili wakati wa vifungu muwe makini na marekebisho yaliyoletwa na Serikali. Kwa hatua hii, sasa ninaomba nimwite Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Omar Mzee; karibu sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nataka nichukue nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo niweze kuhitimisha hoja yangu ambayo nimeitoa asubuhi, inayolitaka Bunge liridhie tuje na sheria mpya ya Bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nataka niwatambue wale ambao wamechangia kwa kuongea nikianza na Mheshimiwa Andrew Chenge, ambaye amewasilisha maoni ya Kamati; wa pili ni Mheshimiwa Halima Mdee, ambaye amewasilisha maoni ya Kambi ya

Upinzani; wa tatu ni Dkt. Juma Ngasongwa; wa nne ni Mheshimiwa Mwinchoum Msomi; na wa tano ni Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, napenda pia niwatambue wale wote ambao wamechangia kwa maandishi, nikianza na Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed.

Mheshimiwa Mwnyekiti, kwa ruhusa yako, labda kwanza niseme tu Wabunge sote hapa tuwe pamoja katika huu Muswada wa Sheria ya Bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tunachokizungumza hapa ni kufanya marekebisho katika Taasisi nzima ya Bima, ndiyo maana tukaleta huu Muswada wa Sheria. Tumesema kwamba, tunaliomba Bunge hili liridhie kuifuta Sheria iliyopo hivi sasa ili tuje na Sheria mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwa kifupi, kabla sijatoa majibu ya hoja kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kwa nini hasa tunakuja na sheria hii mpya ya Bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi, kabla sijatoa majibu kwa baadhi ya hoja; kwa nini hasa tunakuja na Sheria hii mpya ya Bima? Nikijibu ni kwa nini tunakuja na sheria hii mpya ya bima, ninaweza nikawa ninajibu baadhi ya hoja za Wabunge. Sheria iliyopo hivi sasa, haijamlinda mteja kikamilifu, ndio maana Waheshimiwa Wabunge wengine walidiriki kusema hapa kuna nenda rudi, njoo kesho, kutolipwa kwa muda, kutolipwa kwa ukamilifu. Hiyo ilisababishwa na sheria inayokwenda sasa hivi kuwa kuna mianya mingi tu na ndio maana tukasema kwamba ni lazima tuje na sheria mpya, ambayo itaziba hii mianya na kumsaidia huyu mteja. Mteja hapa ni yule ambaye anaweka bima na ndio maana tukasema tunataka sheria hii mpya tuianzishe hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii itapunguza hii nenda rudi, kwa sababu makampuni haya na mawakala tumeyabana ndani ya hii sheria. Tumetoa meno kwa Kamishna na kwa Mahakama na vilevile tumetoa meno kwa chombo ambacho kitaundwa na makampuni yenyewe, kama yatapata matatizo kutokana na maamuzi ya Kamishna. Katika sheria ambayo tunakwenda nayo hivi sasa, mambo hayo hayakuwepo au yapo lakini mtu anaweza akapenya kwa njia nyingine au kwa vifungu vingine; hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tunakuja na sheria hii mpya kwa sababu sisi sote tunaelewa kwamba, bima ni biashara; kama sisi Watanzania hatujawekeza katika biashara ya bima, atakuja mgeni kuwekeza. Mgeni anapowekeza katika biashara ya bima, anatoka na mapato yote anakwenda kupeleka huko anakotoka, Watanzania tunabaki kupiga kelele. Tukasema katika hii biashara ya bima na Watanzania tuingie na tukasema kwamba, tuingie kwa kiwango kisichopungua moja ya tatu, tunasema kisichopungua. Kampuni inayotaka kuja kuanzisha shughuli ya bima, tunaiambia mapema kwamba, tunataka na Watanzania waingie katika kampuni hiyo na mtaji usipungue moja ya tatu.

Mheshimiwa Chenge na Mheshimiwa Ngasongwa wamesema, sasa hata *Board Members* wasipungue moja ya tatu. Hii ni kwa sababu hii ni biashara, kama kila siku Watanzania tutakuwa tunanung'unika tunakaribisha wageni; tukasema hapana na sisi tuingie. Kwa hiyo, katika sheria yetu hii mpya inaweka wazi kwamba, Watanzania tutashiriki kikamilifu katika suala hili ili hicho kitakachovunwa basi na sisi kama ni wananchi, tuweze kufaidika kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria hii mpya vilevile tumesema kwamba, Tanzania sasa hivi imebadilika sio kama miaka ya nyuma. Miaka ya nyuma ilikuwa ukimkuta Mtanzania hapa anaendesha gari zuri zaidi utasikia ni Toyota; leo Watanzania wanaendesha magari yenye gharama kubwa. Tukasema kama Mtanzania atakuwa ana uwezo wa kufungua kampuni ya bima, lakini mtu anayetaka kuweka bima chombo chake kina gharama kubwa, basi aweze kushirikiana na makampuni ya nje ambayo yana uwezo mkubwa wa kulipa ile bima. Mfano mzuri ni Kampuni ya *American Insurance Group (AIG).* Watanzania wanaweza wakasema kwamba, sisi huyu aliyekuja kuleta bima gharama ya chombo chake ni kubwa, hatuna uwezo lakini wasiiache ile kazi; wachukue kazi ile halafu washirikiane na makampuni makubwa yaliyoko nje ili wao wapate na ile kampuni iweze kupata. Sheria hii vilevile tumeipa ule uwezo wa kuweza kufanya mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tumesema katika sheria iliyopita, hiki chombo kilikuwa kinatambuliwa kama Idara ya Bima, lakini kilikuwa kinafanya kazi kama mamlaka. Bahati nzuri tunakuja na sheria hii ambayo tunakata kuibadilisha. Angetoka Mtanzania mmoja akasema hawa ni Idara lakini wanafanya kazi kama Mamlaka; uwezo huo wameupata wapi; chombo hiki kingelikuwa na matatizo. Tukasema tunataka tuombe ridhaa ya Bunge, hiki chombo sasa badala ya kuitwa Idara iitwe Mamlaka. Tukipe uwezo zaidi wa kuweza kufanya shughuli za bima, kama ambavyo sheria inataka. Kwa hiyo, tumeomba tuje na hayo mapendekezo ya kwamba, chombo hiki kiwe Mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tumesema kwamba, kwa sababu makampuni haya ya bima yapo mengi; sasa hivi Tanzania tunayo zaidi ya 20 na kwa sababu haya makampuni yanafanya shughuli za kibiashara, yaweze kuchunguzwa mwenendo wake kibiashara; yaweze kukaguliwa, tuweze kuyaona mapema kwamba haya makampuni hayaendi vizuri. Kamishna atoe melekezo kwamba, wewe sasa hauendi vizuri, aidha tukupe kampuni ikulee au tukufunge. Sio kumfunga jela ni kuifunga ile kampuni yenyewe kwamba, inasimamisha shughuli zake. Vinginevyo, utawakuta hawa wateja wanaathirika.

Vilevile tukajiuliza ikitokea kampuni ambayo inaenda ovyo hawa wateja watafidiwa na nani? Tukasema kwamba, sheria hii tuipe meno hayo ili iweze kufanya kazi, kwa hiyo kila mtu ambaye atakuwa na bima mahali asiwe na wasiwasi; madhali yeye anatoa mchango wake kwa mujibu wa ile bima yake, basi asiwe na wasiwasi tena na shughuli zile ambazo tunazifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukasema kwamba, katika kanuni ambazo hivi sasa tuko mbioni kuzimalizia maana yake tumekwenda sambamba na kutayarisha sheria na kanuni, ni lazima kuwe na kima cha chini cha kuanzisha biashara hii na isiwe kila mmoja anakuja na kima chake. Tukasema hivi leo hata kuanzisha *Bureau De Change*, Sheria ya *BoT* inatuambia ni lazima kuwe kuna *minimum of USD 45,000;* haiwezekani hawa wakawa wanakuja tu wanasema sisi tunataka tuanzishe bila kuona hicho kianzio kiko wapi. Tukasema sheria hii ndio itakayotusaidia kutuwezesha kufikia huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niseme tu kwamba, tumesikia maelezo, maoni na mapendekezo ya Wabunge kuhusu *NIC.* Sijamsikia hata Mbunge mmoja aliyesema kwamba *NIC* ifungwe, wengi wamesema tuliboreshe Shirika letu la Bima la Taifa. Sisi Wizara ya Fedha tunakubaliana na ninyi kwa asilimia mia moja na ndio hivi sasa tuko mbioni kufanya hivyo. Tumejaribu kuwa-*retrench* wafanyakazi wao na kila mmoja kumlipa mafao yake na hivi sasa tunajaribu kuliunda upya shirika hili. Tunajaribu kuangalia uwezekano wa kulipa madeni ya *NIC* yanayodaiwa na wateja ili hili shirika litakapokuja lije na nguvu za kushindana na mashirika mengine na makampuni mengine ya bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza mwanzo kwamba, Muswada huu ni kwa ajili ya *industry* nzima na sio kwa ajili ya *NIC;* kwahiyo nitaomba sana Waheshimiwa Wabunge, tutakapokuwa tunachangia, tuchangie au tusaidiane katika suala hili la *industry* nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, labda sasa nijibu baadhi ya hoja ambazo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamezitoa. Michango yao itusaidia katika utendaji wa hii Mamlaka itakapokuwa inaanza shughuli zake, pamoja na Makampuni ya Bima. Wabunge wachache wametoa maoni na wametaka ufafanuzi.

Mheshimiwa Msomi, amesema hajaona hii sheria ina wajumbe wangapi wa bodi. Sheria hii itakuwa na Mwenyekiti, ambaye atateuliwa na Rais na itakuwa na Wajumbe wengine wanane ambao watateuliwa na Waziri, ambaye anasimamia masuala ya bima. Ukitazama katika mtiririko mzuri wa sheria hii, tumeangalia sura ya Muungano vilevile, angalau basi kuwe kuna Wajumbe kutoka Zanzibar *at least* wawili wawepo. Kwa hiyo, sura ya Muungano tumeiangalia katika sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kama nimemuelewa vizuri Mheshimiwa Msomi, ametaka kufahamu kama tutakuwa na kitengo Kikanda. Nataka niseme tu kwamba, Mamlaka itakuwa na Makao yake Makuu pale Dar-es-Salaam, lakini makampuni, mawakala na madalali wa bima watakuwepo Tanzania nzima; wataweza kufanya hiyo shughuli ya bima Tanzania nzima na watafika katika wilaya zote. Kila anayetaka kuweka bima ya maisha, anayetaka kuweka bima ya gari, anayetaka kuweka bima ya nyumba, atakuwa na uwezo wa kuweza kufikiwa na bima. Tatizo letu ni kwamba, tunachagua bima gani, tunachagua kampuni gani, ndio tatizo; lakini ukweli ni kwamba, makampuni ya bima yatakuwepo katika maeneo yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mdee na Mheshimiwa Msomi, wametaka Watanzania waelimishwe juu ya suala zima la uwekaji wa bima. Mimi nataka nisema kwamba, hii hoja ni nzuri sana kwa sababu Watanzania sasa hivi tuko katika *transition period,* tunahitaji taaluma katika maeneo mengi, kwetu ni mapya. Kwa wenzetu kuna Bima ya *Marriage,* Watanzania hatuna. Leo Watanzania tukiwa na harusi tuna michango, kumbe kuna Bima ya Ndoa, wewe mwenyewe unafika miaka yako 18, 19 au 20, unaanza kuweka bima kwa ajili ya ndoa. Ukifika miaka yako 30 au 40 ukasema sasa unataka kwenda kuoa, bima inakupa pesa unakwenda kuoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, kuna Bima za Afya. Watanzania wengi leo bima kubwa ambayo tunaweka ni Bima ya Gari na hiyo tunaweka *third part.* Hatuelewi faida ya *comprehensive* na hatuelewi hasara ya *third part. Third part* maana yake ukigongana na mwenzako gari lako halitengenezwi, linatengenezwa la mwenzako; na kama una abiria ndani bima haitam-*cover.* Ukiweka *comprehensive,* hata kama umebeba abiria ndani inam-*cover* na yule abiria uliyembeba. Ndugu zangu tunakuwa na kigari chetu kimoja cha familia, tunabeba familia nzima tunakwenda nayo safari. Kwa hiyo, haja ya taaluma ya bima kwa wananchi wetu mimi nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwa asilimia mia kwa mia kwamba, ipo haja hiyo kwa sababu Watanzania bado hatujaielewa hii taaluma ya bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niseme kwamba, kuna faida nyingi sana katika bima. Licha ya kwamba, tupo katika jitihada za kutoa hii taaluma, naomba nichukue fursa hii, kuwaomba wananchi wote waangalie mfumo wa bima na wanagalie ni wapi waweke bima zao. Wengi tuliomo humu ndani, hata Wabunge hatuna Bima za Afya. Hii ni dhahiri kwamba, ukiumwa wewe unakwenda unajitibu kwa pesa zako. Mara nyingine *pressure* inapanda mara inashuka, kwa hiyo, ninawaomba ndugu zangu hasa sisi Wabunge, tujitahidi sana kuwaelimisha wananchi wetu katika Majimbo yetu juu ya faida za bima, sio bima ya gari tu peke yake, kuna bima nyingi sana ambazo tutaweza kufahamishana wakati utakapofika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijaribu kama nitaweza kujibu maswali ambayo aliniuliza Mheshimiwa Abubakar na kama sitaweza Mwanasheria yupo, tutakapoingia kwenye vifungu basi atatusaidia. Kwanza, nataka niseme katika Sheria ya Ndoa ambayo ipo Tanzania, nitamwomba *AG* ani-*correct* tutakapopitia kifungu kwa kifungu tukifika kwenye kifungu hicho; inatambua ndoa za aina zote na ndio maana ikawa inaitwa ndoa.

Nakubaliana na Mheshimiwa Abubakar, nataka niseme sio Zanzibar, kwa sababu kuna watu walisema kabla ya kuoa hakuna mwanaume; halafu kuna wengine wakasema Zanzibar, nataka ni-*correct* kidogo. Sio Zanzibar, ile ni *under Islam.* Chini ya Uislamu, kabla ya kuoa huwezi ukasema huyu ni mume wangu, huwezi ukasema huyu ni mke wangu, hayo yanakuja baada ya kuoa. Baada ya kuoa ndio unasema huyu ni mke wangu na una haki naye sasa na huyu mume wangu na una haki naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba, kifungu hicho tutakiangalia zaidi na kwa bahati *AG* yupo atatusaidia; kama kinakidhi atatuambia kinakidhi na kama hakikidhi atatuambia tuondoe hilo neno tuweke lingine. Vilevile

nataka niseme katika maelezo yake Mheshimiwa Abubakar kuhusu kifungu namba 131 hapa alisema, Kamishna tumemwachia aendelee na tumempa uwezo hapa aweze kuangalia tatizo ni nini; kama kampuni imeshindwa kulipa *dues* katika muda uliowekwa wa siku 45, tumempa uwezo Kamishna aangalie tatizo ni nini.

Anaweza akawaambia *I am giving you seven days extra only*, u-*file* ulipe *claims* zako, kwa sababu anatazama uzito wa lile tatizo. Leo ukija kumfunga hapa ni lazima tukubaliane kwamba, kuna makampuni mengine yana matatizo makubwa na yana madeni makubwa. Sasa ataangalia lile tatizo, atakuja na *judgement*, ataangalia muda wa kuweza kumpa, ataangalia *income statement* za huyu; Kamishna ataangalia kila kitu, halafu atasema wewe ninakupa siku kadhaa za nyongeza ili uweze kulipa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamishna ndiye atakayembana huyu kampuni aweze ku-*clear* hayo madeni ambayo anatakiwa kulipa. Kwa hiyo, hapo tumefanya, lakini Mheshimiwa Abubakar na Waheshimiwa Wabunge, tunasema sheria yetu iliyopita ambayo ndio hii tunayoomba tuifute, ile *business trend* yake ilikuwa ni ndogo sana, lakini kwa sasa kwa sababu Kamishna ana nguvu hizo za kuitazama hii kampuni kama ina mwelekeo wa kibiashara, nafikiri Kamishna ataweza ku-*trace* kwa haraka zaidi kama kampuni hii inaweza ikawa na matatizo katika kipindi kifupi.

Kwa hiyo, ndio tukasema kwamba, acha tumpe madaraka haya Kamishna tuone tutakwenda naye vipi, pengine huko mbele tunakokwenda, tunaweza tukawa na makampuni ambayo hayatakuwa na matatizo katika ulipaji. Amezungumzia suala la *penalty* ya milioni tano, akasema kama kosa ni kubwa zaidi ya milioni tano, hii milioni tano ndipo watu watakapokimbilia kulipa. Nadhani tutakapoingia kwenye kifungu tutamwachia *AG* aweze kutushauri tutairekebishaje hii, kama inakidhi hivyo ilivyo kwa makosa ambayo tunayaona au kama kutakuwa kuna kosa zaidi ya milioni tano, kifungu gani kingine kinaweza kikaibana hiyo kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, kwa heshima na taadhima sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Bima wa Mwaka 2009
***(The Insurance Bill, 2009)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukursa wa 12 kwenye *definition* ya *marriage*, nilisema kwamba, *marriage shall have the same meaning assigned to it by the Law of Marriage Act or any other law*. Nilisema kwa kuwa sheria hii ina-*apply* mpaka Zanzibar, kwa hiyo, ioneshwe kwamba na zile sheria za Zanzibar kule zimekuwa *included*. Kwa sababu *the Marriage Act* ni ya hapa Tanzania Bara na *any other law* inakuwa *refered* kwa sheria za hapa Tanzania Bara, zile sheria za Zanzibar hazipo hapa.

**MWENYEKITI:** Nimepata tabu kukufuatilia, lakini kwa sababu tunaye mtaalamu hapa atatusaidia. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimemuelewa vizuri, Mheshimiwa Abubakar anasema kwamba, kifungu kilivyo hapa sasa hivi kwa hii *definition* hai-*apply in Zanzibar*. Mimi ninavyoisoma naona ina-*apply*, kwa sababu sheria hii ina-*apply* Zanzibar pia. *Definition* ya *marriage*, ukisoma hiki kifungu kinasema *marriage shall have the same meaning assigned to it by the Law of Marriage Act and any other law*. Kwa hiyo, *other law* ni pamoja na zile za Zanzibar na sio za *Mainland* tu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 13

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16

Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38
Ibara ya 39

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 40

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48
Ibara ya 49
Ibara ya 50
Ibara ya 51
Ibara ya 52
Ibara ya 53
Ibara ya 54

Ibara ya 55
Ibara ya 56
Ibara ya 57
Ibara ya 58
Ibara ya 59
Ibara ya 60
Ibara ya 61
Ibara ya 62
Ibara ya 63
Ibara ya 64
Ibara ya 65
Ibara ya 66
Ibara ya 67
Ibara ya 68
Ibara ya 69
Ibara ya 70
Ibara ya 71
Ibara ya 72
Ibara ya 73
Ibara ya 74
Ibara ya 75
Ibara ya 76
Ibara ya 77
Ibara ya 78
Ibara ya 79
Ibara ya 80
Ibara ya 81
Ibara ya 82
Ibara ya 83
Ibara ya 84
Ibara ya 85
Ibara ya 86
Ibara ya 87
Ibara ya 88
Ibara ya 89
Ibara ya 90
Ibara ya 91
Ibara ya 92
Ibara ya 93
Ibara ya 94
Ibara ya 95
Ibara ya 96
Ibara ya 97
Ibara ya 98
Ibara ya 99
Ibara ya 100

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 101

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu hoja alisema kwamba, atatupa maelezo wakati wa Kamati hapa kuhusu *whether* ni sawa kwa mwanamke au mwanamume kabla ya ndoa kuitwa mume au mke. Sasa nilikuwa naomba nipate maelezo, kifungu hiki kitarekebishwa vipi iweze ku…

**MWENYEKITI:** Kipengele gani hasa hapa kwenye 101?

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** 101(1)(b).

**MWENYEKITI:** Kisome vizuri.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** *Before or during marriage a woman effect or cedes for the benefit of her husband.* Suala ni kwamba, *before* ikiwa ni *before* basi kutakuwa hakuna *husband* kama ni mwanamke na ikiwa ni mwanamume kama ni *before* kutakuwa hakuna mke.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoa hoja alishalizungumzia suala hili lakini ninavyofahamu ni kwamba, zipo ndoa za aina nyingi na wakati mwingine watu hukaa kama mke na mume kabla ya kuoana. Kwa hiyo, hii sheria inaangalia ndoa za aina zote, sio ndoa za aina moja tu.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubalia kwamba, kuna ndoa nyingine ambazo hata kama mtu hajaoa basi baadaye ikiwa wanakaa pamoja wanakuwa ni mtu na mumewe, lakini kuna ndoa nyingine hasa za Kiislamu nilizozizungumzia, ikiwa hakuna ndoa huwezi kuwa na mke au huwezi kuwa na mume. Kwa hiyo, hili neno *before* ama liondoke iwe ni *after the marriage,* kwa sababu *before the marriage* hakuna mume wala mke. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hii sheria ni ya watu wote sio ya baadhi ya watu tu, kwa hiyo, kama ni kweli kwamba kuna watu wanakaa pamoja kabla ya kufikia nia ya kuoana na kama alivyosema Mheshimiwa mtoa hoja ni kwamba, kuna ile *insurance* ya ndoa; sasa mkisema watu wanakaa pamoja lakini hawajaoana lakini kuna vitu ambavyo wanavifanya, sasa wanapooana wasije wakaathirika kwa vitu ambavyo walishavishughulikia.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Anachojaribu kukielezea hapa, unapotunga sheria ni lazima ku-*capture scenario* nyingi; wapo watu wanaishi miaka kumi, ishirini na kadhalika, wana watoto ni mume na mke. Kwa maana hiyo, sheria hii inazungumzia *benefit of her husband actually* inataka kulenga akina

mama watakaoachwa katika mazingira hayo. Mimi nadhani liemeeleweka kwa ufafanuzi wake.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 102
Ibara ya 103
Ibara ya 104
Ibara ya 105
Ibara ya 106
Ibara ya 107
Ibara ya 108
Ibara ya 109
Ibara ya 110
Ibara ya 111
Ibara ya 112
Ibara ya 113
Ibara ya 114
1baraya 115
Ibara ya 116
Ibara ya 117
Ibara ya 118
Ibara ya 119
Ibara ya 120
Ibara ya 121
Ibara ya 122
Ibara ya 123
Ibara ya 124
Ibara ya 125
Ibara ya 126
Ibara ya 127
Ibara ya 128
Ibara ya 129
Ibara ya 130

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 131

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY**: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 131, nilizungumzia hii *extra time* ambayo Kamishna anaweza aka-*grant*. Mheshimiwa Waziri alisema kwamba, inategemea *insurer* yule pengine ana shughuli zake nyingi sana, matatizo yake ni makubwa, sasa tukitoa *time it means* tunamfunga. Swali langu ni kwamba, ikiwa kuna kampuni ambazo zimeshaonekana tokea mwanzo

kwamba shughuli zake ni kubwa zaidi, kwa nini tutoe *45 days* ambazo tunahisi zitakuwa ni kidogo?

**MWENYEKITI*:*** Mheshimiwa Abubakary, sasa hivi tunatunga sheria, kwa hiyo, unaposimama unatushirikisha sote kwa kusoma pale mahali unapoona kuna tatizo ili sote tulione halafu tuone namna ya kwenda nalo. Kwa hiyo, nakuomba uende moja kwa moja kwenye kifungu husika utueleze ni mstari gani una tatizo nao na pendekezo lako ni nini?

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Kifungu cha 131 kinasema: *"Every insurer shall pay claims within forty five days …"* Sasa ikiwa *claim* haijakuwa *settled, the Commissioner may grant an extra time within which the claim shall be settled.*

Nilimuuliza Mheshimiwa Waziri kwa nini tuka-*grant an extra time*; haikutajwa hapa kwamba, *time* yenyewe iwe kwa mfano *20 days* au *three weeks*? Waziri alipokuja alisema kwamba, *insurers* wengine wana shughuli zao kubwa, kwa hiyo, *Commissioner* ndiyo anaweza aka-*access.* Sasa ikiwa *Commissioner* anaweza aka-*access* kwa sababu ya shughuli kubwa; kwa nini hapa mwanzo tukaweka *forty five days* wakati tunajua kwamba kuna *insurers* wengine shughuli zao ni kubwa ambazo zitahitaji *more than forty five days;* na je si kuwafunga *insurers* ambao wana shughuli kubwa?

**MWENYEKITI:** Kama nimekuelewa Mheshimiwa Abubakar, hoja yako ni kwamba, Kamishna naye apewe tarehe ya mwisho ya kushughulikia masuala haya.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wakati nilipokuwa najieleza labda Mheshimiwa Abubakar hakunielewa vizuri; ninachokisema ni kwamba, sheria ime-*provide* siku 45 kwa makampuni kuweza ku-*settle* ile bima ambayo mteja anapaswa kulipwa.

Vilevile inaweza ikatokezea kampuni ikawa na matatizo katika kipindi kile cha siku 45 ikashindwa kulipa, Kamishna anapaswa kuiita hiyo kampuni ili aelewe kwa nini hawakulipa *within 45 days*. Kamishna atawasikiliza, atalichunguza lile tatizo atawaambia okay, tatizo lako nimeliona ni *genuine*, nakupa *another seven days* au nakupa *another 14 days* uweze ku-*settle* hiyo Bima.

Hii ndiyo sheria ambayo tukasema kwamba, tusimfunge Kamishna kumuwekea *limit* kwa sababu kila kampuni inaweza ikaja na matatizo. Hatutegemei kwamba, makampuni yote yatakuwa yana matatizo hayataweza kulipa *within forty five days.* Tunarajia kwamba makampuni yataweza kulipa *within 45 days* kwa sababu ya hivi vipengele ambavyo tumeviweka sasa hivi, *supervision* itakuwa karibu zaidi. Kwa hiyo, tutaweza kuiona hii kampuni ya bima kama itakuwa na matatizo au haina. Kwa hiyo, tunasema kwamba, tumwachie Kamishna aweze ku-*determine* matatizo ya hiyo kampuni kwa nini imechelewa kulipa ili aweze ku-*access* ni siku ngapi za ziada aweze kuwapa wa-*settle*.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sisemi kwamba, Kamishna awekewe *limit*, lakini hapa tukiweka *maximum days* ambazo Kamishna anaweza akatoa; tukisema kwa mfano *maximum days* ni 30, Kamishna anaweza akatoa *seven days* au *14 days* anazosema au akatoa *20 days*; sasa mradi tu Kamishna anajua kwamba uwezo wake ni *30 days* mwisho ili kuwasaidia wananchi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Hoja ya Mheshimiwa ni kwamba, akiachiwa Kamishna afanye maamuzi yake anaweza akayafanya kwa tarehe ambayo haijulikani; anaweza akaongeza muda hata wa mwaka. Nafikiri ndiyo wasiwasi wa Mheshimiwa, kwa hiyo, mtu asipate malipo yake.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana labda unaelekea huko, mimi napata wasiwasi tutakapoweka *limit* ya Kamishna, *criteria* tuliyoitumia ni nini hasa tukisema tunataka kumwekea limit ya siku 30, 40, 60, miezi sita? Sisi tunachokisema, tumwache Kamishna ayasome mazingira ya ile kampuni halafu aweze ku-*determine.* Huo ndiyo wasiwasi wangu; hizi siku 45 tulizomwekea tumeweka baada ya kuona mlolongo mzima mtu anapopata ajali, traffic anakuwepo, *statement* ya *traffic*, tukajikuta kwamba tunahitaji *about 40 to 45 days.* Huu mlolongo unakwisha, lakini tuki-*upper limit* hii, mimi ninapata wasiwasi kwamba *criteria* ambazo tumetumia au *tangible parameters* ambazo tumezitumia zinanipa wasiwasi.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiacha hivi hivi ile ni *very effect* ya kutaka ku-*solve problem* iliyokuwa *created* katika sheria iliyopita, itakuwa bado tunaweka; kwa sababu hapa ni kwamba, hawa watu wataendelea kuteseka na sheria hii inawazuia *insurers* hawa wasiwatese Watanzania. Sasa ikiwa hakuna *limit, definitely* sheria iliyopita *it means* tuna-*incorporate* hapa katika kifungu hiki na hilo sio lengo la Bunge hili. (*Makofi*)

Tukiweka kifungu ambacho kina-*limit* uwezo wa Kamishna, hapo ndiyo tumeshaweza kuwasaidia Watanzania wetu na hayo ndiyo madhumuni makubwa ya sheria.

**MWENYEKITI:** Hoja ya Mheshimiwa Bakary, mimi nimemuelewa kama Mwenyekiti na nadhani nimemuelewa vizuri kwamba, kifungu hiki lengo lake ni kuzibana kampuni ili wanaostahili kulipwa walipwe ndani ya siku 45.

Hoja yake ni kwamba, ili lengo hilo likamilike lazima na Kamishna naye abanwe, hata kama ni kwa siku 45 nyingine au siku zozote nyingine, lakini lazima na yeye apewe ili lengo lile likamilike. Hebu tumsikilize Mheshimiwa Chenge kwanza.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa majumuisho uliyofanya sasa hivi; ni vizuri tu Serikali ikalitambua hili kama madhumuni ni kusaidia wateja wa bima, tumeanza na siku 45; mtu atakuuliza mmetumia *criteria* gani? Kwa hiyo, msingi tunaoutafuta na ndiyo hoja ya Mheshimiwa Abubakar

kwamba, ile *extension* ambayo inapendekezwa iombwe kwa Kamishna ni vyema nayo ikawekewa ukomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni rahisi sana kwa sababu Kamishna hawezi akapewa mamlaka ya kuongeza muda mrefu zaidi ya ule ambao umetajwa na sheria. Kwa maana hiyo, tunaweza tukasema nusu ya kipindi kile cha siku 45 au tukaheshimu msingi wa sheria ile ile yeye akabanwa kwa kipindi kisichozidi siku 45 tukawa tumemaliza.

Mimi nadhani tumwachie Waziri sasa aone uzito wa hoja hii ili aweze kuhitimisha, lakini kuiandika ni rahisi maana tunataka tuweke *sealing* ya muda huo; ni hicho tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Chenge, kwa mchango wako; umetusaidia sana. Sasa ngoja tusikilize upande wa Serikali, Mwanasheria Mkuu au Mheshimiwa Waziri.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nakubaliana na Mheshimiwa ni vizuri tuliangalie tena suala hilo. Mheshimiwa Waziri, ndiye anayeweza kusema kwamba ni siku ngapi tunazoweza kumpa Kamishna. Nakubaliana kabisa kwamba, labda *within 21 days* kitu kama hicho, lakini kwa kuwa Mheshimiwa ndiyo mwenye Muswada anaweza kusema ni siku ngapi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, sasa tumsikilize Mheshimiwa Waziri mwenye sheria yake.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Wengi wape, nakubaliana na ile *part* ya pili ya Mheshimiwa Chenge kwamba, Kamishna tusije tukampa siku zaidi ya sheria ilivyotoa, lakini nakubaliana kwamba na yeye asizidishe siku 45. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tunakubaliana hapa?

**MHE. GOSBERT B. BLANDES**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mimi ninapata shida kidogo, kwa sababu awamu ambayo tunayo hapa mbele yetu ya kutunga sheria hii sijui Mheshimiwa Waziri atafanyaje kuweka hayo marekebisho katika sheria hii; kwa sababu utaratibu unataka lazima ije *schedule of amendment*, sasa katika hili nilikuwa naomba mwongozo wako?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Blandes katika hatua hii ya Bunge Zima na kwa badiliko hili ambalo halibadilishi maana ya kifungu cha sheria, bali linahuisha kwa kuweka sawa sawa ili sheria ile iwe na maana kwa wananchi, hili tunakubali kama mtaafiki nitakapowahoji; kama hamtaafiki basi litakuwa suala lingine.

Ibara ya 132
ibara ya 133

ibara ya 134
ibara ya 135
ibara ya 136
ibara ya 137
ibara ya 138
ibara ya 139
ibara ya 140
ibara ya 141
ibara ya 142
ibara ya 143
ibara ya 144
ibara ya 145
ibara ya 146
ibara ya 147
ibara ya 148
ibara ya 149
ibara ya 150
ibara ya 151
ibara ya 152
ibara ya 153
ibara ya 154
ibara ya 155
ibara ya 156
ibara ya 157
ibara ya 158
ibara ya 159
ibara ya 160
ibara ya 161
ibara ya 162
ibara ya 163
ibara ya 164
ibara ya 165

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

ibara ya 166

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza hapa katika kifungu cha 166 kuna *General Penalty* inasema kwamba: *"Every person who acts in contravention of any of the provisions of this Act commits an offence and shall, where no punishment has been stipulated by any other section in this Act for that offence, on conviction be liable to a fine not exceeding five million shillings."*

Sasa nilisema kwamba, kifungu hiki ukikisoma pamoja na kifungu cha 131(3), ambapo huyu mtu baada ya kupewa siku 45 halafu na Kamishna akampa tena siku 45 tulizokubaliana hapa na ikawa bado hajatekeleza; atachukuliwa kwamba amefanya shughuli hii katika *bad faith*.

Sasa ikiwa mteja anadai kwa mfano milioni 30 na huyu *insurer* ameshawekwa katika *bad faith* na faini yake *is not exceeding five million*; je, hatuwafanyi *insurer* wote wasitekeleze kifungu cha 131 kwa sababu watapata *bad faith* ambayo watalipa shilingi milioni tu wakati yeye anadaiwa zaidi ya milioni; si kwamba tunafanya makusudi ili *insurer* aweze kuja katika kifungu 166?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nakielewa vizuri hiki kifungu cha 131(3), *bad faith* imekuwa *defined* hapa; ni kwamba, *an insurer's delay in the processing of a legitimate claim beyond a time period consistent with normal industry practice*.

Hilo ndiyo kosa ambalo linazungumziwa. Kwa hiyo, ni kuchelewa tu kulipa, ku-*process* yale malipo siyo kulipa malipo. Kwa hiyo, nadhani kosa hili siyo kubwa ni dogo, ndio sababu adhabu yake imewekwa isizidi shilingi milioni tano.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye katika kifungu hiki, lakini katika kifungu cha 166 ameambiwa kwamba, *penalty* yake itakuwa *not exceeding five million shillings,* haikuongezwa kwamba pamoja na zile fedha ambazo anadaiwa za msingi.

Kwa hiyo, *it means* kisheria madhali tumeshaandika hivi, huyu *insurer* atalipa *five million shillings* tu. Sasa mimi ninacho-*suggest* ni kwamba, *not exceeding five million plus* zile fedha ambazo mteja anadaiwa itakuwa ni *penalty* ya *delay* pamoja na zile fedha ambazo anadaiwa. *Otherwise,* hapa tutamwachia atakwenda zake tu baada ya kumlipa milioni tano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bakary, tusaidiane sote na Wanasheria mliomo humu tufungueni macho tuone. Hii ni g*eneral penalty; every person who acts in contravention of any of the provisions of this Act.* Kwa hiyo, ni *general* inazungumzia mambo mbalimbali yaliyomo ndani ya sheria hii.

Kwa hiyo, ukitaka tuongeze ile milioni tano, maana yake ukifanya chochote kinyume na sheria hii, faini yake ni mamilioni ya shilingi. Ndilo hilo unalisimamia Mheshimiwa Bakary kwamba, chochote kikiguswa kinyume cha hapa iwe ni mamilioni ya shilingi; ndiyo hoja yako? Hebu iweke vizuri.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, kifungu cha 131 kinasema kwamba, *claim beyond forty five days* na kama tulivyokubaliana hapa ni kwamba, ikiwa *within forty five days* haikuwa *settled;* kwa hiyo, Kamishna atakuwa na uwezo wa ku-*grant an extra forty five days*.

Endapo hizo *extra forty five days* zitakwisha na *insurer* hajalipa kwa mteja; *insurer* huyu atawekwa katika *bad faith.* Sasa *bad faith* adhabu yake ipo katika kifungu cha 166 na imesema kwamba, akipatikana na kosa hili la *bad faith* basi …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bakary, iko wapi *bad faith?* Hebu tusomee.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Kifungu cha 166 (1) kifungu cha kwanza.

**MWENYEKITI:** Kisome.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** *Every person who acts in contravention of any of the provisions of this Act commits an offence and shall, where no punishment has been stipulated by any other section in this Act for that offence, on conviction be liable to a fine not exceeding five million shillings.*

**MWENYEKITI:** Nilitaka uone kwamba, hilo neno *bad faith* wala halipo. Unaweza ukaendelea.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** *Bad faith* ipo kwa sababu kifungu cha 131 kinazungumzia *delay* hii ya *bad faith* ikiwa haikuwa *provided.* Naomba usome kifungu hicho.

**MWENYEKITI:** Nakubali kifungu 131 kimetaja hilo neon, lakini nilichotaka ni kwamba, kifungu cha 136 haikijataja neno hilo; endelea baada ya hapo.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana. Kifungu cha 131(4) kimetaja *the provisions of Section 166 shall apply to an insurer who engages in bad faith claim*. Kwa hiyo, hapa …

**MWENYEKITI:** Tunakubaliana kwamba, hilo lipo kama unavyolieleza. Ninachosema ni kwamba, 166 haipo kama unavyoieleza. Endelea kuanzia hapo.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imo kwa sababu kijifungu cha (4) kime-*refer* kifungu namba 166, vinatakiwa visomwe kwa pamoja. Ina-*refer the provisions of section 166 shall apply to an insurer who engages in a bad faith claim.*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Karibu Mheshimiwa Andrew Chenge, kabla ya Mwanasheria Mkuu.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mwanasheria mwenzangu, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary kwa hili; lakini nifafanue kitu kimoja kwamba; kifungu cha 131(4) kinaturejesha kwenye kifungu cha 166 kwa Kampuni ya Bima ambayo imeshindwa kumlipa mteja wake ndani ya kipindi ambacho kimetajwa na Sheria ni kosa la jinai na kama atapatikana na hatia ndiyo adhabu inayosema isizidi shilingi milioni tano.

Sasa sote tunafahamu kwamba, faini hizi za Mahakama zinakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, haziendi kwa wateja wa Bima. Haki ya mteja wa Bima kwa mkataba wake ipo palepale dhidi ya kampuni hiyo ya Bima.

Kwa hiyo, ataendelea kudai lakini sisi tutamtafuta huyu kwa sababu amekiuka Sheria na ni lazima ashughulikiwe. Kwa hiyo, anashughulikiwa lakini madai chini ya *policy* yake yanabaki palepale. Hiyo ndiyo tafsiri sahihi ya vifungu vyote hivi viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Andrew Chenge amechangia tu, sasa ni zamu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Chenge kwa ufafanuzi alioutoa; lakini bado nabakia palepale, kwa sababu huyu mtu anaonekana kwamba amekosa kwa ajili ya kushindwa ku-*process* malipo ya mteja wake kwa muda uliopangwa, lakini madai yake yapo palepale.

Kwa hiyo, nadhani hii adhabu iliyotolewa kwenye kifungu cha 166 kwa kosa hili inatosha kabisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimemuelewa vizuri sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary bado una maneno?

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno ninayo kwa sababu ninakubaliana sana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini ninachosema hiki kifungu cha 166 baada ya kuandikwa *not exceeding* 5,000,000; kuwe na *clause* inayosema kwamba hii haitazuia yule mteja kulipwa fedha zake ambazo anamdai *insurer*.

**MWENYEKITI:** Hebu rudia tena hapo?

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba, hapa *not exceeding 5,000,000* ni *penalty* ambayo inatolewa baada ya kufanya huyu insurer kuonesha *bad faith*. Akishamaliza hii, bado yule mteja anadai zile fedha ambazo anamdai *insurer*.

**MWENYEKITI:** Si ndivyo ilivyo?

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana iko mahali gani haikuandikwa?

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MWENYEKITI:** Ahsante sana nimekupata. Naomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali ufafanue tena ili baada ya hapo nilihoji Bunge.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzoni, hili linahusu juu ya *process* tu, lakini haki yake ya kupewa hela zake zile iko palepale, kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Chenge, ana mkataba, *Insurance Policy* kati yake na *insurer;* kwa hiyo, ana haki ya kwenda Mahakamani kama hakulipwa. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 167

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia Kanuni ya 88 ya Kanuni zetu za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 88(1) na (2), inahusu Muswada katika Kamati ya Bunge Zima, inasema hivi: "Mtoa hoja au Mbunge mwingine anayekusudia kuwasilisha mabadiliko katika Muswada unaojadiliwa, anaweza kumwomba Spika kwamba, hatua ya kuingia katika Kamati ya Bunge Zima iahirishwe hadi wakati atakaoutaja katika ombi lake na Spika atatoa uamuzi wake kadiri atakavyoona inafaa."

88(2) inasema kwamba: "Mabadiliko yote yaliyopendekezwa kufanyika katika Muswada wa Sheria sharti yawekwe katika jedwali la mabadiliko litakaloandaliwa kwa ajili hiyo na kugawiwa kwa Wabunge na katika kujadili na ama kuyapitisha au kutoyapitisha, vyovyote itakavyokuwa, mabadiliko hayo yatashughulikiwa kwa mpangilio utakaofuata na kwa kuzingatia mtiririko wa Ibara za Muswada wa Sheria unaohusika. "

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mara nyingine kwa sababu Bunge lako Tukufu hili linaongozwa na Kanuni ambazo tumejitungia sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ambayo tumeyafanya katika Muswada huu, nilisema kwamba ni kwenda kinyume kabisa na Kanuni za Bunge. Sasa naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Blandes wewe ni Mwanasheria, unazijua taratibu na unapaswa kuzijua vizuri zaidi, maana umeturudisha kwenye kifungu cha zamani na si hiki tunachokiongelea hivi sasa ambacho hakina mabadiliko. Kifungu kile ambacho tumemfunga *Commissioner* na yeye asiwe na zaidi ya siku 45 hakibadilishi maana ya kifungu kile.

Kwa hiyo, hapakuwa na sababu kubwa sana za kutaka jambo hili liwe limeletwa saa ishirini na nne au siku mbili au tatu kabla ya wakati huo.

Mwenyekiti akishaamua jambo unamheshimu, maana ana rungu lake. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 168

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 1
Jedwali la 2

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*
*(Bunge lilirudia)*

***Muswada wa Sheria ya Bima wa Mwaka 2009***
***(The Insurance Bill, 2009)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Bima, yaani *The Insurance Act, 2009* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa*
*Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hiyo, naomba kutangaza rasmi kwamba, Muswada huu wa Sheria ya Bima wa Mwaka 2009, yaani *The Insurance Bill, 2009* umepita katika hatua zake zote katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, utaendelea na mchakato uliobakia kwa ajili ya saini ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Baada ya hatua hiyo, naomba niwakumbushe tu kwamba, kesho kuna semina ambayo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, itaanza saa 3.30 juu ya alama, katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Sababu ya kuanza saa tatu na nusu juu ya alama ni kwamba, semina hii tofauti na nyingine zote zilizozoeleka, itatangazwa moja kwa moja redioni na TBC Taifa. Hivyo nawaomba sana, muwahi kufika kesho asubuhi saa tatu na nusu. Hayo ni mambo ya Mheshimiwa George Lubeleje.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile shughuli zilizokuwa zimepangwa kwenye *Order Paper* ya leo zote zimakamilika kama zilivyopangwa, naomba kuahirisha shughuli za Bunge hili hadi Jumatatu, saa tatu kamili asubuhi. (*Makofi*)

*(Saa 01.12 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 27 Aprili, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*